

Liahona

Maandiko Yanatafsiriwa Namna Gani? uk. 20

Kujifahamishana na
Mtume Wetu Mpya, Mzee
Ronald A. Rasband, uk. 12

Wamisionari
Wakubwa: Mmeitwa
Kuhudumu, uk. 26

Wakati Waume
Wanapotaabika na
Ponografia, Wake
Wanahitaji Uponyaji
Pia, uk. 34

Jifunze Kucheza
Wimbo wa Dini katika
Dakika 10, uk. 54





*“Kwani tazama, hivi ndivyo asema Bwana, nitakulinganisha, Ee nyumba ya Israeli, na mzeituni uliochukuliwa na mtu na akaulisha shambani mwake; . . .
“. . . Na heri nyinyi; kwani kwa sababu mmekuwa na bidii katika kutumikia na mimi katika shamba langu la mizabibu, na mmetii amri zangu, na kuniletea tena matunda ya kawaida, kwamba shamba langu sio bovu tena, na iliyo bovu imetupwa mbali, tazama mtapokea shangwe na mimi kwa sababu ya matunda ya shamba langu la mizabibu.”*

Yakobo 5:3, 75

Mizeituni, hulimwa kwa kiasi kikubwa sana katika nchi za Mediterania, ina historia ndefu sana katika maandiko, kutoka wakati ambapo njiwa alimletea Nuhu tawi la mzeituni, hadi wakati Mwokozi alipokuwa akifundisha katika Mlima wa Mizeituni, hadi Yakobo alipotoa mfano wa miti ya mizeituni.



UJUMBE

- 4 Ujumbe wa Urais wa Kwanza: Unabii na Ufunuo Binafsi**
Na Rais Henry B. Eyring
- 7 Ujumbe wa Mwalimu Mtembeleaji: Mabinti wa Baba yetu wa Milele**

MAKALA YA HABARI MAALUMU

- 12 Mzee Ronald A. Rasband: Kiongozi Mwenye Kipaji, Baba Mwenye Kujitua**
Na Mzee M. Russell Ballard
Mume na baba mwenye upendo, Mzee Rasband alikuza ujuzi wa uongozi kupitia miaka ya unasihi kutoka kwa viongozi wafanisi wa kibiashara na ukuhani.
- 18 Yeye ni Askofu?**
Na Patrick J. Cronin III
Nilielewa ni kwa nini hakuweza kuamini nilikuwa sasa nahudumu kama askofu. Miaka thelathini iliyopita nilikuwa mtu tofauti sana.

- 20 Tafsihi ya Maandiko: Hadi katika Lugha ya Moyo Wetu**
Na R. Val Johnson
Kusoma maandiko katika lugha yetu wenyewe ni kama kuja nyumbani kiroho.

- 26 Nyakati za Wamisionari Wakubwa**
Na Rais Russell M. Nelson
Tafadhali sali kuhusu hii nafasi ya kujenga nyakati zuri za wamisionari wakubwa pamoja.

- 28 Wamisionari Wakubwa: Hitajika, Barikiwa, na Pendwa**
Na Richard M. Romney
Wanandoa hugundua kuwa kuhudumu misheni ni rahisi, sio ghali sana, na kunafurahisha zaidi kuliko walivyokuwa wakidhani.

- 34 Wakati ambapo Pornografia Inaathiri Nyumba—Wake na Waume Wote Wanahitaji Kuponywa**
Jina limefichwa
Askofu anaeleza jinsi anavyo-wasaidia sio tu waume ambao wanapambana na pornografia bali pia wake zao, ambao vile vile wanahitaji uponyaji wa Mwokozi.

- 38 Walinzi Juu ya Mnara**
Imarisha kuelewa kwako kwa manabii kwa kujifunza jinsi wao ni kama walinzi juu ya minara.

IDARA

- 8 Tafakari: Je, Maelekezo Yanaleta Maana?**
Na Ruth Silver
- 9 Kuhudumia ndani ya Kanisa: Asante kwa Huduma Yako**
Jina limefichwa
- 10 Fasihi za Injili: Ukuhani: Nanga Imara**
Na Mzee L. Tom Perry
- 40 Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwisho**
- 80 Mpaka Tutakapokutana Tena: Kutafuta Karama za Kiroho**
Na Rais George Q. Cannon

KWENYE JALADA

Jalada la mbele na ndani ya jalada la nyuma: Picha na Les Nilson. Ndani ya Jalada la Mbele: Picha © RayTango/Thinkstock



44 Kutambua Vitu Bandia vya Shetani

Na Dennis C. Gaunt

Kwa kutafuta tofauti kati ya uongo wa Shetani na Mafundisho ya Kristo licha ya kufanana, tuta-kuwa na uwezo wa kutambua vitu bandia vya Shetani.

48 Maelezo Mafupi Kuhusu Vijana Wakubwa: Kupima Baraka huko, Madagaska

Na Mindy Anne Selu

Licha ya kuishi katika nchi yenye shida nyingi, Solofo Ravelojaona anahisi maisha yake yakiwa na baraka tele.



*Tazama
kama unaweza
kuiona Liahona
iliyofichwa
katika toleo hili.
Dokezo: Kufuata
dokezo hii,
fuata nabii.*

50 Kuwa Imara Kiroho: Kujenga Meli Isiyoweza Kuzamishwa
Na Mzee Dale G. Renlund
Kama ilivyo kwa meli kwa uangalifu lazima ijengwe ili iwe imara, sisi kila mmoja wetu anaweza kuwa imara kwa kufuata kanuni hizi nne.

54 Jifunze Kucheza Wimbo wa Kidini katika Dakika 10!
Na Daniel Carter

57 Msimamo wa Kuacha
Na Gretchen Blackburn
Ningefanya chochote ili niache kucheza kinanda, kwa hivyo wakati wazazi wangu waliposema ningeweza kuacha ikiwa ningejifunza nyimbo 50 za kidini, nilianza.


58 Mshtuko Huzuni, na Mpango wa Mungu
Na Paola Çajupi
Nikikumbuka tukio lililolibananga zaidi maishani mwangu, hivi sasa ninajua kwamba Baba wa Mbinguni alikuwa nami wakati huo wote.

60 Hata Kama Unaona Haya
Na Mzee José A. Teixeira
Mwamini Bwana na atakubariki katika juhudi zako za kueneza injili.

62 Nafasi Yetu

63 Bango: Linaonekana Zuri?

64 Maswali na Majibu
Ninafanyiwa kejeli shuleni kwa kuwa MSM. Ninajua ninapaswa kutetea ninachoamini lakini ni vigumu sana! Ni namna gani naweza kuwa mjasiri vya kutosha?



66 Majibu kutoka kwa Mtume: Je, Mitume hufanya nini?
Na Mzee David A. Bednar

67 Amani Moyoni Mwangu
Na Carol F. McConkie
Nilipomwona nabii na kumsikiliza akizungumza, nilijisikia amani.

68 Ushuhuda wa Ethan
Na Larry Hiller
Ilionekana kana kwamba kila mtu isipokuwa Ethan alikuwa na ushuhuda.

70 Pesa za Baba wa Mbinguni
Na Angela Peña Dahle
Bila ya Pesa kusalia, Ana aliwaza, "Tutakula nini kesho?"

72 Kuwafuata Manabii na Mitume
Na Jenna Koford
Ni kwa njia gani unaweza kumfuata nabii mwezi huu.

74 Mashujaa wa Kitabu cha Mormoni: Alma Alitubu

75 Ninaweza Kusoma Kitabu cha Mormoni?

76 Hadithi za Kitabu cha Mormoni: Alma Anabatiza Watu Wengi

79 Ukurasa wa Kupaka Rangi: Sabato ni Siku Maalum

Gazeti la Kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Urais wa Kwanza: Thomas S. Monson, Henry B. Eyring, Dieter F. Uchtdorf

Akidi ya Mitume Kumi na Wawili: Boyd K. Packer, L. Tom Perry, Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, M. Russell Ballard, Richard G. Scott, Robert D. Hales, Jeffrey R. Holland, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd Christofferson, Neil L. Andersen, Ronald A. Rasband, Gary E. Stevenson, Dale G. Renlund

Mhariri: Joseph W. Sitati

Wahariri Wasaidizi: James B. Martino, Carol F. McConkie

Washauri: Brian K. Ashton, Randall K. Bennett, Craig A. Cardon, Cheryl A. Esplin, Christoffel Golden, Douglas D. Holmes, Larry R. Lawrence, Carole M. Stephens

Mkurugenzi Mwendeshaji: David T. Warner

Mkurugenzi wa Utendaji: Vincent A. Vaughn

Mkurugenzi wa Magazeti ya Kanisa: Allan R. Loyborg

Meneja wa Biashara: Garff Cannon

Mhariri Mtendaji: R. Val Johnson

Meneja Msaidizi wa Uhariri: Ryan Carr

Msaidizi wa Uchapishaji: Megan VerHoef

Kuandika na Kuhariri: Brittany Beattie, David Dickson, David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Lori Fuller, Garrett H. Garff, LaRene Porter Gaunt, Jill Hacking, Charlotte Larcabal, Michael R. Morris, Sally Johnson Odekirk, Joshua J. Perkey, Jan Pinborough, Richard M. Romney, Mindy Anne Selu, Paul VanDenBerghe, Marissa Widdison

Mkurugenzi Mtendaji Sanaa: J. Scott Knudsen

Mkurugenzi wa Sanaa: Tadd R. Peterson

Usanifu: Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, Mandie M. Bentley, C. Kimball Bott, Thomas Child, Nate Gines, Colleen Hinckley, Eric P. Johnsen, Susan Lofgren, Scott M. Mooy, Mark W. Robison, Brad Teare, K. Nicole Walkenhorst

Mratibu wa Haki Miliki: Collette Nebeker Aune

Meneja wa Uzalishaji: Jane Ann Peters

Uzalishaji: Connie Bowthorpe Bridge, Julie Burdett,

Katie Duncan, Bryan W. Gygi, Denise Kirby, Ginny J. Nilson, Gayle Tate Rafferty

Kabla ya Chapa: Jeff L. Martin

Mkurugenzi wa Uchapishaji: Craig K. Sedgwick

Mkurugenzi wa Usambasaji: Stephen R. Christiansen

Kwa manunuzi na bei nje ya Marekani na Kanada, nenda store.lds.org au wasiliana na kituo cha usambasaji cha Kanisa ama kiongozi wa kata au tawi.

Wasilisha miswaada na maswali katika mtandao liahona.lds.org; kwa barua pepe liahona@ldschurch.org ama barua *Liahona*, Rm. 2420, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150-0024, USA.

Liahona (neni katika Kitabu cha Mormoni linalomaanisha "dira" ama "kielekezo") imechapishwa katika Kialbeni, Kiarmeni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisebuano, Kichina, Kichina (Kilichorahisishwa), Kikroesia, Kicheki, Kidenshi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kijiji, Kifinisi, Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kianguya, Kiaislandi, Kiindonesia, Kiitaliano, Kijapani, Kikiribati, Kikorea, Kilatvia, Kilithuania, Kimalagasi, Kimarshalizi, Kimongolia, Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamoa, Kislovenia, Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalogi, Kitahiti, Kithai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietnamu. (Masafa hutofautiana kwa lugha.)

© 2016 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa imechapishwa Marekani.

Nakala na nyenzo za picha katika *Liahona* zinaweza kunakiliwa kimuafaka, kwa matumizi yasiyo ya kibiashara ya kanisa au nyumbani. Nyenzo za picha hazivezi kunakiliwa kama vikwazo vimeelezwa katika laini ya sifa na mchoro. Maswali a haki ya kunakili yanapaswa kuelekezwa ofisi ya Intellectual Property, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150, USA; barua pepe: cor-intellectualproperty@ldschurch.org.

For Readers in the United States and Canada:

April 2016 Vol. 3 No. 1. LIAHONA (USPS 311-480) Swahili (ISSN 2326-3695) is published once a year (April) by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA subscription price is \$1.00 per year; Canada, \$1.20 plus applicable taxes. Periodicals Postage Paid at Salt Lake City, Utah. Sixty days' notice required for change of address. Include address label from a recent issue; old and new address *must* be included. Send USA and Canadian subscriptions to Salt Lake Distribution Center at address below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit card orders (American Express, Discover, MasterCard, Visa) may be taken by phone or at store.lds.org. (Canada Post Information: Publication Agreement #40017431)

POSTMASTER: Send all UAA to CFS (see DMM 507.1.5.2). NONPOSTAL AND MILITARY FACILITIES: Send address changes to Distribution Services, Church Magazines, P.O. Box 26368, Salt Lake City, UT 84126-0368, USA.

Mawazo kwa ajili ya Jioni ya Familia Nyumbani

Toleo hili lina makala na shughuli ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya jioni ya familia nyumbani. Ufuatao ni mfano mmoja.



"Hata Kama Unaona Haya," ukurasa wa 60: Unaweza kuitumia jioni ya familia nyumbani kufundisha injili! Jadilianeni kama familia ni hofu ipi inayofanya uone vigumu kushirikiana na wengine injili na kisha ombeni juu ya mtu wa kumwalika kwenye jioni ya familia. Fikiria kumwalika kila mwana familia kutoa ushuhuda wakati wa somo. Unaweza kuchagua kufundisha somo juu ya Urejesho au mpango wa wokovu. Fikirieni kuandika mliyoyafanya na hisia zenu katika shajara zenu.

ZAIDI KWENYE MTANDAO

Liahona na nyenzo zingine za Kanisa zinapatikana katika lugha nyingi katika languages.lds.org. Tembelea [facebook.com/liahona.magazine](https://www.facebook.com/liahona.magazine) (Inapatikana kwa Kiingereza, Kireno, na Kihispania) kupata ujumbe wa kutia msukumo, dhana za jioni ya familia nyumbani, na mambo mengine ambayo unaweza kuwafundisha marafiki na familia yako.

MADA KATIKA TOLEO HILI

Nambari zinawakilisha ukurasa wa kwanza wa makala.

Amani, 50, 67

Amri, 8, 72

Asili ya Kiungu, 7

Bandia, 44, 63

Huduma, 9, 26, 28, 41

Huzuni, 58

Imani, 34, 48, 58, 60

Karama za kiroho, 80

Kazi ya umisionari, 26, 28, 60

Kitabu cha Mormoni, 43, 44

Kufundisha, 75

Maandiko, 20

Manabii na Mitume, 10,

12, 66, 67, 72

Msamaha, 34

Muziki, 54, 57

Pornografia, 34

Roho Mtakatifu, 44, 50

Sala, 41, 64

Siku ya Sabato, 79

Talanta, 40, 54

Toba, 18, 74

Ualimu wa kutembelea, 9

Uaminifu, 62

Ubatizo, 75, 76

Ufuasi, 12, 26

Ufunuo, 4, 10, 20, 41, 42,

50, 70, 72

Uhudhuriaji kamili, 18

Ujasiri, 48, 64

Uongofu, 43, 58, 75, 76

Upatanisho, 34

Upendo, 40

Ushuhuda, 64, 68

Utiifu, 8, 34, 62, 72

Wito, 18

Yesu Kristo, 20, 34, 43, 58

Zaka, 62, 70



**Na Rais
Henry B. Eyring**

Mshauri wa Kwanza
katika Urais wa
Kwanza

Unabii

NA

UFUNUO BINAFSI

Kanisa la Yesu Kristo la kweli limerejeshwa na liko duniani hivi leo. Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho daima limekuwa likiongozwa na manabii na mitume walio hai, ambao hupokea mwongozo siku zote kutoka mbinguni.

Mfumo huo mtakatifu pia ulikuwa wa kweli siku za kale. Tunajifunza katika Biblia: “Hakika Bwana Mungu hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake” (Amosi 3:7).

Mungu amezungumza tena katika siku zetu, kupitia Nabii Joseph Smith. Alifunua kupitia Nabii Joseph Smith Injili ya Yesu Kristo katika utimilifu wake. Alirejesha ukuhani wake mtakatifu na funguo na haki zote, nguvu, na kazi za nguvu takatifu za ukuhani.

Katika siku zetu, manabii na mitume walio hai wanayo mamlaka ya kuzungumza, kufundisha, na kuongoza kwa mamlaka kutoka kwa Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo. Mwokozi alimwambia Nabii, “Kile ambacho Mimi Bwana nimesema, nimekisema, na wala sijitii, na ingawa mbingu na dunia zitapita, neno langu halitapita kamwe, bali litatimia, iwe kwa sauti yangu mwenyewe au kwa sauti ya watumishi wangu, yote ni sawa” (M&M 1:38).

Katika mkutano mkuu mara mbili kwa mwaka, tunabarikiwa na nafasi ya kusikiliza neno la Bwana yetu kutoka watumishi Wake. Hii ni fadhila kuu sana. Lakini thamani ya fursa hiyo hutegemea kama tunapokea maneno yao chini ya ushawishi wa yule Roho ambaye alitolewa kwa

watumishi wale (ona M&M 50:19–22). Kama vile ambavyo wao wanapokea mwongozo kutoka Mbinguni, na sisi lazima iwe vivyo hivyo. Na hivyo huhitajika kutoka kwetu juhudi za kiroho sawa sawa na hizo.

“Fanya Maandalizi”

Miaka kadhaa iliyopita mmoja wa washiriki wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili aliniomba nisome hotuba ambayo alikuwa akitayarisha kwa ajili ya mkutano mkuu. Nilikuwa mshiriki mdogo wa akidi. Ilikuwa heshima kubwa kwangu kwa sababu ya imani yake kwangu kuwa ningeweza kumsaidia kutafuta maneno ambayo Bwana angemtaka azungumze. Aliniambia huku akitabasamu, “Oh, hii ni rasimu ya 22 ya hotuba.”

Nilikumbuka ushauri wa mpendwa na mkarimu Rais Harold B. Lee (1899–1973) aliokuwa amenipa mapema kwa msisitizo mkubwa: “Hal, ukitaka kupokea ufunuo, fanya maandalizi.”

Nilisoma, nilitafakari, na kusali kuhusu ile rasimu ya 22. Niliisoma vyema kadiri iwezekanavyo chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Na wakati yule mshiriki wa ile akidi alipotoa hotuba yake, nilikuwa nimetimiza maandalizi yangu. Sina uhakika kama nilisaidia, lakini ninajua kwamba nilibadilika wakati niliposikiliza hotuba hiyo ikitolewa. Ujumbe ulionijia ni zaidi ya yale maneno ambayo nilikuwa nimeyasoma na yale aliyokuwa akiongea. Maneno hayo yalikuwa na maana kubwa zaidi kuliko yale niliyokuwa



nimesoma kwenye rasimu. Na ujumbe ulionekana ulikusudiwa kwa ajili yangu, maalum kwa mahitaji yangu.

Watumishi wa Mungu hufunga na kusali ili wapokee ujumbe ambao Yeye anao ili wao wawape wale wanaohitaji ufunuo na maongozi. Kile ambacho nilijifunza kutoka tukio hilo, na matukio mengine mengi kama hayo, ni kuwa ili kupata manufaa makuu yanayoweza kupatikana kutokana na kuwasikiliza manabii na mitume walio hai, ni lazima tulipe gharama sisi wenyewe ya kupokea ufunuo.

Bwana anampenda kila mtu ambaye anaweza kusikiliza ujumbe Wake, na anajua mioyo na mazingira ya kila mmoja wetu. Anajua ni marekebisho gani, kuhamasisha gani, na ukweli upi wa injili utakuwa bora zaidi kumsaidia kila mmoja kuchagua njia yake katika safari hii ya kuelekea uzima wa milele.

Sisi ambao husikiliza na kutazama ujumbe wa mkutano mkuu mara nyingine hufikiria baadaye, “Ni kipi naweza kukumbuka vizuri sana? Matumaini ya Bwana kwa kila

mmoja wetu ni kwamba jibu letu litakuwa: “Sitaweza kamwe kusahau wakati ambapo niliisikia sauti ya Roho akilini mwangu na moyoni ikiniambia kile ambacho ningeweza kufanya kumridhisha Baba yangu wa Mbinguni.”

Tunaweza kupata ule ufunuo binafsi wakati tunapowasikiliza manabii na mitume na tunapojitahidi kwa imani kuupokea, kama vile Rais Lee alivyo-sema tunaweza. Ninajua kuwa hayo ni kweli kutokana na tukio hili na kulingana na ushuhuda wa Roho. ■

KUFUNDISHA KUTOKA KATIKA UJUMBE HUU

Fikiria kusoma kwa sauti kubwa simulizi ya Rais Eyring kuhusu kusoma rasimu ya hutoba ya mkutano mkuu ya mshiriki wa akidi yake. Waweza kujiuliza, “Gharama ya kupokea ufunuo ni nini?” Baada ya majadiliano

yenu, mwaweza kuwaalika wale ambao mnawatembelea kutafakari na kutekeleza mpango wa kupokea ujumbe wa mkutano mkuu ujao “chini ya ushawishi wa yule yule Roho ambaye ametolewa kwa watumishi wa [Mungu].”

Baba wa Mbinguni Amesema Nami kwa Njia ya Hotuba ya Mkutano Mkuu

Na Anne Laleska Alves de Souza

Nilikwa na shaka juu kuhusu kile nitasoma Chuo kikuu. Watu wengi walizungumza vibaya juu ya kozi ambayo nilitaka kuichukua, hivyo nikaomba kwa Bwana ili kuona kama Yeye alikubaliana na uamuzi wangu.

Jibu langu lilikuja siku iliyofuata wakati nikiwa nasoma mahubiri ya mkutano mkuu katika *Liahona*. Nilijisikia kana kwamba Baba wa Mbinguni alikuwa akiniambia kwamba Yeye asingeweza kunichagulia—huu ulikuwa ni uamuzi wa kufanywa na mimi pekee yangu. Nilijua kwamba lolote nitakalochagua, nitapaswa kufanya kazi kwa bidii ili nifanikiwe.



Ninajua kuwa sala yangu ilijibiwa. Uthibitisho wa Roho Mtakatifu ulinisaidia kufanya uamuzi. Nimejifunza kutoa jitihada zangu zote na ninajua kwamba Baba wa Mbinguni atanisaidia.

Mwandishi anaishi Sergipe, Brazili.

WATOTO

Kumfuata Nabii.

Manabii na mitume huna nena kwa niaba ya Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Wao hutufundisha namna ya kumfuata Yesu. Fuata njia ili upate baadhi ya vitu ambavyo nabii na mitume wametugiza sisi tufanye.



Kwa maombi jifunze maneno haya na utafute kujua kitu cha kufundisha. Ni jinsi gani kuelewa “Familia: Tangazo kwa Ulimwengu” kutazidisha imani yako kwa Mungu na kubariki wale unaowachunga kupitia Ualimu wa Kutembelea? Kwa taarifa zaidi, nenda kwenye reliefsociety.lds.org.

Mabinti wa Baba yetu wa Milele

Maandiko yanatufundisha kuwa “sisi tu wazao wa Mungu” (Matendo ya Mitume 17:29). Mungu alimtaja Emma Smith, mke wa Nabii Joseph Smith kama, “binti yangu” (M&M 25:1). Tangazo la familia lina-tufundisha kuwa kila mmoja wetu “ni binti mpendwa wa kiroho . . . wa wazazi wa mbinguni.”¹

“Katika maisha [kabila ya kuzaliwa], tulijifunza kuhusu utambulisho wetu wa milele wa kike,” alisema Carole M. Stephens, Mshauri wa Kwanza katika Urais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama.

“Safari yetu duniani haikubadilisha kweli hizo.”²

“Baba yako wa Mbinguni anajua jina lako na anajua mazingira yako,” alisema Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili. “Yeye husikia maombi yako. Anajua matumaini na ndoto zako, pamoja na hofu yako na kuvunjwa moyo kwako.”³

“Kila mmoja wetu ni wa familia ya Mungu na anahitajika katika



familia hiyo ya Mungu,” alisema Dada Stephens. “Familia za duniani zote zinaonekana kuwa tofauti. Na tunapofanya vyema kadiri tuwezavyo kuunda familia za kawaida zilizo imara, ushiriki katika familia ya Mungu hautegemei hadhi ya aina yoyote—hali ya ndoa, hali ya uzazi, hali ya kifedha, hali ya kijamii, au hata aina yoyote ya hali tunayoweka kwenye mtandao wa kijamii.”⁴

Maandiko ya Ziada

Yeremia 1:5; Warumi 8:16; Mafundisho na Maagano 76:23–24

MUHTASARI

1. “Familia: Tangazo kwa Ulimwengu,” *Liahona*, Nov. 2010, 129.
2. Carole M. Stephens, “Familia ni ya Mungu,” *Liahona*, Mei 2015, 11.
3. Jeffrey R. Holland, “Kwa Wasichana,” *Liahona*, Nov. 2005, 28.
4. Carole M. Stephens, “Familia Inatoka kwa Mungu,” 11.
5. Ona Mada ya Injili, “Historia ya Ono la Kwanza,” topics.lds.org

Fikiria Hili

Ni jinsi gani kujua wewe ni binti ya Mungu huathiri uamuzi wako?

Imani, Familia, Usaidizi



Kutoka katika Historia Yetu

Katika Historia yake ya Ono la Kwanza,⁵ Nabii Joseph Smith anathibitisha ukweli mwingi—ikijumuisha kwamba Baba wa Mbinguni anajua majina yetu.

Kijana Joseph alihangaika ili apate kujua ni kanisa gani angeji-unga nalo na alipata mwongozo katika Yakobo 1:5. Joseph alihitimisha kwamba angemwomba Mungu.

Asubuhi moja wakati wa majira ya kuchipua mwaka wa 1820, alienda msituni kuomba lakini mara akashikwa na nguvu fulani za giza. Juu ya haya aliandika:

“Katika wakati huu wa hofu kubwa, niliona nguzo ya mwanga juu ya kichwa changu, ambao ulikuwa na mng’aro uliozidi mwangaza wa jua, ambao ulishuka taratibu hadi ukashuka juu yangu.

“Mara ulipoonekana nilijikuta kuwa nimekombolewa kutokana na adui yule aliyenifunga. Mwanga ulipotua juu yangu nikawaona Viumbe wawili, ambao mng’aro na utukufu wao wapita maelezo yote, wakiwa wamesimama juu yangu angani. Mmoja wao akaniambia, akiniita mimi kwa jina na kusema, huku akimwonyesha yule mwingine—*Huyu ni Mwanangu Mpendwa. Msikilize Yeye!*” (Joseph Smith—Historia 1:16–17).

JE, MAELEKEZO YANALETA MAANA

Na Ruth Silver

Safari kwa baiskeli ilinshawishi juu ya haja ya kuangalia mara kwa mara ramani ya barabara ya maisha.

Miaka kadhaa iliyopita nilienda safari ya baiskeli kule Ufaransa pamoja na dadangu, shemeji yangu, na binti yake. Kila asubuhi tulipewa kurasa tatu zilizokuwa na maelezo ya kina ambayo, ikiwa yangefuatwa sawasawa, yangetuongoza hadi mwisho wa safari ya siku hiyo. Tulipokuwa tukendesha baiskeli kupitia mashamba ya mizabibu, maelekezo yangetuelekeza, “nenda futi 165 (50 m) Kaskazini, kisha geuka upande wa kushoto na uende futi 330 (100 m).” Mara nyingi, maelekezo yalitupa ishara na majina ya barabara.

Asubuhi moja tuliendesha baiskeli kwenye barabara ya kuvutia lakini punde tukagundua ya kwamba maelekezo yetu hayakuwa yanalingana na eneo hilo. Tukiwa tunapotea kwa haraka sana, tuliamua kurudi mahali ambapo tulijua kuwa tulikuwa kwenye barabara sahihi ili kuona ikiwa tungeweza kutatua ni wapi tungeenda.

Kwa uhakika, tulipofika pale, tuliona ishara ndogo ya barabarani, ilioonyeshwa kwenye maelekezo yetu,

ambayo tulikosa kuiona. Punde tulikuwa njiani tena, tukilinganisha mwendo wetu na maelekezo, ambayo tena yalikuwa yanaleta maana kamilifu.

Tukio hilo lilikuwa kama sitari ambayo ilijibu swali la kutatanisha nililokuwa nalo: Kwa nini, wakati ambapo mtu ameisha kuwa na ushuhuda kuhusu injili, anawezaje kupotea njia tena? Ilikuwa wazi kwangu kuwa tunapochukua hatua mbaya (dhambi) au kukosa kufuata amri za Mungu, maelekezo (neni la Mungu) hayaleti maana tena. Ramani, kama ilivyokuwa, hailingani na eneo tulilokuwemo. Ikiwa hatujapotea mbali sana, tunaweza kugundua kwamba makosa ni yetu na kuwa tunahitaji kurudi (kutubu) au kuahidi tena kuishi jinsi ambavyo Mungu ametuamuru mahali ambapo tulijua tulikuwa kwenye njia sahihi.

Mara nyingi sana wakati maelekezo hayalingani na mahali tulipo, tunakuwa na shaka kuhusu maelekezo. Badala ya kurudi nyuma, tunalaumu maelekezo na kisha kuyaacha kabisa. Hatimaye, tukiwa tumepoteza ono la

mwisho wa safari yetu, tunapotea, tukizurura katika njia ambazo zinaweza kuonekana, kwa muda, za kuvutia mno lakini hazitatufikisha mahali ambapo tunahitaji kwenda.

Kila siku tunayo fursa ya kusoma maandiko. Na kila miezi sita, tuna mkutano mkuu wa Kanisa. Je, hizi sio nyakati ambazo tunaweza kuangalia ramani zetu za barabara na kuhakikisha kuwa tuko mahali ambapo tunahitaji kuwa? Wakati mmoja, nilipokuwa nikisikiliza mkutano, nilihisi kuwa, licha ya mapungufu tuliyonayo, tunaweza kujua tuko kwenye njia sahihi ikiwa maelekezo haya yanaleta maana kamilifu kwetu.

Jinsi ambavyo kufuata mwelekeo sahihi kutatufikisha mwisho wa safari zetu maishani, kusoma maandiko na kutii ushauri wa manabii walio hai huturuhusu sisi kuangalia njia yetu na kurekebisha pale inapohitajika ili, hatimaye, tuwasili nyumbani kwetu mbinguni. ■

Mwandishi, ambaye aliishi Colorado, Marekani, aliaga duniani mwaka jana.



ASANTE KWA HUDUMA YAKO

Jina limefichwa

Wewe ni mfano wa wale wanawake ambao, tangu siku za Nauvoo, wametumikiana wao kwa wao kupitia ualimu wa kutembelea kwa upendo na kuinuana.

Sijui jina lako, una umri gani, wala Sijui cho chote juu yako. Ninachokijua tu ni kwamba wewe ni mwalimu wa kutembelea Joann, na ninakushukuru kwa moyo wangu wote kwa huduma yako yenye kujali.

Ninajua kwamba kumtembelea dada asiye hudhuria kanisani kama Joann (jina halisi limebadilishwa), binti mkwe wangu, siyo rahisi, hususani pale anapokuwa si mkarimu. Ni na shaka hata kama alitaka umtembelee kwanza. Lakini Joann ameniambia kwamba wewe umekuwa rafiki wa kweli kwake, ukipita kumjulua hali na kumkubali yeye kama alivyo.

Katika miaka 19 tangu Joann aolewe na mwanangu, hii ni mara ya kwanza yeye kutamka kuwa anaye mwalimu mtembeleaji. Hivi karibuni ameniambia jinsi unavyomtembelea mara kwa mara na jinsi unavyomjali na mkarimu daima. Ameniambia umemsaidia mara nyingi wakati alipokuwa mgonjwa na hata umeomba umpeleke mjukuu wangu kwenye darasa la wasichana.

Kwa miaka 10 iliyopita, yeye, mwanangu, na familia yao wameishi umbali wa mamia ya maili kutoka kwetu. Nimekuwa nikiomba kwamba watu wengine wawapende na kuwajali kama mimi nifanyavyo, na



nimeomboleza kwa machozi kwa Baba wa Mbinguni kwamba wengine wawafikie kama ambavyo mimi ningefanya kama wangeishi jirani na sisi. Kutokana na kile asemacho Joann wewe umekuwa jibu la maombi yangu.

Hata kama Joann na mwanangu hawatii Neno la Hekima na hawahudhuria kanisani, bado wao ni watu wema na wanawependa watoto wao. Kwa namna fulani macho yako hayakugubikwa na moshi wa sigara ya Joann. Ukumhukumu yeye kama atahudhuria kanisa au la. Uliweza kumjua na kujifunza kuwa yeye ni mama mwenye upendo ambaye anataka binti yake ahudhurie kanisa na kupata ushuhuda.

Na Joann alipofanyiwa upasuaji, ulimletea chakula badala ya kushangaa na kuwaza kuwa labda amejiletea mwenyewe matatizo hayo ya kiafya.

Ni shukrani iliyoje kwangu kwamba wewe umekuwa mfano kwa binti-mkwe wangu huyu. Anaweza kuiga mfano wako huu kama mtu anayemjali kila mtu na mwenye kujitolea kuonyesha upendo. Aliniambia kwamba siku moja ulipokuwa huna gari, ulitembea kwa miguu zaidi ya maili moja kwenda nyumbani kwake pamoja na watoto

wako kumpelekea biskuti.

“Nimekuwa nikikuwaza wewe na mama yako na nilitamani kufanya kitu kizuri kwa ajili yenu—kwa sababu tu,” ulimwambia.

Natamani ningeweza kukuambia ni kiasi gani ninashukuru kwa kujitolea kwako katika wito wako kama mwalimu wa kutembelea. Wewe ni mfano wa wale wanawake ambao, tangu siku zile za Nauvoo, wametumikiana wao kwa wao kupitia ualimu wa kutembelea kwa upendo na kuinuana. Umeonyesha huduma na upendo huo kwa namna uliyomtembelea kwa upendo binti-mkwe wangu asiyehudhuria kikamilifu kanisani.

Asante. ■



**Na Mzee
L. Tom Perry
(1922–2015)**

Wa Akidi ya Mitume
Kumi na Wawili

UKUHANI: NANGA IMARA

Makala haya yalitayarishwa na Mzee L. Tom Perry mnamo Mei 28, 2015, siku mbili tu kabla ya kuaga dunia, yalikuwa yashirikishwe kwa mwenye ukuhani vijana.

Nguvu kubwa katika maisha yangu imekuwa ukuhani wa Mungu. Ninaamini utakuwa nanga imara pia kwenu ninyi vijana wa kiume. Lakini ili upate kuwa na nguvu katika maisha yenu, unahitaji kuelewa na kuutumia.

Uzoefu wa awali na Ukuhani

Nimekuwa katika mazingira mazuri huko Logan, Utah. Sikuwa na hofu ya kukosa chakula au nyumba wala elimu. Lakini pengine kwa sababu maisha yalikuwa rahisi, nilihitaji kitu cha kushikilia ambacho ningekitegemea kama nanga.

Kwangu mimi nanga hiyo ilikuwa ni ukuhani wa Mungu. Nilikuwa katika hali isiyo ya kawaida wakati nikikua. Baba yangu alitwa kuwa askofu wakati nilipokuwa na umri wa mwaka mmoja, na aliendelea kuwa askofu wangu kwa miaka 19. Mwongozo wa ki-baba na wa kiroho ulikuwa msaada mkubwa sana kwangu.

Nadhani hii ndiyo sababu hasa kwa nini nilitarajia kupokea Ukuhani wa Haruni siku ya mwaka wa 12 wa

kuzaliwa kwangu. Ninakumbuka siku hiyo maalumu niliisikia mikono ya baba yangu juu ya kichwa changu aki-nitawaza. Baada ya hapo, niliendelea kupitia ofisi zote za Ukuhani wa Haruni na kupokea miito niliyoipenda sana.

Kupitisha sakramenti ilikuwa kitu maalum sana kwangu. Ungeweza kuona watu wakiweka ahadi wenyewe ya kumtii Bwana na kushika amri zake wakati wakipokea ishara za mwili Wake na damu Yake.

Kukua katika Uelewa wa Ukuhani

Kadiri muda ulivyokuwa ukisonga, nilihitimu kutoka sekondari, na kisha baada ya mwaka mmoja chuoni, niliitwa kwenda misheni. Nilifurahia kila dakika ya misheni na niliwapenda wenzi wangu. Hususani mmoja ambaye alikuwa nguvu yangu. Nili-jifunza mengi kutoka kwake wakati tukitimiza majukumu yetu.

Kwa sababu nchi ilikuwa vitani, niliporejea kutoka misheni nilijiunga na Jeshi la Marini la Marekani. Vita vilipomalizika, nilirejea chuoni, nikaoa, na kuanza familia. Uhamaji wa mara kwa mara kikazi ulinipeleka sehemu nyingi za Amerika, sehemu ambazo nilijifunza mengi nikitumikia katika miito mingi ya ukuhani. Hatimaye nikatua Boston, Massachusetts, ambako nilitumikia

kama rais wa kigingi. Ilikuwa kutokea hapo ndipo nilipoitwa kuwa msaidizi wa Wale Kumi na Wawili na halafu, baada ya miezi 17, kwenye Akidi ya Mitume Kumi na Wawili.

Mambo Niliyojifunza kama Mtume

Nimejifunza nini kama mshiriki wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili?

Nimejifunza kuwa kuna mwongozo, nanga, na ulinzi katika ukuhani.

Ukuhani daima umekuwepo. Kabla Adamu hajaja duniani, alikuwa na ukuhani. Kadiri uzao wa Adamu ulivyokuwa ukisambaa pamoja na ukuhani, ilionekana kuwa ni muhimu kuweka utaratibu wa namna ya kutawala ukuhani. Bwana alifanya hivyo kwa kumwita Ibrahimu kuwa kiongozi





wa wenye ukuhani katika familia yake. Utaratibu huu uliendelea chini ya Isaka na Yakobo, ambaye jina lake baadae likabadilishwa kuwa Israeli.

Karne kadhaa baadae, wana wa Israeli walijikuta wenyewe utumwani. Bwana alimtuma Musa kuwakomboa, lakini alipofanya hivyo, walijithibitisha wenyewe hawakuwa tayari kama watu kwa Ukuhani wa Melkizedeki. Hivyo wakabakiziwa Ukuhani wa Haruni hadi wakati wa Mwokozi.

Ninaona ni kitu cha kufurahisha sana kile ambacho Mwokozi alikifanya kwanza alipokuwa anaanza huduma Yake. Alianzisha Ukuhani wa Melkizedeki. Akawaita Mitume kumi na wawili na akawafundisha sheria na taratibu za ukuhani. Alimwita Petro kuwa Mtume kiongozi, akianzisha safu ya mamlaka

katika Kanisa Lake. Katika siku ile na siku hii, ni Yesu Kristo ndiye anayemteua Mtume kiongozi Wake ili kuwa kiongozi juu ya Kanisa, na ni Mwokozi ndiye anayemwelekeza yeye katika kazi zake za ukuhani.

Hivyo ukuhani una safu ya moja kwa moja kutoka kwa Bwana na Mwokozi wetu kupitia kwa Mtume kiongozi hadi kwa Mitume wengine na kuendelea kwa makuhani wengine katika Kanisa. Funguo za mamlaka zimetolewa kwa Mitume, na ilimradi funguo hizo ziko duniani, tutaongozwa na Bwana Mwenyewe. Mwingozo huu wa kiungu hutulinda na kututhibitisha kwamba Kanisa halitapotoka mbali na ukweli. Litabaki imara kwa sababu haliongozwi na kiumbe ye yote wa duniani. Linaongozwa na Bwana.

Jifunzeni Mafundisho ya Ukuhani

Ushauri mkubwa kabisa ninaowapa ninyi vijana wa kiume ni kujifunza mafundisho ya ukuhani, eleweni nguvu mliyonyo katika kutumia ukuhani wenu, na jifunzeni namna, inavyoweza kubariki maisha yenu na maisha ya wengine.

Ninakuahidini kama mtajifunza mafundisho ya ukuhani na kutimiza kazi zenu za ukuhani, ukuhani utakuwa nanga imara ambayo itawaweke salama kiroho na kuwaleteeni furaha tele. Kuweni akidi ya kweli ya ukuhani. Wasaidieni marafiki zenu na waleteni katika akidi zenu. Jengeni udugu katika akidi yenu ambayo itakuwa msingi imara kwa maisha yenu. ■

Mzee Ronald A. Rasband

KIONGOZI
MWENYE KIPAJI,
BABA MWAMINIFU

Na Mzee M. Russell Ballard

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Ron Rasband kamwe hakuwa na shaka kwamba angetumikia misheni. Swali pekee ambalo kijana huyu wa miaka 19 alikuwa nalo alipokuwa akifungua barua ya wito wake wa kutumikia kama mmisionari lilikuwa *ni wapi* anghudumu.

“Baba yangu alikwenda misheni huko Ujerumani. “Kaka yangu mkubwa alikwenda misheni huko Ujerumani. “Shemeji yangu mtarajiwa alikwenda misheni huko Ujerumani,” anakumbuka. “Nilidhani nilikuwa naenda Ujerumani.”

Lakini Bwana alikuwa na mipango tofauti. Badala yake, Ron alikuwa ameitwa, katika Misheni ya Eastern States, iliyokuwa na makao makuu yake kule Jijini New York, Marekani. Akiwa amesikitika, alichukua barua ya wito wake hadi chumba chake cha kulala, akapiga magoti kando ya kitanda chake, akaomba, bila mpangilio maalumu akafungua maandiko yake, na akaanza kusoma:

“Tazama, na lo, ninao watu wengi katika eneo hili, katika maeneo ya jirani; na mlango wenye kuleta matokeo yanayotakiwa utafunguliwa katika maeneo ya jirani katika *nchi za mashariki*.

“Kwa hiyo, Mimi, Bwana, nimewaruhusu ninyi kuja mahali hapa; na hivyo niliona ni muhimu kwa wokovu wa wanadamu” (M&M 100:3–4; mkazo umeongezwa).




Mara moja, Roho Mtakatifu akamthibitishia Ron kwamba wito wake katika Misheni ya Eastern States haukuwa makosa.

“Niligeuka kutoka kuwa mwenye masikitiko hadi kuwa na msukumo wangu wa kwanza kati ya misukumo mingi ya kimaandiko kuwa huko ndiko Bwana alikohitaji mimi niende,” anakumbuka. “Hilo lilikuwa tukio la muhimu sana kwangu.”

Misheni yake kule Eastern States ilikuwa ya kwanza kati ya miito kadhaa ya Kanisa ambayo ingempeleka sehemu ambazo kamwe hangetarajia kwenda. Na kila wito—kama mwalimu, askofu, mjumbe wa baraza kuu, rais

Juu Kulia: Mzee Ronald A. Rasband kama rais wa misheni kule Jijini New York 1998. Kulia kabisa: Mzee Rasband na Dada yake, Nancy Schindler; mama; na kaka zake, Russell na Neil. Kulia: Akiwa na wazazi wake kama mvulana wa miaka saba.



wa misheni, mshiriki wa Sabini, Rais Kiongozi wa Sabini, na Mtume wa Bwana Yesu Kristo—Mzee Ronald A. Rasband amekubali mapenzi ya Bwana na ameendelea kumtegemea Roho wake akiwa anawahudumia watoto wa Mungu.

Alizaliwa na Wazazi Wema

Katika Mahubiri yake kama Mtume wa Yesu Kristo, Mzee Rasband alionyesha shukrani zake za dhata kwa ukoo wake. “Nilizaliwa na wazazi wema katika injili,” alisema, “na wao pia walitokana na wazazi wema vizazi sita vilivyopita.”¹

Mama yake, Verda Anderson Rasband, alikuwa kiongozi mpendwa ambaye aliulea upendo wa maandiko wa kijana Ron. Baba yake, Rulon Hawkins Rasband, alikuwa mwenye ukuhani mwaminifu ambaye alionyesha mfano wa maadili ya kufanya kazi kwa bidii.

Alizaliwa Februari 6, 1951, jijini Salt Lake, Utah, Marekani, Ronald A. (Anderson) Rasband alikuwa mtoto wa pekee wa muungano wa wazazi wake. Wote wawili walikuwa wameshawahi fungua ndoa na kutalikiana, Ron alilelewa



lakini anakiri kuwa kwa upande mwingine alikuwa na utundu.

“Zaidi ya mara chache, walimu wangu [wa Msingi] walimwendea mama yangu, rais wa Msingi wa kigingi, na kusema, ‘Yule Ronnie Rasband ni mtoto mdogo mtukutu,’” anasema. “Lakini kamwe hawakufa moyo juu yangu.

Walinionyesha upendo mkubwa na kunialika tena darasani.”²

Kitovu cha utoto wa Ron kilikuwa Kanisa —mikutano ya kata, sherehe za kata, karamu za kata, na timu za michezo za kata. Wakati alipokuwa hana shughuli katika jumba la mikutano la Kata ya Kwanza ya Cottonwood, alikuwa anafanya vibarua, akifanya shughuli za maskauti, na akishinda na marafiki zake. Nyumbani, kitovu cha familia kilikuwa maandiko, michezo, na kazi za nyumbani.


Baba yangu alinifundisha kazi kwa njia ya mfano wake,” alisema. “Mama yangu alinifundisha kazi kwa kunifanya niifanye.”

Baba yake Ron aliendesha gari la kusambaza mikate, akiamka

chini ya utunzaji ulioongezeka wa kaka wawili wakubwa na dada mmoja mkubwa.

“Alikuwa kiunganishi cha wazazi wetu, kwa hivyo sisi sote tulimpenda,” anasema dada yake, Nancy Schindler. “Ron hakuwaruhusu Mama na Baba kusimama pamoja au kuketi pamoja bila yeye kuwa katikati yao.”

Ron kwa kawaida alikuwa mvulana mzuri,



kila siku 10:00 alfajiri na kurejea nyumbani usiku kila siku. Mama yake alikaa nyumbani kuwalea watoto, akiongezea mapato ya familia kwa kutengeneza na kuuza wanasesere waliotengenezwa kwa kauri zenye lesi.

Uwezo wa Ron wa kuzaliwa nao katika kuongoza, kukasimisha na kufanya mambo yafanyike—ambao ungemsaikia sana katika majukumu yake ya kikazi na kanisani—ulithibitisha kuwa na manufaa mapema sana.

“Ron alipewa jukumu la kukata nyasi,” dada yake anakumbuka. Lakini Ron, kama Tom Sawyer wa Mark Twain, alikuwa na njia ya kuwashawishi wenzake kutoa usaidizi.

“Ningetazama nje, na kungekuwa na rafiki yake mkubwa akikata nyasi kwa niaba yake,” Nancy anasema. “Wiki inayofuata mmoja wa marafiki zake alikuwa akikata nyasi. Aliketi tu mbele barazani na kucheka na kufanya utani nao huku wakifanya kazi yake.”

Wazazi wake Ron walikuwa na shida kife-dha, lakini familia ilikuwa na injili. “Kamwe hatukuwa na pesa nyingi,” Ron anakumbuka, “Lakini hilo halikuathiri furaha yangu.”

Aliwaamini Marafiki na Viongozi

Alipokuwa akikua, Ron alibarikiwa kuwa na marafiki wazuri na viongozi wa ukuhani waaminifu, pamoja na rais wa kigingi wakati wa ujana wake kwa miaka 14—James E. Faust (1920–2007), ambaye hatimaye alihudumu katika Akidi ya Mitume Kumi na

Wawili na katika Urais wa Kwanza. Familia ya Ron ilikuwa na uhusiano wa karibu na Rais Faust na familia yake. “Siku zote alinitambua kama mmoja wa vijana wake wa Cottonwood kwa sababu alisaidia katika kunilea,” anasema.

Ron hakuwa na wakati kwa michezo ya shule alipofika katika shule ya upili kwa sababu alikuwa na kazi siku zote, lakini alitengeneza muda kwa urafiki wa kuaminika ambao umedumu maisha yake.

“Siku zote nimetazama na kupendezwa na Ron kwa vile alivyo, lakini hakuwa mkamilifu,” anasema rafiki yake wa utotoni Kraig McCleary. Kwa tabasamu, anasema, “Siku zote nimemwambia kama ataingia mbinguni, pia na mimi nitaingia kwa sababu tulifanya mambo yaliyo sawa tukiwa tunakua.”

Ron alienda misheni yake mapema 1970 lakini Kraig alikuwa akifikiria kuhusu kuahirisha misheni yake hadi baada ya msimu wa mawindo ya majira ya kupukutika majani. Hapo ndipo Ron alipompigia simu kutoka kwenye misheni yake.

“Sijui jinsi ambavyo alipata ruhusa ya kupiga simu, lakini alinishutumu kwa kukosa kusisimka zaidi juu ya kwenda kuhudumu

Kutoka mwanzoni wa ndoa yao, Mzee na Dada Rasband wamemweka Bwana Mbele. Walioana Septemba 4, 1973 (chini), hatimaye walibarikiwa na mabinti wanne na mwana (juu). Ukurasa mkabala: Jon Huntsman Mkubwa., mfanya biashara mwenza na mshauri wa hapo awali wa Mzee Rasband, humu-ita Rasband “kiongozi mwenye kipaji cha uaminifu mkubwa.”



misheni mara moja,” Ndugu McCleary anasema. “La hashu, sikuahirisha.”

Ron huita misheni yake kuwa ni tukio la “ajabu.” “Bwana alinibariki na matukio mengi ya miujiza, matukio ya kujenga imani,” anasema. “Misheni yangu ilikuwa na maana kubwa kwa maisha yangu ya kiroho.”

Ron alitumikia sehemu ya misheni yake katika visiwa vya Bermuda. Rais wa misheni yake, Harold Nephi Wilkinson, alituma tu “wamisionari mishale mikali” huko kwa sababu angeweza tu kuwatembelea mara chache.

“Tulikuwa tumeachwa peke yetu kabisa, lakini rais hakuwa na sababu ya kuwa na wasiwasi juu yetu,” Ron anakumbuka. “Kazi ilifanyika.”

“Msichana wa Ndoto” wa Delta Phi

Baada ya kumaliza misheni yake mwaka 1972, Ron alipata kazi, na akajiunga na Chuo Kikuu cha Utah majira hayo ya kupukutika majani, na kujiunga na Delta Phi Kappa, udugu wa wamisionari waliorejea kutoka misheni zao. Katika shughuli za kijamii za udugu, hakukosa kumwona mwanamke kijana aliyependeza aliyetitwa Melanie Twitchell. Melanie alikuwa mmoja wa “wasichana wa ndoto,” wa Delta Phi waliochaguliwa na waliosaidia katika shughuli za huduma za udugu.

Kama Ron, Melanie alitoka katika familia ya Watakatifu wa Siku za Mwisho walio wahudhuriaji kamili. Baba yake, alikuwa ofisa wa kijeshi wa kudumu, na mama yake hakuruhusu kuhamahama kwa kila mara kuwa kisingizio cha kukosa kuhudhuria Kanisani.

Melanie alivutiwa na ukarimu wa Ron, hisani, na elimu yake ya injili. “Nilijisemea mwenyewe, ‘Huyu ni mwanaume wa kushangaza na katu sitajali hata kama sitawahi kuwa na miadi naye. Ninataka tu kuwa rafiki yake mkubwa.’”

Kadiri uhusiano wao ulivyokuwa ukikua, Roho alithibitisha hisia zake juu ya Ron na kujitoa kwake kwa Bwana. Punde uhusiano wao ulichanua na kuwa kile Melanie anachokiita “kitabu cha hadithi, hadithi ya mahaba ya vichimbakazi.”

Mzee Rasband anasema kuwa alilingana naye kikamilifu. “Melanie alikuwa katika kila njia sawa nami katika mapenzi ya injili na katika urithi. Tulikuja kuwa marafiki wa dhati, na hapo ndipo nilipomwomba nimuoe.”

Walioana Septemba 4, 1973, katika Hekalu la Salt Lake. Kutoka wakati huo, anasema, “mwandani wake wa milele asiye na ubinafsi . . . amesaidia kunifinyanga kama udongo wa mfyanzi hadi kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo aliyekwatuliwa zaidi. Upendo na msaada wake, na ule wa watoto wetu 5, na wandani wao, na wajukuu wetu 24, unaniimarisha.”³

“Na Twende zetu.”

Akiwa anahudumu kama rais wa akidi ya wazee wa kata yake ya wanafunzi waliofunga ndoa, Ron alikuja kumjua Jon Huntsman Sr., mshauri wa kata kutoka baraza kuu. Mara moja Jon alivutiwa na namna Ron alivyokuwa akiiongoza akidi hiyo.

“Alikuwa na ujuzi mkubwa wa uongozi na wa kuratibu,” anakumbuka Mzee Huntsman, ambaye alihudumu kama Sabini wa Eneo kutoka 1996 hadi 2011. “Nilifikiri ilikuwa sio kawaida kwa kijana ambaye alikuwa angali katika chuo kikuu kuweza kuendesha akidi kwa namna hii.”

Kwa muda wa miezi kadhaa, Jon alimtazama Ron akigeuza dhana kuwa vitendo alipokuwa akikamilisha majukumu ya ukuhani. Wakati nafasi ya afisa masoko mwandamizi ilipokuwa wazi katika kampuni ya Jon—ambayo ingekuja kuwa Huntsman Chemical Corporation—aliamua kuwa Ron alikuwa na ujuzi aliohitaji na akampa kazi hiyo. Nafasi hiyo ilianza wiki iliyofuata kule Ohio, Marekani.

“Nilimwambia Melanie, ‘Sitaacha shule na nihame,’” Ron anakumbuka. “Nimefanya bidii maisha yangu yote kuhitimu kutoka chuo kikuu, na sasa niko karibu kutimiza lengo langu.”

Melanie alimkumbusha Ron kwamba kupata kazi nzuri ndiyo sababu iliyomfanya kuwa shuleni.

“Ni kipi kinachokupa wasiwasi?” Aliuliza.

“Ninajua jinsi ya kupakia na kuhama. Nimekuwa nikifanya hivyo maisha yangu yote. Nitakuruhusu uzungumze na mama yako kila usiku. Twende zetu.”

Imani ya Jon katika Ron ilidhihirika kuwa sawa. Chini ya ushauri wa Jon, Ron alipanda vyeo kwa haraka sana katika kampuni hiyo iliyokuwa ikizidi kukua, akaja kuwa rais wake na ofisa mkuu mwendeshaji mwaka wa 1986. Alisafiri sana kwa niaba ya Kampuni—nyumbani na kimataifa. Licha ya ratiba yake yenye shughuli nyingi, Ron alijaribu kuwa nyumbani wakati wa mwishoni mwa wiki. Na aliposafiri, mara nyingine angesafiri pamoja na wanafamilia.

“Wakati alipokuwa nyumbani, kwa kweli aliwafanya watoto wajisikie kuwa ni watu muhimu na wenye kupendwa,” Melanie anasema. Alihudhuria shughuli zao na matukio ya spoti wakati ilipowezezana. Jenessa MacPherson, mmoja





wa wasichana wanne wa wana ndoa hawa, anasema kuwa majukumu ya baba yao kidini kwa siku ya Jumapili mara nyingi yalimzuia kuketi pamoja na familia yake wakati wa mikutano ya Kanisani.

“Tungepigania juu ya yule ambaye angepata kuketi pembeni yake Kanisani kwa sababu ilikuwa ni jambo geni sana kuwa naye pale,” anasema. “Ninakumbuka nikiweka mkono wangu mkononi mwake na kuwaza, ‘ikiwa tu nitaweza kujifunza kuwa kama yeye, nitakuwa katika njia sahihi na nitakuwa nikikaribia kuwa kama Mwokozi.’ Alikuwa shujaa wangu siku zote.”

Mwana wa wanandoa hawa, Christian, anakumbuka kumbukumbu nzuri za “wakati wa baba na mwana.” Marafiki walikuja na kwenda kwa sababu ya familia kuhama sana, anasema, “lakini baba yangu siku zote alikuwa rafiki yangu wa dhati”—ijapokuwa ni wa mashinano sana.

Iwe ni kurushiana mpira wa vikapu na Christian, kucheza mchezo wa ubao na mabinti zake, au kuvua samaki na familia na marafiki zake, Ron alipenda kushinda.

“Tulipokuwa tukikua, kamwe hangeweza *kumwacha* mtu yeyote ashinde,” Christian anasema. “Tulihitaji kuchuma kwa kufanya kazi, lakini hilo lilitufanya kuwa bora. Na desturi hii inaendelezwa na wajukuu wake wapendwa.”

Kwa muda wa miaka mingi, familia yake Ron hawakukosa kuona jinsi kuhudumu katika uongozi Kanisani kulikuza uwezo

wake wa kuonyesha upe-
ndo na huruma, kuonyesha hisia za roho, na kuwatia wengine moyo ili wafanye vyema. Baada ya kuzaliwa kwa Paxton, mjukuu wa Ron na Melaine, familia ilitegemea pakubwa sana nguvu za Ron za kiroho na kuhimili.

Paxton, alizaliwa na ugonjwa nadra sana wa kurithiwa, aliteseka kutokana na matatizo mengi sana ya kiafya ambayo yalijaribu familia kimwili, kimawazo, na kiroho. Mzee Rasband aliita safari iliyofuatia kuzaliwa kwa Paxton “majaribu makali ya kujifunza masomo maalumu yanayounganishwa na milele.”⁴

Wakati wa miaka mitatu mifupi ya Paxton ulimwenguni—wakati maswali yalipokuwa mengi na majibu yakiwa machache—Mzee Rasband alisimama kama nguzo ya kiroho, akiongoza familia yake katika kutegemea nguvu ya Upatanisho wa Yesu Kristo.

Kwa kutangazwa kwa wito wake mpya, wana familia kadhaa na marafiki hawakushangazwa. “Wale kati yetu wanaomfahamu vyema,” Christian anasema, “tuliinua mikono yetu juu zaidi wakati alipopigiwa kura ya kukubalikawa kama Mtume.”

“Nitaenda Kuhudumu”

Mwaka 1996, akiwa na umri wa 45, Ron alikuwa katikati ya kazi yenye mafanikio



Juu Kushoto: Mzee na Dada Rasband na waumini wa Kanisa huko New Delhi, India, Novemba 2015. Juu: Mzee na Dada Rasband wakati wa huduma yake kama Rais wa Misheni Jijini New York, 1996–99; pamoja na mjukuu wao Paxton, ambaye alisaidia familia kujifunza “masomo maalumu yanayoungana na milele”; na wakati wa she-rehe ya jive la kona la Hekalu la Sacramento California.

wakati wito ulipokuja aende kuhudumu kama rais wa misheni ya New York, New York Kaskazini. Kama Mitume wa zamani, “mara moja akaziacha nyavu [zake]” (Mathayo 4:20).

“Kukubali wito kulichukua chini ya sekunde moja tu,” Mzee Rasband anasema. Alimwambia Bwana, “Unataka niende kuhudumu, nitaenda kuhudumu.”

Ron alichukua somo kubwa alilokuwa amejifunza kutoka katika matukio yake ya kikazi: “Watu ni wa maana kuliko kitu kingine chochote.”⁵ Na elimu hiyo na ujuzi wake wa kuongoza ulionyooka, alikuwa tayari kuanza huduma ya umisionari katika Ufalme wa Mungu.

Ron na Melanie waligundua kazi ya umisionari kule New York ikiwa na changamoto na ya kuisisimua. Ron alikuwa mwepesi kugawa majukumu kwa wamisionari—na kutia moyo uaminifu wao, na kufundisha, kujenga, na kuwainua katika mchakato huo.

Katika mwaka wa 2000, miezi minane tu baada ya Ron na Melanie kukamilisha misheni yao, Ron aliitwa kuwa Sabini, mahali ambapo matayarisho yake, uzoefu wake, na vipaji vyake vingi vimelibariki Kanisa. Kama mshiriki wa Sabini, alihudumu kama mshauri katika Urais wa Eneo la Kati la Ulaya, akisaidia kusimamia kazi katika mataifa 39. Ingawaje aliondoka chuoni zaidi ya miaka 40 iliyopita, bado angali mwanafunzi mwenye bidii, akikubali ushauri endelevu kutoka kwa Ndugu zake wakubwa katika Ukuhani alipokuwa akisimamia maeneo ya Kaskazini mwa Amerika ya Magharibi, Kaskazini Magharibi, na maeneo matatu ya Utah; alihudumu kama Mkurugenzi Mtendaji wa Idara ya Mahekalu; na akahudumu katika Urais wa Sabini, akifanya kazi kwa karibu sana na wale Kumi na wawili.

Hivi majuzi, Mzee Rasband alisema, “Ni heshima na fadhila kubwa iliyoje kwangu kuwa mdogo miongoni mwa hawa Kumi na Wawili na kujifunza kutoka kwao katika kila njia na kila fursa.”⁶

“Waliyoyajua, Ninayajua”

Michoro miwili inapamba kuta za ofisi ya Mzee Rasband. Moja ni ya wamisionari wa Mormoni wakifundisha familia fulani kule Denmaki miaka ya 1850. Ya pili ni ya mmisionari wa mwanzoni Dan Jones akihubiri kutoka juu ya kisima katika Visiwa ya Uingereza. Michoro (juu kulia) inamkumbusha Mzee Rasband kuhusu ukoo wake.

“Hawa watangulizi wa mwanzoni walitoa vyote vilivyokuwa vyao kwa ajili ya injili ya Yesu Kristo na wameacha urithi kwa wazao wao kuendeleza,” ameshuhudia.⁷ Kilichowasukuma mababu wa Mzee Rasband kusonga mbele licha ya kuwa kati kati ya shida na mateso ndicho kinachomwezesha zaidi yeye katika wito wake mpya:



ufahamu na ushuhuda wa kweli wa Bwana na kazi Yake.

“Nina mengi sana ya kujifunza katika wito wangu mpya,” amesema. “Ninajisikia mnyonge kuhusu hilo. Lakini kuna kipengele kimoja katika wito wangu ninachoweza kukifanya. Ninaweza kutoa ushuhuda ‘wa jina la Kristo ulimwenguni kote’ (M&M 107:23). Yeye yu Hai!”⁸

Kama kitukuu cha waanzilishi, anaongeza: “Walivyojisi- kina nami ninajisikia. Waliyoyajua ninayajua.”⁹

Na yale waliyotarajia katika watoto wao yamedhi- hirishwa katika maisha, mafunzo, na huduma ya Mzee Ronald A. Rasband, ambaye anafuata mfano wao na kuheshimu urithi wao anaposonga mbele kama mmoja wa mashahidi maalumu wa Bwana. ■

MUHTASARI

1. Ronald A. Rasband, “Ninashangaa,” *Liahona*, Nov. 2015, 89.
2. Ronald A. Rasband, “Rafiki kwa Rafiki,” *Rafiki*, Okt. 2002, 8.
3. Ronald A. Rasband, “Ninashangaa,” 89.
4. Ronald A. Rasband, “Masomo Maalum,” *Liahona*, Mei 2012, 80.
5. Ronald A. Rasband, mkutano na waandishi wa habari, Okt. 3, 2015.
6. Ronald A. Rasband, ushuhuda, ibada fupi kwa Idara ya Ukuhani na Familia, Dis. 1, 2015.
7. Ronald A. Rasband, “Ninashangaa,” 89.
8. Ronald A. Rasband, ushuhuda.
9. Ronald A. Rasband, Hotuba ya Siku ya Waanzilishi, Tabernacle, Jijini Salt Lake, Julai 24, 2007.

JUU KUSHOTO: Picha na Wendy Keeler, kulia: Wahubiri wa Misionari wa Kwanza kule Denmaki, na Arnold Friberg (kutokana na Michoro wa Christen Dalsgaard, 1856); Dan Jones amsha Wales, na Clark Kelley Price

*Kwa sababu nilikuwa si mhudhuriaji mzuri miaka iliyopita,
muumini aliyenijua mimi wakati huo hakuweza kuamini niliitwa kuwa askofu.*

Na Patrick J. Cronin III

Wakati wa mkutano wa baraza la utendaji la ukuhani, wamisionari wetu walirifu kukutana na muumini ambaye kumbukumbu zake hazikuwepo katika kata. Nililitambua jina mara lilipotajwa kwamba mimi na yeye tuliwahi kuwa katika kata moja kwa miaka mingi iliyopita.

Mmoja wa wamisionari hao alisema, “Ndiyo, askofu, alisema hilo na alionekana kushangazwa kwamba wewe ni askofu.”

Niliwauliza, “Alisema nini?”

Walisesema alionekana kushangazwa sana na alisema, “*Yeye ndiye askofu?*”

Nilicheka na kueleza kwamba dada huyu alinijua kama mtu tofauti kabisa miaka 30 iliyopita.

Nilipolitafakari jambo hili baadae, niliwaza ni kiasi gani maisha yangu yamebadilika katika kipindi cha miaka 30 na zaidi ambayo mimi na familia yangu tumekuwa waumini. Nimewafahamu waumini wengi wa kata yangu kwa miaka 20 na nimetumikia kama rais wa tawi na kama askofu, lakini hakuna yeyote katika waumini hawa aliyenijua mimi miaka 30 iliyopita. Ingawa mara chache nimesimulia matukio ya maisha yangu ya zamani ili kufundisha toba na Upatanisho wa Yesu Kristo, sehemu kubwa ya kata hawajui safari ngumu ya kushangaza ya maisha yangu katika Kanisa ilivyokuwa.

Familia yangu na mimi tulitambulishwa kwa Kanisa Mei 1979, na nilijua mara moja kwamba hapa ndipo sisi

tunapaswa kuwa. Tulibatizwa Juni, na mwanzoni kabisa sote tulikuwa wahudhuriaji wazuri, lakini haikuchukua muda kabla ya mimi kuacha kuhudhuria na kurudi katika tabia zangu za zamani. Kamwe sikuwahi kwa kweli kuwa na shaka kuhusu ukweli juu ya injili na Urejesho, lakini sikuwahi kuwaza kwamba nilikuwa na cha kunifanya kuwa muumini mzuri wa Kanisa.

Mwaka 1982, kwa sababu ya kuendekeza utawaliwa wa ulevi, mke wangu, ambaye kamwe hakuwahi ku-shindwa katika imani yake, aliomba talaka. Wakati huo familia yangu ilikuwa ikiishi Oklahoma, Marekani, lakini mimi nilirejea Illinois, Marekani, mahali nilikolelewa. Nilifika mahali ambapo nilikuwa karibu kupoteza kitu cha pekee ambacho kwa kweli ni cha thamani kwangu: familia yangu.

Nilianza kusali nikipiga magoti asubuhi na jioni kwa Mungu ambaye sikuwa tena na uhakika kama yupo au kama alikuwepo, nilidhani Yeye amekwisha nisahau muda mrefu uliopita. Lakini kwa miezi mitatu nilisali kwa uaminifu kabisa. Mapema asubuhi moja, wakati nikiwa nimezama katika sala, hisia za usaidizi zikaja juu yangu na nikajua kwamba Mungu anaishi, na kwamba ananijua, na kwamba ananipenda. Pia nilijua sitagusa tena tone jingine la kileo.

Jioni ile ile nilipokea simu kutoka kwa mke wangu akini-fahamisha kwamba anatuma makaratasi ya talaka ili niweke saine. Wakati wa mazungumzo hayo ghafla akasema, “Kuna

Yeye ndiye ASKOFU?

kitu tofauti sana juu yako. Siamini kama utakuja kunywa tena, na nitachana makaratasi haya.” Tukarudiana, na miaka miwili baadae akamzaa mtoto wetu wa tatu wa kiume.

Mtu angefikiri kwamba ningelirudi na kuwa mhudhuriaji mkamilifu katika Kanisa, lakini mimi mwenye kichwa kigumu. Nilirudi kwa muda hata nikapokea wito kuwa mwalimu katika akidi ya wazee. Lakini mara nikaanza kujisikia nisiyetoshia kufundisha na tena nikasimama kuwa mhudhuriaji

Katika mwaka 1991 tulihamini katika tawi dogo. Miezi kadhaa kabla ya siku ya kuzaliwa ya mwaka wa nane ya mwana wetu mdogo wa kiume, mke wangu, rais wa Msingi, walimwuliza yeye ni nani angependa afanye ubatizo wake. Ni wazi alitaka baba yake afanye ibada hiyo. Mke wangu akamwambia kwamba yawezekana hiyo haitatokea. Yeye hakukubali jibu hilo na akajitwika jukumu la kumrejsha baba yake. Alikuwa wa kujishughulisha sana, na kwa ufupi nilijikuta nikitumika kama Skautmasta, na baadae nikambatiza na kumthibitisha mwanangu wa kiume.

Miezi minane iliyo-
fuatia baada ya kurudi

katika uhudhuriaji kamili kulikuwa na matukio mengi. Tulifunganishwa pamoja kama familia katika Hekalu la Illinois Chicago, na mimi tena nikaitwa kuhudumu kama mwalimu wa akidi ya wazee, lakini wakati sikuacha tena. Kisha niliitwa kuwa mshauri katika urais wa tawi, na miezi mitano baadae nikaitwa kutumikia kama rais wa tawi. Ni mwezi hivi kama sikosei baada ya wito wangu, ninakumbuka kufikiria, “*Mimi rais wa tawi?*”

Nimewaeleza Watakatifu wengi wanaohangaika kwa miaka mingi kwamba kama mimi nimeendelea katika injili, basi mtu ye yote anaweza. Ni suala tu la kuelewa nguvu halisi za Mwokozi na Upatanisho Wake na kuchukua hatua za kuja Kwake.

Milele nitamshukuru mke wangu na watoto na walimu wote wa nyumbani walio waaminifu, viongozi wa akidi, maaskofu, na Watakatifu walio waaminifu ambao waliweka mfano mwema kwa ajili yangu. Imekuwa fursa nzuri kwangu kumtumikia Bwana na Watakatifu kwa miaka hii 20 iliyopita. Maisha yangu yamebarikiwa kupita cho chote ambacho naweza kufikiria. ■

Mtunzi anaishi Illinois, Marekani.

TAFSIRI YA MAANDIKO:

KWA **Lugha** YA **Moyo Wetu**

Tukio hili linajulikana kwa wale ambao wamehusika katika kutafsiri maandiko kutoka Kingereza hadi lugha nyingine. Inafanyika mara kwa mara:

Kijana Mwarmenia aliyekuwa na Kitabu cha Mormoni mkononi ambacho kilikuwa tu kimetafsiriwa karibuni katika lugha yake alimkaribia mshiriki mmoja wa timu ambaye alisaidia katika tafsiri ... “Asante,” yeye anasema. “Nimekisoma Kitabu cha Mormoni katika Kingereza. Nimekisoma Kitabu cha Mormoni katika Kirusi. Nimekisoma katika Kiukreni. Lakini hadi nilipoweza kukisoma katika Kiarmenia, kwa kweli sikuwa nimekielewa. Nilipokisoma katika Kiarmenia, hatimaye kilileta maana. Ilikuwa kama kuja nyumbani.”

Kuja Nyumbani

Ikiwa injili ya Yesu Kristo ni nyumbani kwetu kiroho, basi ni vyema tu ikiwa itahisika starehe na kujulikana. Nyumbani tunapumzika. Tunajilisha. Tunazungumza na wale tuwapendao katika lugha tuliyofundishwa magotini mwa mama. Hii ndiyo lugha ya moyo wetu, na kwa vile moyo ndiyo kitu ambacho injili inafaa kufikia, kusoma maandiko katika lugha ya moyo wetu ni muhimu.

Mafundisho na Maagano kinapendekeza hivyo. Hapo Bwana anafunua kuwa kupitia funguo za ukuhani zinazoshikiwa na Urais wa Kwanza, “mkono wa Bwana utakapofunuliwa katika uwezo kwa kuyashawishi mataifa . . . juu ya injili ya wokovu wao.

“Kwani itakuja kutokea katika siku ile, kwamba kila mtu atasikia utimilifu

MATUKIO YASIYO NA HESABU YANAONYESHA MKONO WA BWANA KATIKA KAZI YA KUTAFSIRI MAANDIKO YAKE.

Na R. Val Johnson
Majarida ya Kanisa





Maandiko yanagusa moyo kwa nguvu zaidi wakati yanaposomwa katika lugha yetu ya mama—lugha ya moyo wetu.



**Kitabu cha Mormoni kamili
kimechapishwa katika lugha 89,
na uteuzi kutafsiriwa katika lugha
zingine 21.**

wa injili katika ulimi wake, na katika lugha yake mwenyewe, kupitia wale waliotawazwa kwa uwezo huu, kwa huduma ya Mfariji, aliyemwagwa juu yao kwa ajili ya ufunuo wa Yesu Kristo” (M&M 90:10–11).

Jim Jewell, ambaye alifanya kazi na timu ya tafsiri ya maandiko katika makao makuu ya Kanisa, anaeleza simulizi kuhusu jinsi maandiko yana-weza kuleta hisia za kuwa nyumbani wakati yanapokuwa yametafsiriwa katika lugha ya roho:

“Katika kutafsiri Kitabu cha Mormoni katika Sesotho, lugha ambayo inazungumzwa katika taifa la Afrika la Lesutu, tulihitaji mtu wa kutusaidia kutathmini kazi ya timu ya tafsiri. Msimamizi wa mradi huo, Larry Foley, alimpata mshiriki mmoja wa Kanisa kutoka Lesutu ambaye alikuwa mwanafunzi wa shahada ya pili katika Chuo Kikuu cha Utah State. Kule Lesutu, masomo yanaendeshwa katika Kiingereza, kwa hivyo mwanamke huyu na watoto wake walikuwa wamesoma katika Kiingereza kuanzia darasa la kwanza kuendelea, lakini walikuwa wakizungumza nyumbani kwao katika Sesotho.

“Alikubali kushughulikia tafsiri hiyo. Tathmini ya sura ambazo tulimtumia kwa kweli ilikuwa na usaidizi. Mara kwa mara tuliwasilisha maswali maalum kuhusu msamiati na muundo wa lugha ambapo alitoa majibu yenye manufaa. Hata hivyo, tulibaini kuwa alikuwa ameangazia akitumia rangi ya manjano aya nyingi sana ambazo hazikuwa na uhusiano na maswali yetu. Tulipomwuliza kuhusu aya alizokuwa amezisisitizia, alisema: ‘O, aya hizo

ni zile ambazo ziligusa moyo wangu sana ambazo sikuwa nimewahi kuzielewa kikamilifu katika Kiingereza. Niliziangazia ili niweze kuzishiriki na watoto wangu.’”

Mfano wa Tafsiri ya Maandiko

Kutafsiri kwa Biblia kuna historia ndefu sana ya kuvutia, kuanzia na tafsiri ya sehemu kadhaa za Agano la Kale kutoka Kiebrania hadi Kigiriki. Baadaye, Biblia kutafsiriwa kutoka

Kigiriki hadi Kilatini, na kutoka Kilatini, Kiebrania, na Kigiriki hadi Kiingereza na lugha zingine nyingi mno.¹ Kutokana na hayo, Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho halitafsiri Biblia kwa lugha tofauti lakini hukubali matoleo ambayo yashakubaliwa kama yenye kuaminika na Wakristo wanaozungumza lugha hizo.²

Kazi nyingi ya tafsiri ya kimaandiko ambayo Kanisa hufanya, hivyo basi, ni ya Kitabu cha Mormoni (kikiwa cha

**“KWANI ITAKUJA KUTOKEA . . . KWAMBA KILA MTU ATASIKIA UTIMILIFU WA
INJILI KATIKA ULIMI WAKE, NA KATIKA LUGHA YAKE MWENYEWI, KUPITIA
WALE WALIOTAWAZWA KWA UWEZO HUU” (M&M 90:11).**



MCHAKATO WA TAFSIRI YA MAANDIKO

1 Idhini ya Kutafsiri

- Tafsiri ya maandiko huitishwa na Urais wa Eneo wakati idadi ya washiriki wa Kanisa ambao wanazungumza lugha hiyo inaongezeka na wakati nyenzo za msingi za Kanisa zimetafsiriwa katika lugha hiyo.
- Ombi hilo linafanyiwa mapitio na kamati kadhaa za makao makuu ya Kanisa, ikiwa ni pamoja na washiriki wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili na Urais wa Kwanza.

Awamu za Tafsiri

Awamu ya Utangulizi:

- Tafsiri ya Biblia iliyopo inachaguliwa kwa matumizi ya Kanisa.
- Rasimali za msingi hutafsiriwa kwanza: *Misingi ya Injili* (ni pamoja na mafundisho ya msingi na pia jina la Kanisa, maombi ya sakramenti, maombi ya ubatizo, na Makala ya Imani), *Kijitabu cha Ushuhuda wa Nabii Joseph Smith*, na ukurasa wa tovuti kwenye LDS.org.
- Hotuba za mkutano mkuu zinaweza pia kutafsiriwa katika lugha hiyo.

Awamu 1:

- Kitabu cha Mormoni, Mafundisho na Maagano, Lulu ya Thamani Kuu (Takriban Miaka 10 ya kazi).
- Nakala za msingi kama “Familia: Tangazo kwa Ulimwengu,” “Kristo Aliye Hai: Ushuhuda wa Mitume,” nyimbo za kidini zilizochaguliwa, na *Hubiri Injili Yangu*.



kwanza kutafsiriwa), Mafundisho na Maagano, na Lulu ya Thamani Kuu. Lugha ambayo vitabu hivi hutafsiriwa ni kutoka Kiingereza, lugha ambayo Nabii Joseph Smith alivifunua, lugha ya moyo wake. Mchakato ambao hutumika katika kutafsiri maandiko hadi kwa lugha ambazo si Kiingereza yafaa kujulikana na wanafunzi wa historia ya Kanisa. Ni karibu tu sawa na mchakato ambao Nabii alitumia katika kutafsiri Kitabu cha Mormoni hadi kwa Kiingereza.

Joseph Smith alikuwa mnyenyekevu, mvulana asiyesoma sana wa mashambani. Lakini alikuwa na tabia na uwezo ambao Bwana alihitaji kwa ile kazi ambayo ilihitajika kufanywa. Kwa kweli, Joseph na familia yake waliandaliwa na kuwekwa mahali palipo stahili ili kufanya kazi hii.³

Joseph pia alipewa usaidizi—kutoka mbinguni na kutoka kwa binadamu—katika kutafsiri kumbukumbu hizi za wanefi. Malaika Moroni alimtembelea Joseph kila mwaka kwa miaka minne kabla ya kumruhusu kuichukua kumbukumbu hiyo. Hatujui kila kitu ambacho Moroni alimfundisha Nabii, lakini ziara zake inaonekana zilimuandaa kiroho na kiakili kwa kazi iliyokuwa mbele.⁴

Bwana pia alitayarisha “vikalimani” mbele ya muda kama njia ya kutafsiri lugha ambayo ilikuwa imepotea. Vilivyoielezwa kama mawe mawili masafi yaliyofungwa katika fremu za chuma, hizi na kifaa kama hicho kinachoitwa jwe la muonaji vilimsaidia Nabii kutafsiri kumbukumbu hiyo ya Wanefi hadi kwa Kiingereza. Nabii hakuzungumza kwa undani kuhusu

mchakato huo: alisema tu kwamba alitafsiri Kitabu cha Mormoni “kwa kipawa na uwezo wa Mungu.”⁵

Kama nyongeza kwa usaidizi wa mbinguni aliopewa, Joseph Smith alikuwa na usaidizi wa binadamu kupitia waandishi ambao walitoa nakala iliyoandikwa ambayo wengine mwishowe walitayarisha, wakapiga chapa, wakalipia gharama, na kusambaza ulimwenguni.

Si kama utayarishaji na usaidizi ambao Joseph alipata katika kazi yake ya kutafsiri, wale waliopewa jukumu la kutafsiri maandiko kwa wakati huu wanatayarishwa na Bwana na kupewa usaidizi katika kazi yao—kutoka mbinguni na kutoka kwa binadamu.

Kazi ya Ufunuaji

Inayolowesha mchakato huu mgumu wa kutafsiri ni nguvu ya kiroho ambayo inaweza kuelezwa bora kama “ufunuo kupitia baraza.” Watu hao wawili au watatu wanaochaguliwa kama wafasiri hujiunga pamoja na wengine katika kufanya kazi hiyo. Wana wasimamizi kutoka makao makuu ya Kanisa, wahakiki wa eneo, kamusi ya marejeo,⁶ miongozo ya tafsiri, programu za tarakilishi, na usaidizi wa viongozi wa Kanisa unaotamba hadi kwa Urais wa Kwanza. (Ona chati inayoambatana nayo) Wakati ambapo Urais wa Kwanza unatoa idhini ya mwisho ya tafsiri, kazi hiyo kisha inatayarishwa, inapigwa chapa, na kusambazwa. Ikiwa imetayarishwa katika muundo wa digitali, pia inawekwa katika LDS.org na katika Gospel Library app.

Juhudi za ushirikiano huu zilikuwa za umakinifu na zenye maongozi.



Inahusisha kuwa mwangalifu sana kwa ubora wa yaliyomo na ubora wa umbo la muundo ambao umetumika kuyawasilisha. Tafsiri hufanyiwa mapitio katika viwango vingi, hasa katika kiwango cha kidini ambapo idhini ya Bwana inatafutwa. Ni wakati tu idhini hiyo inapotolewa ndipo tafsiri inaweza kusonga mbele. Huku ikiwa si kwa ufunuo sawa na ile njia Nabii Joseph Smith alitafsiri Kitabu cha Mormoni, mchakato huu ni wazi kuwa unaongozwa na Bwana—kwa karama zake na kwa nguvu zake.

Hii haimaanishi kuwa tafsiri huwa kamilifu wakati inapokamilika mara ya kwanza. Mara nyingi, muda na mapitio zaidi na wale wanaosoma maandiko hupendekeza uboreshaji katika sarufi na msamiati au wanapata makosa ya utayarishaji au tahajia. Ni nadra, mabadiliko yafanyike katika kueleza mafundisho. Wakati haya yanapofanyika, yanafanyika chini ya uongozi wa urais wa Kwanza.

Bwana Huandaa

Bwana huruzuku kazi hii ya kutafsiri kwa njia zingine pia. Kawaida huwa kunaripotiwa na timu ya tafsiri katika makao makuu ya Kanisa kuwa wakati mahitaji yanapotokeza, Bwana huandaa.

Kama mojawapo ya mifano mingi, mfasiri alihitajika kwa ajili ya kutafsiri na kurekodi raslimali za Kanisa katika Mam (inatamkwa “mum,” ukoo wa lugha na Wamaya, inayozungumzwa Gwatemala). Miongoni mwa wamisionari wa kwanza walioitwa Gwatemala kulikuwa na mzee ambaye Babu

yake alizungumza Mam. Mmisionari alikuwa amelelewa mjini na alizungumza tu Kihispania. Lakini kila usiku babu yake angemjia katika ndoto na kumfundisha lugha ya Mam. Huyu mzee alikuja kuwa mfasiri wa pekee wa Mam Kanisani.

Mara nyingi, kazi ya kutafsiri hufanyika kwa kujitolea binafsi. Kutegemea na hali za kifedha, baadhi ya wafasiri hutoa msaada wa huduma na wengine hulipwa ili waweze kuwa na wakati wa kutenga kwa minajili ya kufanya tafsiri.

Mwanaume ambaye alikuja kuwa mmoja wa wafasiri wa Urdu aliongolewa kwa Kanisa kule Pakistani alipokuwa akifanya kazi kama mwalimu. Kwa sababu ya kuongoka kwake, alipoteza kazi yake; akapoteza nyumba yake, ambayo ilikuwa imetolewa na shule ambayo alikuwa akifundisha; na akapoteza masomo kwa watoto wake. Msimamizi mmoja wa tafsiri wa Kanisa alimwendea kuhusu kuhudumu kama mfasiri na kumpa malipo wastani. Baada ya kufanya kazi kama mfasiri kwa miezi kadhaa, bwana huyo alimtembelea msimamizi huyo na kwa woga kuuliza ikiwa msimamizi angeweza kumnunulia kalamu mpya ya wino. Ile ambayo alikuwa akitumia ilikuwa imeisha wino. Hapo tu ndipo msimamizi aligundua na kurekebisha makosa ya maandishi yaliyosababisha mfasiri kupokea tu kiwango kidogo cha malipo ambayo alistahili kupewa.

Lakini tu jinsi ambavyo Bwana alimbariki Joseph Smith kwa njia ambazo zilimwezesha kukamilisha kazi yake, Bwana huwabariki wafasiri wake. Kwa mfano, mfasiri wa maandiko ya

Awamu 2:

- Raslimali zingine nyingi zaweza kuitishwa, kama vile jarida la *Liahona*, vitabu vya kiada vya vyuo, mafundisho ya Jumapili, nyimbo za kidini na nyimbo za watoto, raslimali za hekalu na historia ya familia, na fasiri kwa ajili ya mtangazo ya kigingi na eneo.

Vikundi Muhimu vya Kufanya Kazi

Timu ya Tafsiri:

- Washiriki wawili au watatu wa Kanisa wanaostahiki kuingia katika hekalu na waliokomaa katika injili.
- Wakisaidiwa na mwongozo wa tafsiri wa aya kwa aya, kamusi ya marejeo, na msimamizi wa tafsiri kutoka makao makuu ya Kanisa.

Kamati ya uhakiki ya viongozi wa kanisa:

- Kati ya wanaume na wanawake watatu hadi watano ambao ni viongozi wa Kanisa katika eneo hilo.
- Waliopewa mwito na kusimikwa ili wasaidie katika kuhakiki tafsiri hiyo kwa uwezo wa kusomeka na usahihi wa mafundisho.
- Mabadiliko katika mpangilio wa maneno haubadiliki hadi kamati inapokubaliana kwa kauli moja na mabadiliko yanapoli-ngana na maelekezo ya tafsiri.

Wahakiki waumini:

- Waumini wa Kanisa katika eneo hili pia huhakiki tafsiri hiyo.
- Wao hutoa maoni kuhusu ubayana na usahihi wa mpangilio maneno.
- Ubayana wa tafsiri unahakikisha kuwa Roho Mtakatifu anaweza kushuhudia ukweli wa mafundisho.

Mchakato wa tafsiri ya maandiko unahusisha kichwa na moyo, ujuzi wa kiakili na umaizi wa kiroho.

Kilativia alikuwa mwanasheria ambaye alikuwa amesomea sheria kule Urusi, ambako alikuwa ameongolewa kwa injili ya urejesho. Kule Latvia, alikuwa anaanzisha biashara yake. Alikuwa pia anahudumu kama rais wa tawi. Alikuwa na shughuli nyingi mno, lakini Kanisa lilimhitaji pamoja na weledi wake wa Kingereza.

Aliomba muda apate kusali kuhusu ombi hilo kwa sababu kukubali

kungekuwa na maana, jinsi alivyo-mwambia mwakilishi wa Kanisa, “kutaondoa chakula vinywani mwa watoto wake.” Baada ya kuomba, aliamua kukubali lakini akamwuliza Bwana ambariki na uwezo wa kufanya kilichokuwa kigumu, uangalifu wa kiroho, na kazi yenye kuchukua muda mwingi.

Alianza kwenda katika ofisi yake ya sheria saa moja mapema kila siku na

kutumia saa hiyo moja kutafsiri Kitabu cha Mormoni. Alimaliza kwa wakati mzuri chini ya muda wa miaka mitano ambao mchakato huo kawaida huchukua. Kwa kweli, hii ilikuwa mojawapo wa tafsiri zilizofanywa haraka sana tangu wakati Joseph Smith alitafsiri Kitabu cha Mormoni katika muda wa takriban siku 60.

Matukio mengi sana yanaweza kutolewa ili kuonyesha mkono wa Bwana katika kazi ya kutafsiri maandiko Yake. Yote yanadhihirisha wazi kuwa hii ni kazi Yake na anajali sana kuihusu. Yeye huwatayarisha watu kufanya kazi Yake. Yeye hutayarisha vifaa wanavyohitaji kuharakisha kazi. Na Yeye anawapa maongozi na kuwabariki njiani.


Matokeo ni ulimwengu ulioimarishwa na neno la Mungu, na kupewa watoto wake katika lugha ya moyo. ■

MUHTASARI

1. Ona mfululizo wa sehemu nane, “Namna Biblia Ilikuwa Kuwa,” na Lenet H. Read ilichapishwa katika *Ensign* between Januari na Septemba 1982.
2. Ona, kwa mfano, “Toleo la Kanisa la Biblia ya Kihispania Iliyochapishwa Sasa,” mormon-newsroom.org.
3. Ona Matthew S. Holland, “Njia ya Kuelekea Palmyra,” *Liahona*, Juni 2015, 14–19.
4. Ona Kent P. Jackson, “Ujumbe wa Moroni kwake Joseph Smith,” *Ensign*, Ago. 1990, 12–16.
5. Joseph Smith, katika utangulizi wa Kitabu cha Mormoni. Kwa maelezo kamili kuhusu tafsiri ya Joseph Smith ya Kitabu cha Mormoni, ona Mada ya Injili, “Book of Mormon Translation,” topics.lds.org.
6. Kamusi ya marejeo hufafanua kila neno katika maandiko ya Kiingereza ili wafasiri waweze kuelewa vyema maana ya maneno. Mara nyingi, maneno huwa na zaidi ya maana moja, kwa hivyo wafasiri lazima wategeme muktadha, msukumo, na ushirikiano kutafuta suluhu mwafaka. Mara kwa mara, maswali kuhusu maana hutatuliwa tu na Urais wa Kwanza.

KATIKA KAZI YA KUTAFSIRI MAANDIKO YA BWANA, NI DHAHIRI KUWA HII NI KAZI YAKE. YEYE HUWATAYARISHA WATU NA VIFAA AMBAYO WANAHITAJI KUHARAKISHA KAZI HII, NA YEYE HUWAPA MAONGOZI NA KUWABARIKI NJIANI.





**Na Rais
Russell M. Nelson**

Rais wa Akidi ya
Mitume Kumi na
Wawili

NYAKATI ZA Wamisionari Wakubwa

Mojawapo ya njia bora za wamisionari wakubwa kuweza kujitengenezea kumbukumbu nzuri sana ni kupitia kuhudumu misheni kwa pamoja.

Wakati marafiki zetu walio na umri wa miaka 60 au 70 husahau kitu, mara nyingi kwa utani sisi huita kupitiwa huku wakati wa wakuu. Lakini ningependa kujadili aina tofauti ya wakati wa wakubwa—ni wakati wa kupendeza mno kiasi cha kuwa kumbukumbu yake itakuwa ya milele. Ni ule wakati ambao wanandoa wamisionari wakubwa hugundua kwamba sasa wanafanya hasa kile ambacho Bwana angependa wafanye. Wakati wa kukumbukwa kama huu wanatambua kuwa:

- Wanayo matukio ya miaka mingi ya kusimuliana, na vipaji, ujuzi, na uelewa wa injili ambao wanaweza kutumia kuwabariki wengine.
- Mfano wao ni baraka kwa watoto wao na watoto wa watoto wao.
- Wanapohudumu wanaunda urafiki wa kudumu.
- Ndoa yao inakua na kuimarika kila siku.
- Huduma katika jina Lake ni tamu.

Nyakati Zinazokuja

Marafiki zangu wana ndoa wakubwa, nyakati kama hizi zinapaswa kutengenezwa na wengi wenu. Fikiria simulizi iliyotolewa na Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili kuhusu kile ambacho wanandoa wakubwa waliokuwa wakihudumu kule Chile walicho-weza kufanya. Mzazi wa mmoja wa mzee kijana alikuwa ameaga dunia. Rais wa misheni alikuwa mbali sana kiasi cha kutoweza kumfikia yule mmisionari kwa haraka.

Lakini kulikuwa na wanandoa wamisionari wazuri sana

[waliokomaa] waliokuwa wakihudumu katika eneo lile, Mzee Holland anasema. Walikuja na wakaketi na yule mmisionari na kumhudumia kwa upole na kumfariji hadi wakati rais wa misheni alipoweza kumfikia yeye mwenyewe. Tulikuwa na wamisionari vijana mashuhuri sana katika misheni zetu, lakini hakuna mmisionari ambaye ange-weza kumhudumia yule mzee jinsi ambavyo wanandoa wale waliweza kufanya.¹

Ujuzi wao kwa wakati ule ulikuwa tu kumfariji katika wakati wa haja. Hawakuwa na wasiwasi kuhusu lugha ya kuongea zaidi ya kuongea lugha ya upendo kama wa Kristo. Hawakuwa na wasiwasi kuhusu kukosa kuwepo wakati wa siku ya kuzaliwa ya mjukuu wao au kubarikiwa kwa mtoto, hata kama shughuli hizo ni muhimu kiasi gani. Walikuwa na haja ya kuwa mahali ambapo Bwana ange-weza kuwatumia ili kubariki maisha ya mmoja wa watoto Wake. Na kwa sababu walikuwa tayari, Yeye aliweza kuwapa nafasi ya kumwakilisha.

Ni Nadra Huduma Kuwa Rahisi

Ukweli ni kwamba, hakuna mmisionari mkubwa ambaye anaona urahisi kutoka nyumbani. Si Joseph Smith, Brigham Young, John Taylor, au Wilford Woodruff. Walikuwa na watoto na wajukuu pia, na walipenda familia zao kama sisi tunavyofanya. Lakini pia walipenda Bwana na wakataka kumtumikia. Siku moja tutaweza kukutana na hawa watu maarufu ambao walisaidia katika kuanzisha kipindi hiki cha injili. Tutakapofanya hivyo, tutakuwa na furaha kwamba hatukujificha kivulini wakati tulipopaswa kuhudumu.

Wengine wanaweza kupendelea kuhudumu wakiwa wangali wanaishi nyumbani. Baada ya ugonjwa wa kiharusi kumwacha Aase Schumacher Nelson (hamna uhusiano) akiwa amezuiliwa kwenye kiti mwendo, alikuwa na hofu kuwa hamu ya maisha yake yote ya kwenda kuhudumu misheni na mumewe Don haingetimizwa. Kisha jirani akazungumza nao kuhusu misheni yake ya huduma ya Kanisa katika ghala la askofu. Wakiwa wametiwa moyo, walizungumza na msimamizi katika kituo hicho, wakajaza fomu zao za mapendekezo, na waliitwa kuhudumu siku mbili katika wiki katika ghala karibu na nyumbani kwao.

Ni rahisi kukaa tu na kufikiria, O, sihitajiki po pote, Aase Nelson anasema. Lakini sasa ninajisikia kwamba *ninahitajika*. Na hiyo imekuwa ushuhuda kwangu.

Kwa Hakika Unahitajika

Ikiwa umejaribiwa kufikiria kuwa hauhitajiki, wacha nikuhakikishie kuwa unahitajika. Hakuna rais wa misheni Kanisani ambaye hangependa kuwa na wanandoa wamisionari zaidi wakihudumu katika misheni yake. Wakubwa huimarisha wazee vijana na kina dada wamisionari. Wao hutoa msaada unaowezesha wengine kuhudumu vyema katika majukumu yao. Na unaweza kufikiria umuhimu wa haya kwa kiongozi ambaye amekuwa tu muumini kwa miaka michache kuwa na uwezo wa kufikia muumini wa Kanisa mwenye tajriba ya hali ya juu? Wanandoa wakubwa mara nyingi huwa ni jibu halisi kwa maombi ya maaskofu na marais wa matawi.

Tunawahimiza marais wa misheni kuwatafuta wanandoa ili kutimiza mahitaji katika misheni zao. Maaskofu wanapaswa kuwatafuta wanandoa wanaoweza kuhudumu. LDS.org inaorodhesha kurasa nyingi mno za nafasi za wanandoa wakubwa. Lakini zaidi ya hayo, wanandoa



Wanandoa kule Seoul, Korea Kusini, wanafurahia raha ya kuhudumu pamoja.

wenyewe wanapaswa kupiga magoti na kumwomba Baba wa Mbinguni ikiwa wakati ni sahihi kwao kwenda kuhudumu misheni pamoja. Kati ya sifa zote, *hamu* ya kuhudumu inaweza kuwa ya muhimu zaidi (ona M&M 4:3).

Huku nikisifu sana kazi ya wamisionari wakubwa, ninatambua kwamba kuna wengi ambao wangependa kuhudumu lakini hawawezi kufanya hivyo. Vizuizi vina vyotokana na umri au afya mbaya vinastahili tathmini ya kweli, vile vile mahitaji muhimu ya wanafamilia. Wakati ambapo una hamu sana lakini vizuizi vya aina hii vipo, wengine waweza kuwa mikono yako na miguu, na wewe unaweza kutoa fedha zinazohitajika.

Wanandoa wakubwa, bila kujali nyinyi ni kina nani au mahali mliopo, tafadhalini ombeni kuhusu nafasi hii ya kutengeneza nyakati nzuri za wamisionari wakubwa pamoja. Baba wa Mbinguni atakusaidia ujue unachoweza kufanya. ■

MUHTASARI

1. Jeffrey R. Holland katika Joseph Walker, "Elder Jeffrey Holland: LDS Church Desperately Needs More Senior Missionaries," *Deseret News*, Sept. 14, 2011, 3.



Kilele: Kina Malmrose hukutana mara kwa mara na Rais Robinson kujadili jinsi wanaweza kutumia vipaji vyao wanapowahudumia wengine. Juu: Vijana wamisionari walio katika kituo cha mafunzo kule Accra, Ghana, wanasema kwamba kupata usaidizi kutoka kwa Mzee na Dada Malmrose ni kama kuwa na mama na baba wa pili wakihudumu pembeni mwao.



KUTOKA NYUMBANI AU MBALI KUTOKA NYUMBANI
Wakihudumu kutoka nyumbani au mbali kutoka nyumbani, wamisionari wakubwa "huja kusaidia" katika kata na matawi, ofisi za misheni, vituo vya wageni, hekalu, misheni za mijini, majukumu ya kimatibabu, vituo vya raslimali za uajiri, mipango ya kujitegemea, mipango ya kupata nafuu kwa watawaliwa, historia ya familia, utunzaji wa rekodi, Mfumo wa Elimu wa Kanisa, uhusiano na umma, huduma za kibinadamu, na zaidi. Na wanandoa zaidi na zaidi wanahitajika.



Wamisionari Wakuu:

HITAJIKA,
BARIKIWA,
NA PENDWA

*Kuhudumu misheni
kama wanandoa
inaweza kuwa rahisi,
sio ghali sana, na
kuleta furaha zaidi
kuliko unavyodhania.*

Na Richard M. Romney

Majorida ya Kanisa

“UNAWENZA KUJA KUSAIDIA?”

Ni swali ambalo Gerald na Lorna Malmrose wa Washington, Marekani, walikuwa wamewahi kulijibu mbeni. Walisema ndio wakati aliyekuwa askofu wao, wakati huo rais wa misheni, aliuliza ikiwa wangeweza kuhudumu naye kule West Indies. Walisema ndio tena wakati rais wao wa kigingi aliwaitia mwito wa kutekeleza misheni ya huduma katika makao makuu ya Kanisa kule Salt Lake City, Utah, Marekani, wakishughulikia tarakilishi na rasimali ya watu.

Wakati ambapo aliyekuwa askofu wao na rais wa misheni, Reid Robinson, aliwaita tena, wakati huu akiwa rais wa kituo cha mafunzo cha misionari kilichoko Accra, Ghana, aliwauliza kina Malmroses ikiwa wangeweza kusaidia mara nyingine.

“Tulijua tungeweza kumwamini Bwana,” Mzee Malmrose anasema. “Kwa hivyo tuliamua kumwamini tena.” Walisema ndio, wakajaza fomu za mapendekezo, wapakokea mwito, na punde walikuwa kule Ghana.

Kuhudumu kama Wanandoa

Uzoefu wa kina Malmrose unaonyesha kanuni kadhaa kuhusu wanandoa wazee wanaohudumu misheni ambazo hazieleweki sana.

- *Kuna misheni za aina mbili.* (1) Rais wa Kanisa huwaita wanandoa wazee kuhudumu kutoka

nyumbani kwao ama mbali kutoka nyumbani.

(2) Rais wa kigingi huwaita wamisionari wanandoa wa huduma ya Kanisa kutimiza mahitaji ya eneo lao kwa muda maalum, kati ya saa 8 hadi 32 kila wiki. Kawaida huwa wanaishi na kuhudumu katika eneo lao lakini mara nyingine wanaweza kuhudumu mbali na nyumbani.

- *Marais wa misheni wanahimizwa kutafuta wanandoa ambao wanaweza kutosheleza mahitaji katika misheni zao, na wanandoa wanaweza kudokeza mapendeleo yao.* “Hatusemi kuwa wanandoa wanaweza kuteua na kuchagua miito yao ya misheni,” anaeleza Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili. “Mwito bado ni mwito. . . [Lakini] tunazungumza na wanandoa wetu wazee kuhusu mapendeleo yao ya huduma, na kila uzingatio unafanywa kuwaruhusu kuhudumu mahali na jinsi wanataka kuhudumu.”¹
- *Marais wa misheni hushauriana na wanandoa kuhusu jinsi wanavyoweza kutumia ujuzi na uwezo wao.* “Kuwa na uzoefu wa maana kama wanandoa wakubwa,” Rais Robinson anasema, “unahitaji kuwa na nafasi ya kufanya kazi unayoipenda na maeneo ambayo una ujuzi kiasi cha kukufanya uhisi kuwa unahitajika.”

Kwa mfano, Rais Robinson alifahamu kwamba Mzee Malmrose anajua kuzungumza Kifaransa, ina manufaa



JITOLEENI

“Tunahitaji wengi, wamisionari waku-bwa wengi zaidi. . . . Jitoleeni. . . . Kuna nyakati chache katika maisha yako ambapo utaweza kufurahia [sana] roho mwema na kuridhika ambako kunatokana na [kuhudumu] kutoa huduma ya pamoja katika kazi ya Bwana.”

Rais Thomas S. Monson,
“Tunapokutana Pamoja Tena,” *Liahona*, Nov. 2010, 6.



kwa sababu Waafrika wengi huzungumza Kifaransa. “Nilikuwa na maono akihusika na usafiri na kushughulikia viza,” Rais Robinson anasema. “Lakini wakati aliwasili hapa, nilihisi kuwa huo haukuwa mvuto wake halisi. Kwa hivyo nilimualika atumie ujuzi wake wa tarakilishi. Ametuokolea masaa mengi, mengi sana.” Mzee Malmrose pia husaidia wamisionari, hasa wamisionari wanaozungumza kifaransa, kutayarisha majina na kufanya kazi ya hekalu kwa niaba ya familia zao. Dada Malmrose, msaidizi wa matibabu aliyesajiliwa, alikuwa na jukumu la kufanya kazi na daktari na muuguzi wa misheni.

Yeye Hutayarisha Njia

Kama kina Malmrose, wanandoa wengine wanagundua kuwa wanapomwamini Bwana, Yeye hutayarisha njia. Hilo ndilo lililowafanyikia Alvin na Corazon Rieta wa Kawit, Cavite, kule Ufilipino.

“Miaka miwili kabla ya uamuzi wetu wa kuhudumu, tulianza kuweka mipango imara kwa ajili ya biashara ya familia yetu,” Mzee Reita anaeleza. “Mwana na binti yetu walikuwa wamehitimu kutoka chuo kikuu na wangeweza kuchukua usukani kutoka kwetu, lakini tulijiuliza ni nani angesuluhisha shida za kibiashara na wateja wetu wangeona namna gani kuhusu mipango yetu.”

Dada Reita pia alikuwa na wasiwasi kuhusu kumuacha mamake mzee. “Nilikuwa na hofu kuwa tungempoteza tukiwa tungali mbali,” anasema. “Pia nilijisikia mpungufu kwa mwito wa kwenda kufundisha injili.”

Walifanya mashauriano na askofu wao na wanandoa ambao karibuni walikuwa wamehudumu kule Davao. “Wote walitoa ushuhuda wa nguvu kuwa Bwana angeongoza kila wanandoa kujua namna ya kushughulikia mambo yao ya nyumbani, na familia zao, na mahitaji yao ya kifedha ya misheni zao,” Dada Reita anasema.

“Tulipokuwa tukitafuta mwongozo,” Mzee Reita anasema, “hofu zetu zilishughulikiwa—biashara yetu iliendelea vizuri licha ya changamoto, wateja wetu walionyeshwa furaha na kutuunga mkono, na familia yetu ilikuja pamoja kwa kumchunga mama yetu mgonjwa. Tulianza kuelewa kuwa kwa kweli Bwana angetusaidia.”

Kina Reita sasa wanahudumu katika usaidizi wa washiriki na viongozi kule Ufilipino katika Misheni ya Cagayan de Oro.

Ni Mengi Unayoweza Kufanya

Wanandoa wengine huwaza kuhusu ufinyu wa viungo, lakini siyo Keith na Jennilyn Mauerman wa Utah, Marekani. Miaka kadhaa iliyopita, miezi minne baada ya kufunga ndoa katika hekalu la Los Angeles California, Keith alisajiliwa na kutumwa katika vita. Kiongozi wa kikosi cha wanahewa, alikuwa akitembea mbele ya wanajeshi wengine wakati bomu la kutegwa ardhini lilipuka. Alipoteza miguu yote. Alipowasili nyumbani, Jennilyn alikiambia pembeni kwake.

“Nilijua sikuhitaji kuwa na wasiwasi,” Keith anasema, “kwa sababu tuna ndoa ya milele. Bibi yangu amenisaidia huu muda wote. Bado angali ananihimili kila siku.”

Wakati ambapo Dada Mauerman alistaafu, tuliamua kuhudumu misheni. Lakini hali ya Mzee Mauerman kukatwa viungo viwili vya mwili inaleta tashwishwi? “Sikuzote kuna mambo *siwezi* kufanya,” anasema, “lakini kuna mambo mengi sana *ninayoweza* kufanya, tulijua kungekuwepo na nafasi kwetu.”

Walipokuwa wakijaza fomu zao za mapendekezo, alichagua sehemu iliyoonyesha kuwa alikuwa amehudumu katika jeshi. Punde walipokea simu kutoka Ofisi ya Kanisa ya Uhusiano wa Kijeshi. “Nilikuwa na Kitambulisho ambacho kingetuwzesha kuingia katika kambi za kijeshi, kwa hivyo walitueliza idhini ya kutupendekeza kuhudumu misheni ya uhusiano wa kijeshi.”

Bwana na Bi Mauerman walipewa mwito

katika kambi ya kijeshi kule North Carolina, Marekani. Mzee Mauerman anakumbuka: “Ishara iliyokuwa kwenye lango ‘Fort Bragg, Nyumbani kwa Wanajeshi wa Angani.’ Wakati mlinzi alipotusalimia kwa wito wa wanajeshi wa angani ‘Pita Ndani!’ ilikuwa mara ya kwanza nilikuwa nimeisikia kwa miaka mingi. Nilijihisi nyumbani, hata kama sikuwa nimeshawahi kuwa Fort Bragg. Nilijua misheni yetu litufaa kikamilifu na kuwa Bwana alinjali.”

“Tulifundisha masomo kuhusu kujitegemea na kuwa imara na kuhusu kuimarisha ndoa,” Dada Mauerman anasema. “Mwanzoni hatukuwa tunataka kushiriki simulizi yetu, lakini tuligundua kuwa kuishiriki kulileta tofauti

Mzee Romrell alikuwa amehudumu kule Brazili kama mmissionari akiwa kijana, alikuwa kidogo amesahau Kireno. Na Dada Romrell hakuelewa kireno. Kusoma na jitihada, hata hivyo, ilisaidia ujuzi wa Mzee Romrell kurejea na wa Dada Romrell kuimarika. Na hata wa ukulele.

“Sikuwa na mpango kamili wa kuileta,” Dada Romrell anasema, “lakini Mzee Romrell alikuwa na msukumo wa kufanya hivyo, na ni ajabu kuona kile ambacho imefanya. Tunapowafundisha wachunguzi na kushughulikia kurejesha katika uhudhuriaji kamili na ushirika, ni furaha kuitumia kufanya watu waimbe nyimbo za kidini. Tunajifunza lugha, na nyimbo za kidini huleta roho wa nguvu pamoja nazo.”



Wakiwa wamesuluhisha wasiwasi wao wa kifedha, Mzee na Dada Reita wanahudumu katika nchi yao, Ufilipino.



Kwa kina Mauerman, kuhudumu katika Uhusiano wa Kijeshi kunawafaa sana. “Inahisi kama kuja nyumbani,” wanasema.



Wakiwa na maongozi wa kusafiri na ukulele, kina Romrell wanaitumia kushiriki lugha ya kote ulimwenguni ya muziki wanapotembelea makazi na kuimba nyimbo za injili.

kubwa. Wanajeshi na wapenzi wao walitutazama na kusema, ‘Ikiwa mnaweza fanya hivyo, pia sisi tunaweza.’”


Kina Mauerman walikuwa na tukio chanya kule North Carolina kiasi cha kuwa walitaka kuhudumu tena. Siku hizi wao husafiri takriban maili 40 (64 km) kutoka nyumbani kwao kule Orem hadi Mji wa Salt Lake mara mbili kwa wiki kwenda kuhudumu katika Ofisi ya Kanisa ya Uhusiano wa Kijeshi. Wao pia huwafunza wanandoa wamisionari katika kituo cha mafunzo kule Provo, ambako wanagundua kuwa karibu tu kila kikundi kinajumlisha mtu ambaye amepambana na vikwazo ili kuweza kuhudumu.

Lugha za Ulimwengu Mzima

Waliitwa katika Misheni ya Brazil Cuiabá, Randy na Lou Ellen Romrell wa Utah walikuwa na wasiwasi. Ingawaje

Hata kama ujuzi wake wa Kireno bado ungali unakua, Dada Romrell tayari ni mweledi katika muziki. “Muziki huleta watu pamoja,” anasema. “Hata kama siwezi kuelewa kila wanachosema tunapowatembelea, tunapoimba, tunaungana.” Walipoalikwa kuzungumza shuleni kuhusu sikukuu ya Marekani ya Kutoa Shukrani, kina Romrell waliimba nyimbo za kidini za kutoa shukrani—ikipambwa na ukulele. Na Dada Romrell pia hutumia ala ya muziki ya kawaida, kinanda, kupamba nyimbo za kidini kanisani.

Na Kireno? “Hata ikiwa wewe si mweledi, kujifunza maneno machache kunasaidia,” anasema. “Kwa kusema tu jambo na kuwasalimia watu kuna umuhimu mkubwa sana. Wajulishe kuwa unajifunza. Ifanya iwe rahisi na mtegemee Roho.” Na Roho, kama ilivyo, ni lugha nyingine ambayo kila mtu anaweza kushiriki.



“KILE UNACHO-TAKA NIWE”

“Ninapofikiria kuhusu mahitaji makubwa ya wamisionari wakuu, kila mara mimi hufikiri kuhusu ule wimbo mzuri wa kidini ‘Nitae-nda Utakapo Niende’ (Nyimbo za Kidini, no. 270) na ujumbe wake, ‘Nitakuwa Uta-kacho Niwe.’”

Mzee Dallin H. Oaks wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili.



WANANDOA WANAHITAJIKA

“Ujumbe wetu kwa wanandoa wetu wa-kubwa wote ni rahisi: tunawahitaji sana. Tunafanya kila juhudi kuifanya iwe rahisi iwezekanavyo kwenu kuenda. . . . Nyakati zina- lilia hayo. Kuna watu ambao wanawahitaji. Tafadhali—nendeni.”

Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, *Deseret News*, Sept. 14, 2011.

Kuhudumu Nyumbani

Paul na Mar Jean Lewis kutoka Utah walikuwa tayari wamehudumu misheni tatu pamoja (Hekalu la Palmyra New York; Hekalu la Hong Kong Uchina; Serbia, na Slovenia na vyuo). Walikuwa wakijitayarisha kuhudumu misheni nyingine wakati rais wao wa kigingi aliuliza, “Mnaweza kuwa na hamu ya kuhudumu papa hapa katika kigingi chetu, mkisaidia misheni tunamoishi?”

“Sisi ni wageni hapa, kwa hivyo ilikuwa nafasi nzuri sana,” Dada Lewis anasema.

kuhusu kile watakachofanya na nyumba yao, gari lao au watakachokosa katika familia zao,” Mzee Lewis anasema. “Tumeweza kuishi nyumbani kwetu na kuendesha gari letu. Tunatiwa moyo kuhudhuria shughuli za familia, muradi tu zisiingiliane na majukumu yetu ya kimisionari. Na hata tulikuwa hapa kwa kuza-liwa kwa mjukuu wetu.”

Baraka za Familia

Kwa upande mwingine, Jill na Kent Sorensen, ambao wanatoka katika kigingi



Kuhudumu kutoka nyumbani, kina Lewis wanafurahia kuwajua wamisionari na waumini wa kigingi chao.



Kina Sorensen huwapa watoto katika Visiwa vya Cook mawe ndogo kuwakumbusha wabaki “imara kama mwamba katika Kristo.”

“Tunahudumu na wale vijana wazee wamisionari na kina dada, tuna uhusiano wa karibu na rais wa misheni, huwa tunahudhuria mi-kutano ya wilaya na zoni, na tunafanya kazi na viongozi wa kata wa umisionari.” Wao pia huwatembelea wachunguzi na wale ambao hawahudhuri kikamilifu.

“Tumekutana na watu wazuri sana ambao hatungeweza kupata kuwajua kwa njia nyingine,” Dada Lewis anasema, “pamoja na wale ambao wamepotea njia. Kuwaona wakirudi, wakipokea maagizo, na kwenda katika hekalu ni baraka kubwa.”

“Wanandoa wengi, wanapofikiria kuhusu kuhudumu misheni, wana wasiwasi

hicho pia wanasema mojawapo ya njia mwafaka za kuimarisha familia yao imekuwa kuhudumu mbali na nyumbani. Dada Sorensen anasema, “Mojawapo ya visingizio vikuu ambavyo wanandoa hutoa kama sababu ya kukosa kwenda ni wajukuu, watoto waliofunga ndoa na walio na matatizo, mabinti wanaotarajia kujifungua, wazazi wakongwe—unaweza kuvitaja. Familia ni kipaumbele, na unawakosa kila siku. Lakini kuhudumu misheni kunatoa ujumbe wa nguvu kuwa kazi ya umisionari ni muhimu pia.”

Kando na, Mzee Sorensen anasema, “kuna njia nyingi sana za kuwasiliana kwa vile hivi sasa waweza kuwajulia hali wakati wowote.”

Safari ya kina Sorensen ya umisionari ilianza miaka mitatu iliyopita, wakati askofu wao aliwauliza kuandaa mikutano ya mafunzo kila mwezi kwa ajili ya wanandoa ambao wana dhana za kutoa huduma ya umisionari. “Baada ya kuizungumzia kila mara,” Dada Sorensen anasema, “ilibidi twende sisi wenyewe!” Walipokea mwito wa kuhudumu katika Visiwa vya Cook, ambako mababu wa Jill walihudumu miaka 50 iliyopita.

Siku hizi, miongoni mwa majukumu mengine, wameombwa kufundisha masomo ya Biblia katika shule.

“Sisi huzungumza kumhusu Kristo akiwa mwamba,” Mzee Sorensen anasema. “Sisi huwapa wanafunzi mawe ndogo



Kote ulimwenguni, wanandoa wanasema kuwa kando na kuwasaidia wengine, kuhudumu pamoja kunaimarisha ndoa zao na kuwaleta karibu na Baba wa Mbinguni.

kuwasihii wabaki imara kama mwamba katika Kristo. Sasa kila tuendapo, watu husema, ‘Imara kama Mwamba!’ Wakati wanapotuona.”

Njoo Utoe Msaada

Ikiwa una dhana za kuhudumu misheni kamififu au misheni ya huduma ya Kanisa, kila mmoja wa wanandoa hawa watakuuliza swali kama lile ambalo Rais Robinson aliwauliza Gerald na Lorna Malmrose: “Mnaweza kuja kusaidia?” Na watakuueleza kuwa, haijalishi jinsi unavyoshiriki, ahadi hii ni ya kweli: Mnahitajika, mnaweza kuchangia, na mtabarikiwa na upendo. ■

MUHTASARI

1. “Mzee Jeffrey R. Holland: Kanisa la LDS Linahitaji Wamisionari Wakubwa Kwa Dharura Sana,” *Deseret News*, Sept. 14, 2011, deseretnews.com.

NJIA NYINGI ZA KUHUDUMU

Tazama Nafasi Ziliopo, sikiliza kutoka kwa wale wanaohudumu hivi sasa, na upate majibu kwa maswali kutoka lds.org/callings/missionary.

NI RAHISI SANA KULIKO WAKATI WOWOTE ULE

Sera rahisi zinafanya iwe rahisi sana kwa wanandoa kuhudumu.

- Wanandoa wa huduma za Kanisa wanaweza kuisi nyumbani na kuhudumu katika maeno yao.
- Wanandoa wanaweza kuhudumu kwa muda wa miezi 6, 12, 18, au 23. Wanaweza kuhudumu kimataifa chini ya muda wa miezi 18 ikiwa watalipia gharama ya usafiri.
- Wanandoa wanaweza, kwa gharama yao, kuchukua likizo ya kutokuwepo, kwa kawaida siku 7 hadi 10, kurudi nyumbani kwa ajili ya tukio la dharura la familia.
- Malipo ya nyumba yamewekewa kizuizi. Wanandoa hawalipi zaidi ya kiasi fulani cha fedha kilichowekwa kwa ajili ya makazi, ikijumulisha kodi, huduma, na samani.
- Makazi yatakuwa salama na ya kustarehesha. Misheni au ofisi za eneo hutafuta makazi safi, yaliyo na samani ya wastani, na yasiyo na bei ghali.
- Ratiba ina mahitaji machache. Wanandoa hawahitajiki kufuata ratiba na masaa ya kazi na shughuli sawa na vijana wamisionari.
- Mawasiliano na familia hufanyika mara nyingi. Wanandoa wanaweza kuwasiliana na familia zao zaidi kuliko ilivyoainishwa kwa wamisionari vijana.



WAKATI AMBAPO
Pornografia
Inaipiga Nyumba
—WAKE NA WAUME
Wote Wanahitaji
Kuponywa

Nimeshuhudia mimi mwenyewe kuwa nguvu za Mwokozi za kuponya zinaweza kuwafikia wake na vilevile waume wakati ambapo waume wanapambana na utawaliwa wa pornografia.



Jina limefichwa

Katika muda wa miezi sita ya kwanza kama askofu, nilikuwa na wanandoa kadhaa katika kata yangu waliokuja kwangu katika imani kunieleza kuhusu mapambano ya waume zao na matumizi ya pornografia. Katika baadhi ya visa, mke alikuwa bado angali katika mshituko wa kutambua siri hiyo ya kusikitisha; wengine walikuwa na habari kwa miezi au miaka mingi.

Nimemwonea huruma kila mmoja wa wanandoa hawa na nimejionea nguvu za Mwokozi za ukombozi kadiri nilivyokuwa nikishauriana mara kwa mara na kwa uangalifu

na kila mmoja wa ndugu hao ili kuwasaidia “kuikata mi-nyororo . . . ambayo ingewafunga [wao]” (2 Nefi 9:45)

Pengine mibubujiko mikuu ya Roho imekuja, hata hivyo, pale nilipokutana na wake zao. Nimegundua kwa-amba, huku baadhi ya vidonda vikiwa ni vya hivi karibuni na vingine vimekuwa makovu kutokana miaka mingi ya kuathiriwa, kina dada hawa wote hukabiliana na maumivu makubwa ya kiroho yanayosababishwa na maswali kama vile, “Mimi nimefanya nini kilichosababisha yeye asivutiwe na mimi?” au “Ni kwa nini yeye anataka kudhania kuwa yuko na mtu mwingine badala kuwa na mimi?”

Kwa sababu ni mume ambaye amefanya makosa, ni rahisi kwa askofu kuonelea kuwa ni mume ndiye anayehitaji zaidi funguo za kufungua nguvu za Mwokozi za uponyaji, lakini nimejifunza kuwa mahitaji ya mke kuponywa uchungu na maumivu ni makubwa kama vile yalivyo mahitaji ya mume kuponywa dhambi na tamaa zisizotulizika.

Katika mahubiri yake kwa Wanefi, nabii Yakobo ali-washutumu wanaume kwa kukosa kuwa waaminifu kwa wake zao, “ambao wengi wao mawazo yao [yalikuwa] ya upole sana na wasafi kimwili na wadhaifu mbele ya Mungu, kitu ambacho ni cha kupendeza kwa Mungu” (Yakobo 2:7). Aliendelea: “Mmevunja mioyo ya wake zenu wapole . . . kwa sababu ya mifano miovu mbele yao; na vilio vya mioyo yao kwa sababu yenu vinamfikia Mungu” (Yakobo 2:35). Nimeshuhudia vilio hivi kwa macho yangu. Mara nyingi vinatokana sio tu na hisia za kina za mke kusalitwa zilizosababishwa na mumewe kutawaliwa na pornografia lakini pia kutokana na maneno ya kudhalilisha na tabia ya ugomvi au ukali inayotokea mara nyingi kama athari ya mapambano yake ya ndani ya mume mwenyewe. Sio jambo geni, kwa kweli, kwa mwanaume ambaye tabia zake zimejulikana kumtupia mkewe lawama kwa sababu ya hizo tabia zake, akidondoa vitendo mbalimbali ambavyo amefanya au kukosa kufanya. Cha kusikitisha zaidi, si ajabu pia kwa mkewe kuanza kutafakari haya na pengine hata kuamini lawama hizi.

Mojawapo ya wanandoa kama hawa waliketi ofisini mwangu baada ya mume kufichua mazoea yake ya kutazama pornografia aliyokuwa nayo tangu ujana wake. Wakati alipokuwa akisikiliza somo la Muungano wa

Usaidizi wa Kina Mama juu ya mahubiri ya Dada Linda S. Reeves katika Mkutano Mkuu wa Aprili 2014, “Ulinzi dhidi ya Pornografia—Nyumbani Ambamo Kristo ni Kitovu Chake,” mkewe alianza kutambua katika tabia za ukorofi za mumewe kuja kwake mielekeo ambayo mwalimu alikuwa akieleza. Kufuatia somo hilo, mke alimkabili mumewe na swali hilo, na alikiri siri hiyo aliyokuwa akificha kwa muda mrefu sana. Kujistahi kwake ambako tayari kulikuwa kumeathirika mno sasa kulijumuishwa na chuki inayowaka. Wakati wa mkutano wao wa kwanza nami, walihangaika kuona ni kwa namna gani ndoa yao ingeweza kuendelea. Niliwahakikishia kuwa kulikuwa na matumaini, nikatoa ushauri wa kwanza, kisha nikawaalika tena waje na wakutane nami kila mmoja peke yake.

Pamoja na maombi ya bidii ambayo nilitoa katika matayarisho ya mikutano hiyo, pia nilifanya mrejeo wa




NI KWA NAMNA GANI VIONGOZI WA UKUHANI WANaweza KUSAIDIA:

Viongozi wanapowasaidia wenza wa waumini ambao wanapambana na pornografia, juhudi zao za kuhakikisha kuwa wenza hawa wanaona kuwa wamesikika na kueleweka zinaweza kuwa muhimu sawa sawa na ushauri wowote wanaoweza kuutoa. Zingatia mapendekezo yafuatayo kutoka Nyenzo za Kuhudumu (ministering.lds.org):

- Kutaneni pamoja mara kwa mara na kutoa usaidizi.
- Sisitiza uwezo wa Mwokozi wa kutoa uponyaji binafsi kwa mke au mume wa mtumiaji wa pornografia (ona Alma 7:11 na Mathayo 11:28–30).
- Kwa wakati unaofaa, mualike mhusika kuzingatia kuhudhuria mkutano wa kikundi cha usaidizi kupitia mpango wa walio katika hatua za uponyaji kwa watawaliwa

na mazoea au kikundi kingine cha usaidizi kama hicho.

- Msaidie mkewe au mumewe kuelewa kuwa anaweza kupata maongozi yake yeye binafsi kujua jinsi atakavyoweza mipaka wazi katika uhusiano na nyumbani.
- Msaidie mkewe au mumewe kutafuta rafiki mwaminifu au mwana familia ambaye anaweza kumpa usaidizi wa maana kwa muda unaoendelea.
- Saidia mtu anayetumia pornografia kuwajibika kwa matendo yake na kumsaidia mkewe au mumewe.
- Zingatia kumwelekeza mke au mume wa mtumiaji wa pornografia kwa msaada wa kitaalamu au anapoweza kupata ushauri nasihi. Baini nyenzo katika eneo lenu zinazotoa huduma kulingana na kanuni za injili.



Chini: Kerri alipata kuvunjika moyo alipogundua changamoto iliyomkamata mume wake kuhusu pornografia, lakini alipata matumaini na uponyaji kupitia kwa Yesu Kristo na Upatanisho Wake.

mapendekezo yaliyotolewa katika Nyenzo za Kuhudumu katika LDS.org, hasa katika misaada kwa ajili ya kuwasaidia wanandoa ambao waume au wake zao ni watumiaji wa pornografia, ambapo nilisoma yafuatayo: “Onyesha upendo na masikitiko yako kwake binafsi, vilevile kwa mumewe au mkewe. Bainisha kuwa yeye si wa kulauliwa kwa ajili utumiaji pornografia wa mwenzake au tabia yake isiyo ya kuridhisha na hatarajiwi kuvumilia tabia ya unyanyasaji.”

Nilipokutana na dada huyu, nilitii ushauri huu na kuongezea hakikisho kuwa vitendo vya mumewe kamwe havikusababishwa na yeye, wala kuhusu kitu ambacho alikuwa amekifanya au amekosa kufanya, lakini yalikuwa yanahusu mapambano ndani ya mume mwenyewe. Nilitazama wimbi la ahueni na faraja likimfunika alipokuwa akimeza maneno haya na kusikia uthibitisho wa Roho kuwa hakika yalikuwa ya kweli. Mwishoni mwa mahojiano, alionba ikiwa ningeweza kumpa baraka za ukuhani. Niligundua kuwa ilikuwa ni kwangu mimi pekee ndiko ambako angeweza kunijia kwa ajili ya baraka kama hizi, kwa vile alipendelea jambo lake hili lingesalia kuwa lake binafsi na si la familia wala marafiki.

Ili kusaidia katika mchakato wa uponyaji huu, nilimwalika mumewe kuhudhuria mkutano wa mtaani wa kikundi cha walio katika hatua za uponyaji cha Watakatifu wa Siku za Mwisho waliotawaliwa na mazoea mabaya, nilimhimiza mkewe kukutana na kikundi kama hicho cha waume au wake na wana familia. Aliniezeza kuhusu faraja aliyokuwa akiisikia kutokana na kukutana na kina dada wengine ambao walielewa alivyokuwa akiteseka

na matumaini iliyompa kuona wanandoa ambao walikuwa wamepitia majaribu kama yake na walikuwa wameweza kukabiliana nayo wakiwa pamoja.

Miezi kadhaa imepita sasa tangu mkutano wangu wa kwanza na wanandoa hawa, na upendo wangu na uhusiano wangu kwao umeongezeka kama matokeo ya mikutano yetu mingi. Huku nikitambua kuwa safari yao haitakosa changamoto, ni furaha kwangu kufahamishwa kila mwezi unapopita kuwa mumewe amejiepusha na tamaa na pornografia na kumwona mkewe akizidi kujiona mwenye kustahiki ndani yake na kujiamini, kitu ambacho tayari kinaonekana wazi.

Katika mahojiano ya hivi karibuni nao, uchungu na machozi yaliyokuwepo katika mikutano yetu ya awali yamebadilishwa na sasa ni tabasamu za mara kwa mara na hata vicheko. Lakini pengine matokeo makubwa zaidi yamekuwa matumaini—matumaini kuwa sio tu kuwa ndoa yao inaweza kundelea lakini pia ina uwezo wa kuwa kitu kizuri na cha kuwainua.

Ninatambua kuwa, kwa bahati mbaya, sio wanandoa wote wanashuhudia matokeo haya. Baadhi ya ndoa huvunjika wakati mtawaliwa na pornografia anapokataa kuchukua hatua ya kurekebika. Bila kujali ni njia ipi mume atachagua, hata hivyo, ni-mejifunza kuwa ushauri wa kuwahudumia wake hawa umetokana na maongozi ya kiungu. Ninatumaini kuwa hakutakuwepo na dada yeyote katika hali hii atakayehisi kuwa hatiliwi maanani, anahukumiwa vibaya, au kukosa kueleweka na askofu wake. Huduma ya askofu ni njia muhimu ambayo kwayo Mwokozi anadhihirisha nguvu Zake kikamilifu ili kuponya kila moyo—hata ile ambayo “ilikuwa imejeruhiwa na vidonda vikubwa” (Yakobo 2:35). ■



USHAURI NA FARAJA KWA WENZA

“Sisi kama viongozi pia tuna masikitiko makubwa kuhusu wenza na familia za wale wanaoteseke kwa kutawaliwa na pornografia. Mzee Richard G. Scott amesih: ‘Ikiwa uko huru kutokana dhambi kubwa wewe mwenyewe, usiteseke bure kwa matokeo ya dhambi za mwingine. . . . Unaweza kuona huruma. . . . Lakini hupaswi kujitwika hisia za majukumu ya matendo hayo.’ Fahamu kuwa hauko peke yako. Kuna usaidizi. Mikutano ya kupata nafuu kwa waume au wake inapatikana, ikijumuishwa kupitia njia ya simu, ambayo inamruhusu mume au mke kupiga simu na kushiriki kutoka nyumbani kwao wenyewe.

Linda S. Reeves, mshauri wa pili katika Urais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, “Ulinzi dhidi ya Pornografia—Nyumbani Ambamo Kristo ni Kitovu Chake,” *Liahona*, Mei 2014, 16.

Walinzi JUU YA MNARA

“Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha Bwana, msiwe na kimya.”

Isaya 62:6

Walinzi

Walinzi walikuwa askari wa zamu waliowekwa kwenye ukuta au ndani ya mnara ili kuweza kuchunga na kuonya kuhusu hatari zinazokaribia kutoka mbali. Waliajiriwa kulinda miji na pia mashamba ya mizeituni, mashamba, na malisho.

Aina ya Minara

Minara katika kuta za mji mara nyingi ilijengwa karibu na milango au katika kona (ona 2 Mambo ya Nyakati 26:9). Minara yote miwili ya langoni na pembeni ilitoa nafasi nzuri ya kuweza kuona hatari iliyokuwa ikikaribia na kujikinga dhidi ya mashambulizi ya adui (ona 2 Mambo ya Nyakati 26:15).

Ngome au minara ya kimbilio kawaida ilikuwa

majengo yasiotegemezwa popote ambayo ilikuwa imejengwa milimani au sehemu nyingine kimkakati. Mara nyingine ilikuwa kubwa kiasi cha kuwa mahali pa mwisho pa kukimbilia kwa watu wa mji mzima walipokuwa wakishambuliwa (ona Waamuzi 9:46–52).

Minara katika mashamba ya mizeituni, mashambani au malishoni ilikuwa majengo madogo yaliyokuwa yamejengwa kwa ajili ya kulinda mimea na mifugo dhidi ya wezi na wanyama (ona 2 Mambo ya Nyakati 26:10; Isaya 5:2; 27:3). Mara nyingi, sehemu ya chini ilikuwa chumba ambacho vifaa vilihifadhiwa.





WAJIBU WA KULINDA

Katika karne zilizopita, manabii wametimiza wajibu wao wakati

ambapo wamewaonya watu kuhusu hatari inayokaribia. Mitume wa Mungu kama ilivyo ada huchunga, huonya, na hunyoosha mkono kuwasaidia wale wanaotafuta majibu kwa maswali kuhusu maisha.

Mzee M. Russell Ballard wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, "Mungu yuko kwenye Usukani," *Liahona*, Nov. 2015, 25.

KWELI ZA BIBLIA



Katika Agano la Kale, Bwana mara nyingine analingani nishwa na ngome au mnara wa kimbi-lio (ona Zaburi 18:2; 61:3; Mithali 18:10; 2 Samweli 22:3),

na manabii mara nyingine hulinganishwa na walinzi (ona Isaya 62:6; Yeremia 6:17; Ezekieli 3:17; 33:7; Hosea 9:8; Mika 7:4).

"Nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi, sikia neno hili litokalo katika kinywa changu, ukawape maonyo haya yatokayo kwangu" (Ezekieli 3:17; ona pia Ezekieli 33:1-7).

Walinzi Juu ya Mnara:

Wana mtazamo wa juu. Kama watumishi wenye mamlaka wa Mungu, manabii wametengwa kutoka mbali na dunia, wanamkaribia, na wanaruhusiwa kuona mambo kwa mtazamo wa mbinguni.

Huona mambo ambayo wengine hawawezi kuona. "Lakini mwonaji anaweza kujua vitu vilivyopita, na pia vitu vitakavyokuja, na kupitia kwao vitu vyote vitafunuliwa, kwa usahihi zaidi, vitu vya siri vitadhahirishwa, na vitu vilivyofichwa kuletwa katika nuru, na vitu visivyojulikana vitajulishwa kwao, na pia vitu ambavyo havingejulikana vitajulishwa na wao" (Mosia 8:17).

Wako macho. Manabii wana wajibu muhimu wa kutuonya kuhusu hatari inayokaribia, na wataendelea kufanya hivyo bila ya kujali maoni ya umma au mienendo katika jamii.

Wanaonya kuhusu mambo fulani yakiwa bado yako mbali na kutendeka. "Nabii hushutumumu dhambi na kutabiri matokeo yake. Yeye ni mhubiri wa haki. Ikibidi, manabii waweza kuongozwa kutabiri siku za usoni kwa manufaa ya wanadamu" (Mwongozo kwa Maandiko, "Nabii," lds.org/scriptures/gs).

Hutoa usalama na ulinzi. Kwa kutii onyo la manabii, tunaweza kupata usalama na kuepukana na misiba ambayo inaweza kutupata, binafsi au pamoja, ikiwa hatutatii. ■



NAFASI YA PILI

Mara ya kwanza nilipokutana naye, nilikuwa nimeshikilia fidla yangu.

Alijiburuzi hadi karibu nami wakati nilipokuwa nikitembea kuelekea chumba cha chakula cha mchana, sanduku langu la fidla likipigapiga mguu wangu.

“Fidla,” alisema huku akinikaribia.

“Ndio,” nilisema.

Kwa kweli sikuwa nimewahi kuzungumza na mtu ye yote mwenye ulemavu na sikujua kipi kingine cha kusema. Alinifuata na hadi kwenye meza yangu na kuketi kando yangu, akiashiria sanduku la fidla yangu.

“Fidla,” alisema tena.

Nilifungua sanduku langu na macho yake yakang’aa. Kwa fujo sana, akakwaruzi nyuzi zake. Moyo wangu ulipiga kwa mshindo nilipofikiria uzi ukikatika kutoka fidla yangu, na pole-pole nikafunga sanduku. Alinizingira kwa kumbatio kabla ya kuondoka.

Nilimuona mara nyingi baada ya hii.

“Fidla,” alisema huku akikaribia.

Kila aliponiona, angevingisha mikono yake mabegani mwangu huku akibusu juu ya kichwa changu.

Kwa muda ulisalia katika shule ya upili, kila mara nilijaribu kumkwepa nilipomwona akija. Aliponipata na kunigubika na kumbatio na busu zake zilizolowa mate, nilizivumilia kwa sekunde chache na tabasamu la kulazimisha kisha ningeondoka haraka bila ya kusema lolote.

“La, hashi,” nilisemea mashavuni nilipomwona kwenye burudani yangu ya okestra ya mwisho wa shule ya upili. Baada ya burudani, alipindapinda kuelekea nilipokuwa nimesimama na marafiki zangu nje ya ukumbi.

Marafiki zangu walirudi nyuma aliponikaribia akitabasamu, mikono yake ilikuwa wazi tayari kukumbatia.

“William!”

Niligeuka na kumwona mwana-mke akikimbia pole pole kuelekea tulipokuwa.

“Pole,” alisema, wakiunganisha mkono yao. “William anapenda fidla. Aliniomba nimlete katika burudani ya usiku wa leo. Twende, mpenzi.”

Hadi wakati huo, sikuwa nimegundua kuwa hata sikujua jina lake. Nilikuwa nimekutana na William miaka

miwili kabla lakini nilitumia muda mwingi nikimkwepa kiasi cha kwamba sikuwa nimefanya jitihada ya kweli ya kumjua. Nilipomtazama William na mamake waki-ondoka, mawimbi ya aibu yalipita juu yangu.

Miaka kadhaa baadaye, baada ya kuolewa, nilijifungua

mvulana mzuri mdogo aliyekuwa na Down’s Syndrome ambaye tulimwita Spencer. Mara nyingi nilipata mawazo yangu yakiwa juu ya William kwa muda mrefu nikiwa namwangalia mwanangu, na nikawa najiuliza ikiwa Spencer angekuwa na matukio sawa na yake. Watu wangemkwepa kwa sababu alibusu sana au alibana sana alipokumbatia? Rika lake wangekuwa hawana faraja kwa sababu ya udhaifu wake?

Spencer alipokuwa na umri wa mi-ezi minne, nilimpeleka katika hospitali ya mtaani kwetu ili kumwona tabibu. Nilipokuwa namuondoa kwenye gari, niliwaona watu wawili wakiondoka hospitalini. Kwa mshangao, niligundua ilikuwa William na mamake.

“William!” Nilimwita tulipokaribia, moyo wangu ukipiga kwa nguvu.


“Halo!” Alitembea kwa mapenzi katika maegesho, na tabasamu kubwa usoni. Alinyoosha mkono wake mbele na kushika wangu kwa salamu za shauku kubwa.

“Hujambo?” Nilimwuliza.

“Fidla,” alisema, msisimko ukionekana machoni mwake.

Fidla. Alinikumbuka pia. “Ndio,” Nilisema kwa sauti ya kwikwi machozi na kicheko, “nilipiga fidla.”

Tulipokuwa tukizungumza, moyo wangu uliinuka kwa maombi kwa ajili ya huruma nyororo za Baba mpendwa wa Mbinguni ambaye alijua kiasi gani nilitamani kukutana na William tena. Ninashukuru kwamba Mungu aliniona—mama kijana aliyekuwa amezidiwa na changamoto za afya ya mwanangu na wasiwasi wa siku za usoni—na kunipa jambo ambalo lilinikumbusha kuwa Yeye anatufahamu. ■ Kaylee Baldwin, Arizona, Marekani





Nilimsikia mwanamke yule akiweka kilichoonekana kuwa kiasi kikubwa sana cha sarafu kwenye kaunta kulipa bili yake.

NENDA UKAMSAIDIE

Nilimwambia kwenye foleni katika kituo cha mafuta. Mbele yangu, mama mwenye watoto wawili wadogo aliagiza petroli ya dola \$3 na aiskrimu koni mbili za vanila.

Kwa mtazamo wa niliweza kuona kwamba walikuwa na pesa kidogo sana. Watoto walikuwa miguu mitupu na walikuwa wamevaa nguo zilizochakaa.

Nilimsikia mwanamke yule akiweka kilichoonekana kuwa kiasi kikubwa sana cha sarafu kwenye kaunta kulipa bili yake.

Baada ya kulipia petroli yangu, nilitoka nje na kutupia jicho gari la mama yule. Lilikuwa modeli ya zamani ambayo huenda ilisafiri maili chache sana ikilinganishwa na matumizi ya petroli.

Nilihisi kichomi cha huruma kwa mama huyu wa watoto wawili, lakini

niliwasha pikipiki yangu na kuendelea na siku yangu.

Chini ya dakika moja katika safari yangu kwenye barabara kuu, sauti iliniija: “Nenda ukamsaidie.” Msukumo ulikuja mara mbili.

Nilitingisha kichwa, nikifikiria kuwa huenda alikuwa ameshaondoka tayari. Ni nini ningemwambia hata hivyo?

Sauti ilikuja wazi mara ya tatu: “Nenda ukamsaidie!”

Niligeuka kuelekea kwenye kituo kile cha mafuta, nikijaribu kufikiria kile ningemwambia ikiwa angekuwa bado yuko mahali pale.

Nilipowasili, niliona kwamba milango ya gari lake ilikuwa wazi. Alikuwa kwenye kiti cha dereva, na watoto wake wadogo wawili walikuwa wakifurahia aiskrimu kwenye kiti cha nyuma.

Nilitoa ombi dogo, nikimwomba Baba wa Mbinguni anijulishe kile ambacho ningesema. Sauti iliniambia, “Jitambulishie na uulize ikiwa anahitaji usaidizi.” Nilikaribia gari lake na kujitambulisha. Nilimueleza kuwa nilihisi msukumo wa kumuuliza ikiwa alihitaji usaidizi wowote.

Alianza kulia na kusema, “Nimemaliza tu kumuomba Yesu, nikimwomba atume mtu wa kunisaidia.”

Baba wa Mbinguni alikuwa amejibu maombi yake. Nililipa kujaza mafuta gari lake na nikampa nambari ya simu ya mtu katika akidi yetu ya wazee ambaye alikuwa akiajiri kwa wakati huo. Sijui yaliyomkuta mama yule kijana baadaye, lakini ninashukuru nilifuata msukumo wa kumsaidia. ■

Thomas Robbins, California, Marekani.

USIPIGE RISASI!

Bob na mimi tuliketi kwenye gari letu la polisi, tukisubiri ishara ya harakati barabarani. Tulikuwa tumeanza uchunguzi wetu masaa mawili yaliyopita baada ya kuliona gari ambalo lilikuwa limetajwa katika tahadhari ya redio ya polisi.

“Wizi wa uporaji unaendelea,” tahadhari ilikuwa imesema. “Wanaume wawili, wote wana silaha. Walikuwa punde tu wameonekana kwenye gari

la rangi ya machungwa. Mashahidi wanasema wanaume hao ni wakatili na wako tayari kupiga risasi.


Mfululizo wa wizi wa kutumia silaha ulikuwa umefanyika katika eneo hilo, lakini licha ya juhudi zetu bora, wezi hao walikuwa wametutoroka mara kwa mara. Fikira hizi zilipotea akilini mwangu punde tu nilipoona maumbo mawili yakitoka kwenye nyumba moja kwenye

barabara hii iliyojaa giza na kuingia kwenye gari la rangi ya machungwa. Walikuwa sasa wanaelekea upande wetu.

“Nikiomba kikosi cha usaidizi,” Nilisema. “Washukiwa wanaelekea kaskazini kutoka eneo tulioko.

Kikosi chetu cha usaidizi, wapelelezi wawili wenye nguo za kiraia katika gari lisilo na alama, walienda mbele ya gari lile huku Bob na mimi

Licha ya misukosuko ya wakati huo, nilisikia sauti. Ilikuwa tulivu lakini yenye mamlaka na nguvu: “Usipige Risasi!”



tukifuata. Baada ya gari zetu tatu kuingia kwenye daraja, kikosi chetu cha usaidizi kilisimama ghafla kufunga daraja mbele ya gari la rangi ya machungwa na sisi tukasimama nyuma yake, tukiwaweka kati washukiwa wetu. Haraka sana, gari lilisimama na maumbo yote mawili yakatoweka machoni petu.

“Tokeni kwenye gari na mikono yenu juu ya vichwa vyenu!” Niliamuru baada ya kutoka nje ya gari langu. Hakuna aliyejibu.

Imara na tayari kupiga risasi, niliamuru tena, “Tokeni kwenye gari na mikono yenu juu ya vichwa vyenu. Fanya sasa hivi!”

Ghafla dereva aliinuka na kugeuka upande wangu. Niliweza kuona kitu ambacho kilichochovywa kwenye nikeli kikitoa nuru ghafla mikononi mwake.

Mafunzo yangu ya kipolisi na maarifa ya kawaida yaliamuru nipige risasi ili kuokoa maisha yangu. Lakini juu ya wasiwasi ya wakati huo, nilisikia sauti. Ilikuwa tulivu lakini yenye mamlaka na nguvu: “Usipige Risasi!”

Nilitarajia kupigwa risasi wakati wowote, lakini nilisubiri mtu kutoka ndani ya gari apige risasi ya kwanza. Badala yake, dereva aliinua mikono yake, akainua juu ya kichwa chake kitu kilichoonekana kama bastola, na kushusha mikono yake kwenye mapaja yake.

“Simama tuli!” Nilisema huku niki-songea gari kwa kasi. “Usisoge!”

Kipindi hicho kilionekana kama kipindi cha televisheni—hadi nilipogundua kwamba wale magaidi sugu ndani ya gari kwa kweli walikuwa wasichana wawili waliojawa na hofu.

Nilichodhania kuwa bastola ilikuwa ni kifungo cha mkanda wa kiti.

Wasichana wale, punde tulikuja kujua kwamba, walikuwa wameazima lile gari toka kwa wapenzi wao. Hawakujua walikuwa wanaume wa aina gani.

“Nilidhani umekufa, Cal!” Bob aliniambia baadaye. “Nilikuwa karibu kupiga risasi. Sijui ni kwa nini sikufanya hivyo.”

Wale wapelelezi wawili katika lile gari lililokuwa halina alama walisema maneno hayo pia, ingawaje hakuna aliyesikia sauti ile isipokuwa mimi. Ninajua kuwa ni nguvu za mbinguni pekee ndizo ambazo zingeweza kuwaokoa wasichana wale kutokana na kifo na maafisa wanne wa polisi kutokana na kufanya kosa la maafa hayo. Tukio hili lilinipa ufahamu hakika kuwa Baba yetu wa Mbinguni anaweza kuingilia kati na atafanya hivyo kwa manufaa yetu. ■

Jina limefichwa

WAFUNDISHE KUSOMA KITABU CHA MORMONI

Wakati tulipokuwa tukihudumu katika Misheni ya Geneva Switzerland, Nilipewa mwito na kusimikwa kuwa rais wa tawi, na mke wangu alipewa mwito wa kuwa rais wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama. Pamoja tulifanya kazi kwa nguvu zetu zote ili kuimarisha tawi hilo lililokuwa na changamoto.

Ingawa lilianzishwa miaka ya 1960, tawi hilo halikuwa na ubatizo wote kwa miaka mingi na halikuwa limetuma wamisionari misheni kwa miaka 15.

Ilikuwa bayana kwamba tulihitaji usaidizi wa Bwana ili kupata suluhi-sho la changamoto nyingi ambazo zililikabili tawi hilo. Baada ya kuomba kuhusu changamoto za tawi hilo, Roho wa Bwana aliniambia, “Wafundishe waumini kusoma Kitabu Cha Mormoni, nawe utafanikiwa.”

Mara moja, tulifanya mipango ya kukubaliana na waumini wote waa-nze kusoma Kitabu cha Mormoni.

Matokeo ya ajabu yalifuata. Amani na Roho ilirudi katika tawi. Familia mpya zilijiunga na Kanisa. Kwa sababu ya kutiwa motisha na hamu ya kuhudumu, kijana mmoja aliondoka kwenda misheni. Ndoa kadhaa zilizokuwa na matatizo ziliimarishwa, na familia zikawa na umoja zaidi. Tawi hili linaendelea kupiga hatua leo.

Sisi na waumini katika tawi lile tulishuhudia wenyewe nguvu za kimiujiza za Kitabu cha Mormoni. Kwa kweli ni jiwe la katikati la tao la dini yetu na kwa ushuhuda wetu wa injili na wa Yesu Kristo. Tunakipenda kwa moyo wetu wote. Ni chanzo cha maarifa yasiyoisha na yasiyobadilika.

Tukio hili lilitufunza kuwa Kitabu cha Mormoni ni njia ya hakika kabisa ya kuwasaidia ndugu zetu na dada zetu kutoka katika vivuli vya giza la kiroho ambalo limezingira dunia. Kitabu hiki kinaleta amani, shangwe, furaha, na hamu kubwa ya kumfuata Mwokozi Yesu Kristo. ■
Emilien Rioux, Quebec, Canada

Kutambua Mambo Bandia ya Shetani

Na Dennis C. Gaunt

N ilikuwa nikiweka noti za dola za Kimarekani ndani ya pochi yangu nikiwa katika duka la vyakula, wakati jicho langu lilivutiwa noti moja. Nilidhani rangi ya kijani kibichi ilikuwa nyepesi kidogo kuliko zingine, kwa hivyo niliichunguza kwa karibu. Halafu nikagundua ile picha ya Rais George Washington ilionekana kuwa duni. Hata karatasi yake ilionekana kuwa mbovu. Ilikuwa bandia! Karani aliibadilisha na noti ya dola halisi kisha akampa meneja wa duka ile noti bandia.

Nimefikiri sana kuhusu ile noti ya dola bandia kutoka siku hiyo. Niliwaza ni kwa muda gani ilikuwa imetumika na ni watu wangapi ilikuwa imewapumbaza kwa miaka mingi. Kwa kweli, kama sikuwa mwangalifu, pia nami ningekuwa nimepumbazwa. Lakini kwa kuilinganisha na ile halisi na kuzingatia tofauti zake badala ya kufanana kwake, niliweza kutambua kuwa ilikuwa bandia.

Kitabu cha Mormoni kimejaa mifano ya watu wenye kubuni mambo bandia ya kiroho, ambao walifuata

mbinu za Shetani za udanganyifu na kuhadaa wengine kwa manufaa yao. Kwa kuchunguza hila na mbinu zao, tunaanza kugundua makosa yao kwa njia sawa na ile ambayo jicho lenye uzoefu linaanza kugundua tofauti kati ya fedha halisi na bandia. Tunavyozidi kufundisha jicho letu kutambua tofauti, ndivyo tutakavyokuwa tumejitayarisha vyema kufichua mambo bandia leo na kupinga uongo wake.

Kufanya Upelelezi kuhusu Mambo Bandia ya Shetani

Shetani anatafuta kutupotosha kwa njia ya aina yake ya vitu bandia vya kiroho, na ikiwa hatutakuwa waa-ngalifu, tutapumbazwa. Rais Joseph F. Smith, (1838–1918) alionya: “Shetani ni mwigaji hodari, na kadiri ukweli wa injili halisi unavyotolewa kwa wingi ambao unazidi kuongezeka ulimwenguni, vivyo hivyo naye anasambaza sarafu bandia ya mafundisho ya uongo. Jihadhari na sarafu yake bandia, haitakununulia chochote ila tu masikitiko, huzuni na kifo cha kiroho.”¹

Kinga bora tuliyonayo dhidi ya

Tunapokabiliwa na mambo ya udanganyifu wa kiroho, Kitabu cha Mormoni kinaweza kutusaidia kuamua kilicho cha kweli na kile ambacho sicho.

kupumbazwa na mambo bandia ya Shetani ni kuzijua vizuri kadiri tuwezavyo kweli hizi za injili. Tukijua ukweli kwa kina zaidi, ndivyo itakavyokuwa rahisi kutambua tofauti wakati Shetani anapowasilisha vitu vyake bandia mbele yetu. Kwa hivyo anapofanya hivyo, tunachohitaji kuchunguza ni tofauti na wala siyo kwa yale yanayofanana nayo, kama vile nilivyofanya kwa noti zangu za dola, kwa sababu hapo ndipo uongo utafichuliwa kila mara.



Rais Ezra Taft Benson (1899–1994) alifundisha: “Kitabu cha Mormoni huwaanika wazi maadui wa Kristo. . . . Mungu, kwa uelewa wake wa mambo kabla hayajawa ndipo akakiunda Kitabu cha Mormoni ili tupate kuweza kuona makosa na kujua jinsi ya kupambana na elimu ya uongo, kisiasa, kidini na falsafa za fikra za wakati wetu.”²

Leo tuko vitani dhidi ya Shetani. Sisi, kama jeshi lolote, tunahitaji kujua kile ambacho adui anafanya. Kujua wakati na mahali ambapo adui

atafanya mashambulizi, kwa mfano, yaweza kuwa taarifa ya thamani kubwa. Hiyo ndiyo sababu istilahi ya kutafuta habari kama hii inaitwa “kufanya upelelezi.” Kumfahamu adui yetu ni kuwa mwerevu kuliko adui yetu huyo. Kitabu cha Mormoni kina-weza kutusaidia “kufanya upelelezi” kuhusu mbinu bandia za Shetani.

Hotuba Ya Kujipendekeza Ni Bandia

Zaidi ya nusu ya wahusika katika mambo bandia katika Kitabu

cha Mormoni wanatumia hotuba za kujipendekeza na haiba kutimiza malengo yao. Kwa mfano, Sheremu “alikuwa na ufahamu kamili wa lugha ya watu wale; kwa sababu hiyo, aliweza kutumia maneno mengi ya kujipendekeza, na alikuwa na uwezo mkubwa wa kuzungumza, kulingana na nguvu ya ibilisi” (Yakobo 7:4). Makuhani waovu wa mfalme Nuhu walinena “maneno ya hovyonyo na ya kujipendekeza” (Mosia 11:7), na hivyo basi kuwafanya watu kujiingiza

katika ibada za sanamu na uovu mwingine. Korihori alipata matokeo kama hayo katika siku zake, “akipotisha mioyo ya wengi” (Alma 30:18). Amalikia na Gadiantoni wote wawili walitumia uhodari wao wa kutumia maneno ya kujipendekeza ili kujenga jeshi la wafuasi waovu (ona Alma 46:10; Helamani 2:4).

Hii siyo kwa bahati mbaya. Udanganyifu ni kina kifupi, unafiki, tupu, na umetiwa chumvi. Nefi alionya kuhusu wale “watakaofundisha kwa namna hii, mafundisho ya uwongo na yasiyofaa na ya kipumbavu, na watajifurisha miyoyoni mwao, na watajitahidi kumficha Bwana ushauri wao; na matendo yao yatakuwa gizani” (2 Nefi 28:9).

Maneno ya kujipendekeza mara nyingi hutumika kulaghai; kwa kawaida huwa na azimio la chini chini au ajenda iliyofichika. Udanganyifu unahusu mtindo zaidi kuliko kiini, na inavutia ubatili na kiburi cha mwadamu wa asili ndani yetu. Manabii wa Mungu, hata hivyo, wanatueleza ukweli rahisi lakini muhimu ambao *tunahitaji* kuusikia.

Kujipendekeza ni lugha ambayo Shetani huongea. Rais James E. Faust (1920–2007), Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza, alielezea: “[Shetani] sauti yake mara nyingi huonekana ikiwa na busara na ujumbe wake ni rahisi sana kuuhalalisha. Ni ya kusihhi, sauti ya kuvutia yenye toni nyororo. Siyo katili na wala haina mfarakano. Hakuna mtu ambaye angesikiliza sauti ya Shetani ikiwa ingesikika kama ya ukatili au dhalifu.”³



“[Sauti ya Shetani] ni ya kusihhi, sauti ya kuvutia. . . . Hakuna mtu ambaye angesikiliza sauti ya Shetani kama ingekuwa katili au dhalifu.”

Wakati ambapo ulimwengu unatupatia dhana, falsafa, au maoni ambayo yanaonekana kutufurahisha tu katika upuuzi wetu au kiburi chetu au mbona hii inaonekana kuwa rahisi hivi kiasi cha kutoaminika, hilo linapaswa kuwa onyo kwetu mara moja. Zichukulie dhana hizo kama bandia. Zilinganisha dhidi ya ukweli unaofundishwa na manabii wa Bwana. Tafuta tofauti, siyo kufanana kwake, na dhana zilizo bandia zitakuwa dhahiri.

Nehori—Mdanganyifu Maarufu!

Nehori alitumia waziwazi mtindo wa udanganyifu wa Shetani. Wacha tumchunguze kama jambo la utafiti wa mtu mdanganyifu wa kiroho. Nehori, ambaye mafundisho yake yanaonekana kukubali dhana ya mkombozi,

alikuwa maarufu na mhubiri mwenye haiba kubwa miongoni mwa Wanefi. Nehori aliweza kuwa na wafuasi wengi kwa kufundisha kwamba “wanadamu wote wataokolewa katika siku ya mwisho” na “watapokea uzima wa milele” (Alma 1:4).

Tunaweza kuona ni kwa nini ujumbe wa Nehori unaweza kuvutia sana? Alikuwa akifundisha kuhusu Mungu ambaye si mkali na ni mtulivu—Mungu ambaye, kwa vile anampenda kila mtu, atamwokoia kila mtu, liwe liwalo. Kwa hivyo endelea kufanya lolote utakalo, kwa sababu yote ni mema. Ni falsafa ya kuvutia ambayo ilikumbatiwa sana na watu wa siku za Nehori (ona Alma 1:5) kama ilivyo kwa watu wengi siku hizi. Tikiti ya bure ya kuingia mbinguni

inaonekana kuwa ni kitu ambacho watu wanataka.

Kwa hivyo kulikuwa na shida gani katika ujumbe wa Nehori? Sasa ngoja tuangalie hoja kuu za mjadala wake:

- Mungu aliumba wanadamu wote—kweli.
- Mungu anawapenda wanadamu wote—kweli.
- Hatupaswi kumwogopa Mungu—kweli.
- Tunapaswa kushangilia dhana ya wokovu—kweli.

Kufikia hapa, kuna kufanana kwini kati ya mafunzo ya Nehori na ukweli wa injili. Lakini kumbuka—kama vile ilivyo kwa pesa bandia, tunahitajika kuangalia tofauti, sio kufanana. Kwa hivyo wacha tuangalie hoja ya mwisho ya Nehori:

- Mungu atawapa wanadamu wote uzima wa milele—uongo!

Sasa hii ndiyo tofauti kubwa ambayo inatuelezea kuwa Nehori alikuwa mwenye udanganyifu wa kiroho. Wokovu kutokana na kifo cha kimwili *ni* hakika kwa wote, lakini wokovu kutokana na kifo cha kiroho inategemea hiari yetu ya kutubu. Ikiwa tutatubu, basi tunaweza kupokea uzima wa milele (ona Yakobo 6:11). Lakini hakuna cha bure.

Gidioni na Alma Walimtambua Mdanganyifu

Uovu wa Nehori ulifichuliwa siku ambayo alikutana na Gidioni,

mwalimu mwenye haki katika Kanisa la Mungu. Gidioni alikuwa amekabilihana na Mfalme Nuhu miaka kadhaa hapo awali na hivyo basi alikuwa na uzoefu na wadanganyifu wa kiroho (ona Mosia 19:4–8). Nehori “akaanza kubishana na Gidioni kwa ukali, ili awapotoshe watu wa kanisa; lakini [Gidioni] alimpinga, na kumwonya kwa maneno ya Mungu” (Alma 1:7). Gidioni alimtambua Nehori kama Mdanganyifu. Mara alipofichuliwa, Nehori aliamua kutumia mbinu nyengine ya Shetani—mauaji. Lakini kifo cha Gidioni hakikuwa bure. Watu walimleta mdanganyifu Nehori kwa Alma ili ahukumiwe.

Alma alitambua kuwa Nehori hakuwa tu na hatia ya ukuhani wa uongo na mauaji lakini pia ikiwa ungeachwa kuendelea, ukuhani wa uongo miongoni mwa watu, “unge-thibitisha maangamizo yao kabisa” (Alma 1:12). Kwa hivyo Nehori alihukumiwa kifo, na alikufa “kifo cha aibu” (Alma 1:15).

Gidioni na Alma ni mifano kwetu. Wakati tukiwa na Roho pamoja nasi, tutaona na kusikia “vile vitu vilivyo” (Yakobo 4:13). Tutatambua mipango na mbinu bandia za shetani “tukiwa na ufahamu kamili, kama mwangaza wa mchana ulivyo kwa giza la usiku” (Moroni 7:15).

Adui yetu wa “vitu bandia” ni mwe-revu, lakini kama Gidioni na Alma, tunaweza kuwa werevu zaidi. Kama vile nilivyoanza kugundua taratibu tofauti kati ya jozi yangu ya noti za dola, tunaweza taratibu kufundisha macho



SHETANI ANAENEZA UONGO

“Shetani, adui yetu, anataka

tushindwe. Anaeneza uongo kama sehemu ya juhudi zake za kuangamiza imani yetu. Kwa ulaghai anapendekeza kuwa mwenye wasiwasi, mwenye kushuku, mbeuzi ni ustaarabu na werevu, huku wale walio na imani kwa Mungu na miujiza yake ni wasiojua, vipofu, au wamepumbazwa. Shetani atatoa utetezi kuwa inapendeza sana kuwa na shaka kuhusu vipawa vya kiroho na mahubiri ya manabii wa kweli.”

Rais Dieter F. Uchtdorf, Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza, “Usiogope, Amini Tu,” *Liahona*, Nov. 2015, 78.

yetu na vilevile akili na roho zetu kutambua tofauti kati ya ukweli na uongo. Tunapofanya hivyo, tutawatambua wenye vitu bandia na kupinga uongo wao. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

MUHTASARI

1. Joseph F. Smith, *Mafundisho ya Injili*, to. la 5 (1939), 376.
2. *Teachings of Presidents of the Church: Brigham Young (1997)*, 280. Ezra Taft Benson (2014), 132.
3. James E. Faust, “Nguvu Ambazo Zitatuokoa,” *Liahona*, Jan. 2007, 4.

Kupima Baraka huko Madagaska

Na Mindy Anne Selu

Majarida ya Kanisa

Baada ya mkewe kuteseke kutokana na kuharibika kwa mimba yao ya kwanza, Solofo Ravelojaona alihisi kuwa maombi yao yalijibiwa mwaka mmoja baadaye kwa mimba yao ya pili. Yeye na mkewe, Hary Martine, wanachukulia kuza-liwa kwa binti yao kuwa mojawapo ya baraka zao kubwa zaidi. Solofo anaeleza, “Kwa sababu tulimwomba Mungu na akatupatia, tulimpatia jina ambalo, kwa Kimalagasi, linamaanisha ‘jibu la Mungu.’”

Solofo, kijana mkubwa kutoka Madagaska, anaamini kuwa Mungu hujibu maombi na kwa wakati wake anawabariki waaminifu. “Maisha ni magumu,” anasema Solofo, “na wakati watu wanapokosa kupata kile wanachotaka, wengine huanza kujiuliza, ‘Ni kwa nini hili limenitokea?’ Wanaweza kuacha Kanisa au kuwa na shaka na imani yao kwa Mungu. Lakini tunapoishi kulingana na injili na kusoma maandiko, inakuwa rahisi. Unapoishi kulingana na injili, kwa kweli unaweza kuona baraka.”


Kuishi katika nchi yenye shida kubwa, kama vile umaskini uliokithiri, kukosekana kwa utengamano serikalini, miundombinu dhaifu, na maafa, ni wazi kwa nini Solofo anasema maisha ni magumu. Lakini kwake, baraka ambazo kuishi kulingana na injili huleta zinashinda taabu zozote. “Siwezi hata kuhesabu baraka ambazo ninapokea, muradi tu ninaishi kulingana na injili,” anasema.

Kwa sababu Kanisa bado geni Madagaska (tawi la kwanza lilifunguliwa 1990), Solofo anasema kuwa sehemu ngumu zaidi ya kuwa muumini ni uvumi na kueleweka visivyo kwa Kanisa. Solofo anatoa maoni kuwa, kama vile ilivyokuwa katika maono ya Lehi ya mti wa uzima, “watu waweza kukosa kukubali injili kikamilifu kwa sababu wanaona aibu mbele za marafiki na wanaogopa kuwa watakataliwa na familia zao.” Kinachomfanya Solofo kuwa tofauti, anapendekeza, ni kuwa, “Sijawahi kuona aibu.” Ninaishi kulingana na injili, na kila mara mimi hutaka kushirikiana na wenzangu kazini, hata kama baadhi yao hawana moyo wa kutaka kujua.” Mara nyingi

Licha ya mageuzi makubwa ya kisiasa na hali ngumu za kiuchumi nchini mwake, Solofo anategemea baraka zinazotokana na kuishi kulingana na injili.

yeye hushiriki na wengine ushuhuda wake, kiasi cha kuwa wafanyikazi wenzake wamempa jina la utani la “mchungaji.”

Katikati ya mtikisiko wa kiuchumi na kisiasa, Solofo na Hary Martine wanategemea baraka za maagano yao ya hekalu (walifunga ndoa katika Hekalu la Johannesburg Afrika Kusini mwaka mmoja baada ya misheni zao—yake Uganda, na ya mkewe Madagaska), na pia imani yao kwa Bwana. “Nina injili, na mimi huweka tu maisha yangu mikononi mwa Mungu,” Solofo anaeleza. Anaweza kutegemea ushuhuda wake imara kwa sababu tayari ana imani katika “majibu ya Mungu.” ■



ZAZIDI KUHUSU SOLOFO

Unapenda kula vyakula gani?

Chakula tunachokula ni wali— wali kwa wingi. Mojawapo ya vitu ambavyo napenda kinaitwa *ravtoto*. Tunatumia kifaa maalum kuponda majani ya muhogo kwa vipande vidogo vidogo na kuvila na wali na nyama ya nguruwe.

Ni nini unapenda kufanya kwa wakati wako wa ziada?

Ninapenda kucheza kinanda, kuimba, na kusoma. Kwa sababu rais wa tawi alijua kuwa nilipenda kuimba na ningeweza kucheza kinanda, nilipoenda kwenye tawi, alisema, "Aa, tuna mtu wa kuiongoza kwaya," na nilijitolea. Hawakuwa na kwaya hapo mwanzoni lakini nilianza kuwafundisha, sasa wanaifurahia.

UKWELI KUHUSU MADAGASKA

Lugha: Kifaransa, Kimalagasi
Mji Mkuu: Antananarivo

KWA IDADI

Watu 22,005,222 (makadirio ya 2012)

Asilimia 50 ya wanyama wanao-patikana Madagaska hawawezi kupatikana mahali kwingine kokote duniani

Ni kisiwa cha 4 kikubwa zaidi duniani

Asilimia 60 ya vanilla dunia mzima usafirishwa ng'ambo kutoka Madagaska

KANISA KULE MADAGASKA

Watakatifu wa Siku za Mwisho
9,190

Kata na matawi 37

Vigingi 2

Misheni 1







**Na Mzee
Dale G. Renlund**

Wa Akidi ya
Mitume Kumi na
Wawili

KUWA IMARA KIROHO KUJENGA MELI ISIWOWEZA KUZAMA

*Tunahitaji msimamo imara wa kiroho wa kutosha ili
tuweze kuishi maisha yetu ya sasa kwa ufanisi na kuweza
kurudi salama nyumbani kwetu mbinguni.*

Mapema katika karne ya 17, Mfalme wa Uswidi, Gustav II Adolf, aliagiza kutengenezwa kwa meli ya kivita ambayo ingepewa jina *Vasa*. Meli hiyo ilileta taswira ya rasilimali nyingi, hasa mwaloni ambao ungetumika katika ujenzi wa chombo hicho. Gustav Adolf alisimamia kwa karibu sana ujenzi wake, akijaribu kuhakikisha kwamba *Vasa* ingefanikisha kikamilifu matumaini yake.

Baada ya ujenzi kuanza, Gustav Adolf aliamuru *Vasa* iwe ndefu zaidi. Kwa sababu nguzo za upana zilikuwa tayari zimejengwa kwa kutumia mwaloni wenyewe thamani, mfalme alielekeza kwamba wajenzi waongeze urefu wa meli bila kuongeza upana wake. Ingawaje waunzi walijua kuwa kufanya hivyo kungetia *Vasa* hatarini, walisita kumwambia mfalme jambo ambalo walijua hakuwa anataka kusikia. Walifanya alivyotaka. Gustav Adolf pia alisisitiza kuwa meli hii isiwe tu na staha moja ya mizinga bali mizinga kwenye staha tatu, na mizinga kubwa kabisa kwenye staha iliyokuwa juu kabisa. Tena, kinyume na busara yao, waunzi walifanya alivyotaka.

Agosti 10, 1628, *Vasa* ilianza safari yake ya kwanza. Baada ya *Vasa* kuondoka bandarini, upepo mkali ulipuliza tanga zake, na meli ikaanza kuinama. Baada ya muda sio mrefu, “ilianza kuinama kwa upande na maji yakaanza kuingia kwa kupitia madirisha madogo ya mizinga hadi ikazama polepole chini ya tanga, bendera ya kuashiria meli na kila kitu.”¹ Safari ya kwanza ya *Vasa* ilikuwa takriban futi 4,200 (1,280 m).

Matamano ya Gustav Adolf ya kuwa na ishara ya hadhi ya ubadhirifu iliharibu ruwaza ya kile ambacho kingekuwa chombo kizuri sana cha baharini, meli yenye uwezo mkubwa sana ya kivita kwa wakati wake. Kusita kusema kwa

waunzi—hofu yao juu ya hasira ya mfalme—kulimnyima mfalme maarifa na umaizi wao. Wale wote waliohusika walisahau malengo ya shughuli ile: kulinda Uswidi na kukuza maslahi yake kule ng'ambo. Meli ambayo inajaribu kwenda kinyume na sheria za fizikia ni jahazi tu ambalo haliwezi kuelea.

Tunahitaji msimamo imara wa kiroho wa kutosha ili tuweze kukabiliana na dhoruba na mikondo kutoka pande zote, ili tuweze kuishi maisha yetu ya sasa kwa ufanisi, kufanya marekebisho yanavyotakikana, na kuweza kurudi salama nyumbani kwetu mbinguni. Kuna mambo ambayo tunaweza kufanya ili tuzidi kuwa imara kiroho. Nitagusia manne.

Kutii Amri za Mungu

La kwanza ni kutii amri za mungu. Jinsi tu *Vasa* ilita-walwa na sheria za fizikia, sote tunatawaliwa na sheria za kiroho. Hakuna aliyesamehewa kutoka kwazo. Tunahitaji kutii sheria hizi za kiroho, ambazo twaziita amri za Mungu.

Kufanya kazi na sheria za fizikia katika ujenzi wa meli ile kunaweza kuwa kulionekana kuwa na vizuizi kwake Gustav Adolf, lakini *Vasa* haingezama kabla ya misheni yake kama ingefuata sheria hizo. Badala yake, ingekuwa na uhuru na urahisi wa kutimiza kile ambacho ilipaswa kufanya.

Kwa hivyo, pia, utiifu kwa sheria za Mungu unahifadhi uhuru wetu, urahisi, na uwezo wa kutimiza uwezo wetu. Amri hazijadhamiriwa kutuzuia. Badala, utiifu unaongoza hadi ongezeko la imarisho la kiroho na furaha ya kudumu.

Utiifu ni chaguo letu. Yesu alielekeza, “Tazama, nimewapatia amri; kwa hivyo tiini amri zangu” (3 Nephi 15:10). Ni rahisi hivyo. Fanya uamuzi. Amua kuwa mtiifu kikamilifu. Hakuna kinachoweza kuzidisha kuwa imara kiroho zaidi. Hakuna kinachoweza kutupa uhuru mkubwa kutimiza lengo la maisha.

Kufuata Ushauri na Kuwa Wanafunzi Maisha Yetu Yote

Pili, tunahitaji kuzingatia na kufuata ushauri kutoka vyanzo aminifu na kujitolea kuwa wanafunzi maisha yetu yote.

Mojawapo ya shida za kupata maarifa ni kiburi ambacho kinaweza kuja tunapofikiri tunajua sana kiasi cha kuwa hakuna tunachoweza kujifunza tena. Sote tumeyana haya kwa wale watu ambao wanaamini sana werevu wao. Ni vigumu sana kumfundisha mjua yote.

Akizingatia haya, na akiwa mwenye kutaka kuwa mwanafunzi maisha yake yote, Rais Henry B. Eyring, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, alisema, “mimi bado ningali mtoto na kuna mengi ya kujifunza. Watu wengi wanaweza kunifundisha kitu.”² Wakati aliponipa mwito wa kuwa Kiongozi Mkuu Mwenye Mamlaka, Rais Eyring alinifundisha somo muhimu sana. Alisema kuwa anaposikia mtu akisimulia hadithi ambayo ameisia mbeleni au akitumia maandiko ambayo anayafahamu vizuri sana, anajiuliza, “Ni kwa nini Bwana ananisisitizia haya?” na “Ni kipi naweza nikajifunza tena kutoka kwa simulizi hiyo au maandiko hayo?” Ikiwa tunataka kuzidi kuwa imara kiroho, tutakuwa tayari kujifunza na tutakuwa wanyenyekevu kiasi cha kutosha kukubali kiongozwa bila ya kujali umri na tajriba yetu.

Utiifu ni chaguo letu kweli. Tunaweza kusikiliza na kufuata ushauri tunaopewa na viongozi wa Kanisa, hasa wale tunaoidhinisha kama manabii, waonaji, na wafunzi; kutoka kwa wazazi; na kutoka kwa marafiki waaminifu—au la. Tunaweza kutaka kuwa wanafunzi maisha yetu yote—au la. Tunaweza kuzidisha kuwa kwetu imara—au la. Tukikosa kuzidisha kuwa imara kiroho, tutakuja kuwa kama *Vasa*—jahazi ambalo haliwezi kuelea.





✦ *Kuhudumia Wengine*

Tatu, kuelekea kutoka ndani kwenda nje, kuwajali wengine, na kuwahudumia wengine kunazidisha kuwa kwetu imara kiroho.

Milele inazidi kuonekana waziwazi wakati tunapowalenga wengine na kutafuta kuwasaidia watoto wa Baba wa Mbinguni. Nimepata kuwa ni rahisi kwangu kupokea msukumo wakati ninapoomba ili nijue jinsi ninaweza kumsaidia mwingine kuliko wakati ninapojiombea tu binafsi.

Tunaweza kuamini kuwa mahali fulani kwa siku zijazo tunaweza kuwa katika hali njema ya kusaidia. Hakika, wakati ni sasa. Tumekosea ikiwa tunadhani kuwa itakuwa rahisi wakati tutakuwa na muda zaidi, pesa zaidi, au chochote zaidi cha kuwahudumia wengine. Bila ya kujali hali, tuna chaguo. Tutawasaidia wengine au la? Tunaanguka mtihani muhimu sana wa maisha ya sasa ikiwa hatutachagua kuwasaidia walio na shida. Na, ikiwa tutatoa msaada, tunazidi kuwa imara kiroho.

✦ *Tumfanye Yesu Kristo Msingi Wetu*

Nne, hatimaye, na la muhimu zaidi, kuwa kwetu imara kiroho kunazidi kwa uwiano na kiasi ambacho tunamfanya Yesu Kristo kama msingi wetu.

Bila Kristo, tunaelekezwa kama chombo kinachoyumba yumba kwenye mawimbi. Hatuna nguvu kwa sababu hatuna tanga. Hatuna uthabiti, hasa nyakati za dhoruba, kwa sababu hatuna nanga. Hatuna mwelekeo au malengo kwa sababu hatuna chochote ambacho twaweza kutumia kuelekeza. Ni lazima tumfanye Kristo msingi wetu.

Ili tuweze kukabiliana, kushinda, na tuwe tayari kwa upepo mkali wa pembeni na mikondo ya maisha inayogongana, tunastahili kutii amri za Mungu; tuwe wanyenyekevu, radhi, na wasomi jasiri maisha yetu yote; kuwahudumia wengine; na kumfanya Yesu Kristo kama msingi wa maisha yetu. Tufanyapo haya, tunazidi kuwa imara kiroho. Tofauti na *Vasa*, tuna uwezo wa kurudi katika bandari salama, tukiwa tumetimiza hatima yetu. ■

Kutoka Ibada katika Chuo Kikuu cha Brigham Young, Sept. 16, 2014. Kwa nakala nzima katika Kiingereza, tembelea speeches.byu.edu.

MUHTASARI

1. Barua kutoka Halmashauri ya Uswidi ya Ufalme wa Mfalme Gustav II Adolf; tafsiri imenukuliwa katika Richard O. Mason, "*Vasa Yazama*," virtualschool.edu/mon/CaseStudies/Vasa/vasa.html. Historia nyingi za *Vasa* zipo; ona, kwa mfano, vasamuseet.se/en kwa historia na tovuti nyingine.
2. Henry B. Eyring, katika Robert I. Eaton na Henry J. Eyring, *Nitawangoza: Maisha ya Henry B. Eyring* (2013), 409.

JIFUNZE KUCHEZA WIMBO WA KIDINI *katika Dakika 10!*

Imekusanywa na Kutoholewa na Daniel Carter

Idara ya Kanisa ya Muziki na Sanaa ya Utamaduni


Kama haujawahi kucheza kinanda hapo awali lakini daima umekuwa hamu ya kujifunza, hii ndiyo nafasi yako. Kile unachohitaji tu ni kinanda cha muziki. Hata kama hauna nyumbani, unaweza kuchukua makala hii na kwenda nayo hadi mahali ambapo kuna piano au kinanda ili uanze kujifunza.

Somo hili ni rahisi sana na jepesi kiasi kwamba utaweza kucheza wimbo wa injili mwishoni. Kwa kweli, inawezekana wewe kucheza melodi ya wimbo wa injili katika somo hili kwa takriban ndani ya dakika 10!

Tayari? Acha tuanze!

Kujitayarisha Kucheza Kinanda

1. Unapoketi karibu na kinanda na kuweka vidole vyako kwenye kiibodi, sogeza benchi nyuma kiasi kwamba viwiko vyako viwe vimejikunja kidogo tu.
2. Keti katikati ya benchi, lililo katikati ya kiibodi.
3. Keti upande wa mbele kabisa wa benchi hilo na mgongo wako ukiwa wima.
4. Pumzisha miguu yako sakafuni.
5. Keti starehe, ukidumisha mkao mzuri.
6. Hakikisha kuna mwangaza mzuri ili uweze kuona kitabu cha muziki na kiibodi.





7. Simama. Teremsha mikono yako pembeni mwako na uipumzishe. Angalia mkunjo wa asili wa mikono yako, kana kwamba imeshikilia mpira. Unapoketi tena, weka vidole vyako kwenye kiibodi ukidumisha mkunjo wake wa kawaida.

8. Weka mikono yako juu ya kiibodi, ukiacha vidole vyako viguse karibu kati kati ya mahali

pale pakubwa palipo na vibonyezo vyeupe. Shikilia viganja vyako juu ya kiibodi, lakini usiviweke juu ya vibonyezo au mbao iliyoko chini ya vibonyezo.

9. Bonyeza kibonyezo kwa pedi ya kidole chako chini tu ya ncha ya kidole. Kunja kila kidole chako, ukikiinua kutoka kifundo nyuma ya mkono wako. Unapobonyeza kibonyezo, dumisha viungo vyako vya kidole vikiwa vimekunjwa.




Kucheza kwa Kutumia Nambari za Vidole

Ili kukusaidia kuweka kidole sahihi juu ya kila kibonyezo, vidole vimepewa nambari kama ilivyoonyeshwa hapa. Nambari

za vidole zimeandikwa karibu na noti kwenye ukurasa.

Weka mkono wako juu ya na kundi lo lote la vibonyezo vitano, ukishikilia kila kidole juu ya kibonyezo kimoja. Fanya mazoezi ya nambari

za vidole kwa kucheza vibonyezo kwa kidole sahihi kama ilivyoonyeshwa. Noti zilizo na mashina yanayoenda juu ni za mkono wa kulia. Noti zilizo na mashina yanayoenda chini ni za mkono wakushoto.



Kucheza “Kuna Mlima wa Kijani Mbali”

Weka mikono yako kwenye kinanda ilivyoonyeshwa chini.

Tumia makundi mawili na matatu ya vibonyezo vyeusi ili kukusaidia kupata mahali sahihi.

Cheza wimbo huu wa injili, ukifuata nambari za vidole kama ilivyoonyeshwa. Noti zilizo na mashina yanayoenda juu ni za mkono wa kulia, na noti zenye shina manayoenda chini ni za mkono wa kushoto. Fanya mazoezi ya wimbo huu wa injili hadi uzoee. Tumia kanuni rahisi za mbinu za kubonyeza zilizoorodheshwa katika orodha ya hoja tisa.


Sasa umetambulishwa katika kucheza kinanda na umejifunza melodi rahisi ya wimbo wa injili. Kucheza nyimbo nyingine za injili, unahitaji kujifunza kanuni kadhaa za msingi kuhusu vipimo vya muziki, sauti, na noti.

Hii ndiyo sehemu bora zaidi: somo ambalo umejifunza tu hivi sasa ni somo la kwanza katika Kozi ya Kiibodi ya Kanisa, inayopatikana katika lugha sita kutoka idara ya Kanisa ya Usambazaji.¹ Mpango huu wa maelekezo yaliyo rahisi kufuata unakusaidia kujifunza peke yako au kwenye vikundi. Unaweza hata kushirikisha familia yako nzima katika kujifunza

kucheza kinanda kama shughuli ya mkutano wa jioni ya familia nyumbani. Kozi hii inaweza kukamilishwa katika muda wa wiki sita tu.

Tafti mbalimbali zinaonyesha kuwa masomo ya muziki kibinafsi husaidia kuimarisha malengo ya wanafunzi, kuboresha msimamo wa kitaaluma na ujuzi wa kufikiri mambo yenye kujenga hoja.²

Kwa kujifunza ujuzi wa kucheza muziki, tunakuza vipaji ambavyo Mungu ametupa, tunaongeza maarifa yetu, na kujifunza njia tofauti ambazo tunaweza kutumia maarifa na vipaji hivyo kujenga Ufalme wake. ■



MUHTASARI

1. Kuagiza Seti ya kujifunza kucheza kinanda nenda kwa store.lds.org
2. Tazama Laura Lewis Brown, “Manufaa ya Masomo ya Muziki,” pbs.org; Jessica Velasco, “Jinsi Sanaa Inavyoweza Kuwasaidia Wanafunzi Kufanya Vizuri,” the Science of Learning Blog, Dec. 11, 2012, scilearn.com/blog/how-arts-help-students-excel; “Muziki Unawasaidia Watoto Kujifunza Hesabu,” *The Telegraph*, Mar. 22, 2012, telegraph.co.uk.

KUJIPA SHARTI LA **Kuacha**

Ujuzi wangu wa kucheza kinanda haukuwa ukiongezeka, hata baada ya mazoezi ya miaka mingi. Wazazi wangu walisema ningeweza kuacha kwa sharti moja tu: Nilihitaaji kujifunza nyimbo 50 za injili.

Na Gretchen Blackburn

Niliingia nyumbani kwa fujo, macho yangu yakifurika machozi baada ya kushindwa somo lingine la kinanda. Ulikuwa ni mwaka wangu wa nne nikijifunza kucheza kinanda, na kwa shida sana nilikuwa nimeboresha kupiga kupita “Meremeta, Nyota Ndogo.” Mwalimu wangu alikuwa amejaribu kutafuta jambo zuri la kusema kuhusu kucheza kwangu kunakotisha, lakini nilijisikia tu vibaya zaidi. Wazazi wangu walikuwa wakilipia masomo yangu ya kinanda ambayo sikutaka na nilikuwa nimekwishapoteza matumaini.

Nilitaka wazazi wangu waniruhusu niache. “Tafadhali,” niliwasihi. Nitafanya chochote. Nifanye nini?

Baada ya kufanya majadiliano baina yao, walisema, “Kama ukijifunza nyimbo 50, tutakukubalia uache.”

Nilianza kufanya mazoezi mara moja. Nilitaka vibaya sana kuacha

kiasi kwamba nilikuwa tayari kutumia muda wa ziada kwenye kinanda. Wimbo wa kwanza, “Asante Ee Mungu kwa Nabii” (*Kitabu cha Nyimbo*, na. 19), ulinichukua karibu mwezi mmoja kuwa stadi. Bado nilikuwa na dhamira ya kuacha, kwa hiyo niliendelea kufanya mazoezi.

Kitu cha kupendeza kilifanyika: ilianza kuwa rahisi kuwa stadi katika nyimbo za injili. Nilijisikia mwenye furaha zaidi wiki mzima. Nilijipata nikivuma nyimbo za injili wakati wa mchana na nikiimba kwa sauti ya juu wakati wa mkutano wa sakramenti.

Hatimaye, niliacha kuhesabu ni nyimbo ngapi nilikuwa nimezajua. Kadiri nilivyokuwa nikiongeza ujuzi kwenye kinanda, niligundua kuwa nilikuwa na uwezo wa kujifunza wimbo mpya kikamilifu katika karibu muda wa chini ya dakika 30.

Wakati mwishowe nilipoziumlisha, nilikuwa nimejifunza zaidi ya nyimbo 50. Na hapakuwa na jinsi ambavyo ningeacha kucheza kinanda. Nilikuwa nimekuwa hodari katika uwezo wangu wa kucheza na nilikuwa nimeona nguvu za nyimbo za injili maishani mwangu.

Nyimbo za injili ni kama maandiko; zinaongea ukweli. Ninapocheza nyimbo za injili, ninajisikia kama kwamba ninajizamisha mwenyewe ndani ya maandiko. Kujifunza kucheza nyimbo za injili imekuwa kama kichocho cha kujenga ushuhuda wangu na kujifunza ukweli. Ninajiona mwenyewe nikipitia maneno ya nyimbo tofauti tofauti ili kunisaidia siku mzima. Kucheza kinanda kumeimarisha ushuhuda wangu na kumenifungulia milango popote niendapo. ■

Mwandishi anaishi New York, Marekani.



MSHTUKO, HUZUNI, NA MPANGO WA MUNGU

*Kupitia tukio lililonibananga zaidi maishani mwangu, nilihisi kuwa **Baba wa Mbinguni alikuwa nami** wakati huo wote.*

Na Paola Çajupi

likuwa asubuhi moja mapema 2008 wakati mama yangu aliponiambia ili niende shuleni. Nilikuwa na furaha asubuhi hiyo, lakini sikujua kuwa ingegeuka kuwa siku mbaya zaidi maishani mwangu au siku ya mwisho ambayo ningekuwa pamoja naye. Sikumaliza masomo yangu siku hiyo kwani rafiki wa familia yetu alikuja kuni-chukua na kuniambia kuwa mama yangu alikuwa amejua. Nilikuwa na miaka 12 tu.

Nilifikiria, “Ni namna gani naweza kuishi bila mama?” Alikuwa rafiki yangu wa dhiti.

Nililia kwa miezi kadha. Sikufurahia kwenda shuleni kwa sababu wale watoto wengine walinitendea tofauti na wengine na kunionea huruma. Sikuwa na fununu nilichohitajika kufanya; nilijua ilinibidi nijipe moyo tu kwa ajili ya kila mtu.

Siku moja, miezi mitano au sita baada ya kifo cha mamangu, nilikuwa peke yangu ndani ya chumba changu karibu na dirisha, nikilia, nikijaribu kuelewa sababu ya kuwa hapa. Ghafla nilisikia sauti akilini: “Wewe ni binti yangu, sitakuacha uteseke.” Nilijua alikuwa Mungu. Lakini ilinishangaza kwa sababu sikuwa nikimwamini tena, hasa kwa sababu niliamini ilikuwa Mungu aliyemchukua mama yangu kutoka kwangu. Hata kama sikujua kile Yeye alichomaanisha, nilijihisi salama.

Miaka mitatu baadaye nilienda Roma, Italia, kumtembelea mjomba wangu. Alishinda akinielezea kuhusu kanisa analoshiriki. Jumapili moja, tuliambatana naye.

Nitakumbuka daima nikitembea kuelekea kwenye milango ya kanisa mara ya kwanza na hisia ya upendo wa Baba wa Mbinguni wakati nilipoingia ndani. Ilihisi kama nyumbani.

Nilianza kwenda Kanisani kila Jumapili na kila shughuli wakati wa wiki. Nilifurahia kuwa na vijana wa Kanisa. Walinifanya kuwa na furaha sana. Walifikiria na kuamini katika mambo sawa sawa na yale yale kama mimi. Baada ya miezi mitatu, likizo yangu ya majira ya kiangazi ilikwisha na ilibidi nirudi Albania.

Niliporudi nyumbani, nilimweleza baba yangu kuhusu hisia nilizokuwa nazo na ile furaha niliyohisi wakati huo. Hakufurahia hayo. Aliniambia kuwa hangekubali niendelee kwenda kanisani wala kujifunza zaidi kuhusu kanisa hilo. Kwa hivyo ingenibidi niwe na subira kwa muda wa miaka mitatu iliyokuwa mbeleni hadi wakati ningehitimu miaka 18. Kisha ningeweza kujiamulia na kubatizwa.

Wakati huu nilibarikiwa na watu wengi ambao wali-nielezea kuhusu walichojifunza kila Jumapili Kanisani. Mmojawapo wa watu wale ilikuwa Stephanie. Alikuwa akiishi Italia wakati mjomba wangu alipojiunga na Kanisa, lakini alikuwa amerudi nyumbani kwao Marekani. Mjomba wangu alifikiri ingekuwa vizuri kwetu kuwasiliana na kila mmoja wetu, kwa hivyo nilimwongeza kama rafiki katika mtandao wa Facebook.


Hata kama hutukuwa tumewahi kukutana katika nafsi

zetu, nitakuwa na shukrani daima kwa kunisaidia kujenga imani yangu na kujifunza zaidi kuhusu injili ya Yesu Kristo. Aliniandikia karibu kila Jumapili na kunieleza kila kitu alichojifunza kanisani na kisha angejibu maswali yangu. Alikuwa rafiki mzuri kwangu.

Hatimaye, baada ya miaka ya kuwa na subira, nilibatizwa siku mbili tu baada ya siku yangu ya 18 ya kuzaliwa. Na karibuni nitamsimulia mamangu ile furaha niliyohisi siku ile, kwa sababu nitabatizwa kwa niaba yake. Ninajua atakuwa mwenye fahari kwa ajili ya maisha niliyochagua.


Ninahisi nimebarikiwa na Baba wa Mbinguni kwa sababu alikuwa pamoja nami safari hiyo yote kwa njia yingi sana. Nilihitaji tu kuwa na subira kwa sababu alikuwa na mpango kwangu. Ni Yeye aliyenipa nguvu za kupitia shida zote nilizokabiliana nazo. Alikuwepo kila mara, akinisaidia kuwa na furaha zaidi. ■

Mwandishi anaishi Albania.





Na Mzee
José A. Teixeira
Wa Sabini



KIELELEO NA DAVID MALAN

HATA KAMA UNAONA HAYA

Mwamini Bwana, Naye atakubariki katika juhudi zako za kueneza injili.

Nilipokuwa rais mpya wa misheni kule Brazili, nilikuwa nikiwasaili wazee fulani. Nilimuuliza mmoja aniambie kuhusu yeye mwenyewe.

“Mimi ni mwenye haya sana,” alisema. Alikuwa na wasiwasi kuwa kuona haya kwake kulikuwa kunaathiri uwezo wake wa kuhudumu.

Nilimuuliza, “Unafikiri Bwana anaweza kukusaidia kuwa mmisionari mzuri kwa njia yoyote?”

“Ninaamini Bwana anaweza kufanya chochote.”

“Basi mwache akusaidie. Unafikiri unaweza kufanya hivyo?”

“Ninaweza,” alisema.

Inabidi nikiri kuwa alipokuwa akiondoka, nilifikiri, “Barabara, natumai atafanikiwa.”

Wiki zilipita na punde wamisionari wale wale wakaja kwenye usaili tena. Wakati huu mwenzake yule mzee mwenye kuona haya alisema, “Rais, sijui ulichomwambia lakini hakika kilileta tofauti. Amekuwa mweledi katika kuzungumza na watu.” Na hivyo nilikuwa na shauku ya kuonana naye tena.

Alipoingia ofisini mwangu, alitazama chini miguuni mwake.

“Nina habari njema,” alisema. “Mimi bado ni mwenye haya, lakini nilimwomba Bwana anisaidie. Kisha nikafungua kinywa changu na nikaanza kuzungumza. Na unajua nini? Mimi hufanya hivyo kila wakati sasa. Hata huwa sikumbuki ninayosema. Cha ajabu ni kuwa watu wanafurahia. Wanahisi Roho. Wanajihusisha nami na yale ninayowaeleza.”

Nilishangaa sana kuona jinsi ambavyo mmisionari huyu alivyobadilika alipoweka imani yake katika Bwana. Alikuwa kuwa chombo kikuu katika kuleta furaha kwa watu wengi.

“Mimi bado ni mwenye haya, lakini nilimwomba Bwana anisaidie.”

Kushinda Hofu

Tunaposhiriki injili, mara nyingine sisi huwa na wasiwasi. Lakini kama mmisionari huyu mwenye haya alivyodhihirisha, Bwana atatuongoza tukimwamini. Roho Mtakatifu atatusaidia kujua la kusema (ona 2 Nefi 32:2–3), na wakati watu wanapohisi Roho, mara nyingi wao hujibu kwa njia chanya. Wengi huvutiwa sana na kile tunachoamini na hutaka kujua zaidi.

Furaha Kubwa

Nina ushuhuda kuwa Baba wa Mbinguni atatuongoza katika juhudi zetu za kushiriki injili, na katika njia hiyo tutasikia furaha kubwa. Kwa kweli, furaha hiyo itakuwa nasi sio tu kwa sasa bali katika ulimwengu ujao. (Ona M&M 18:16.) Hiyo ni sababu mzuri ya kutoka nje ya eneo lako la faraja na kufanya jambo, hata ikiwa wewe ni mwenye haya. ■

HOFU TATU AMBAZO UNaweza KUZISHINDA

Licha ya kuona haya, ninajua kuhusu hofu zingine tatu ambazo husababisha baadhi yetu kusema, “Ninaogopa kuwa ikiwa nitazungumza kuhusu injili, nitapoteza marafiki zangu.” Shukuru kuwa, kwa imani, hofu hizo zinaweza kushindwa.

1. SIJUI VYA KUTOSHA.

Ikiwa hauna maarifa kuhusu injili, wamisionari wanaweza kukusaidia. Wanaweza kutufundisha ujumbe wa Urejesho, kutusaidia kuimarisha imani yetu katika Yesu Kristo, na kutusaidia kuelewa toba na jinsi tunavyoweza kuitekeleza maishani mwetu na kwa nini kubatizwa na kipawa cha Roho Mtakatifu ni muhimu. Nyenzo ingine kubwa ya maarifa ni *Hubiri Injili Yangu*. Ningemsihi kila mvulana na kila msichana kuwa na nakala na kuifanya sehemu ya kujifunza ya kila siku pamoja na maandiko yako.

2. KAMWE SIJAWAHI KUFANYA HIVI KABLA.

Ukiwa hauna uzoefu, fanya mazoezi na wamisionari! Wanaweza kukusaidia kujua la kusema au usilopaswa kusema katika hali fulani. Unapokuwa na wamisionari, utauona upendo wali-ona kwa injili na kwa binadamu wenzao. Wamepata ujasiri wa kushiriki injili; wanaweza kukusaidia kufanya vivyo hivyo.

3. NINAOGOPA KUSHIRIKI.

Tunaposhiriki ushuhuda wetu, tunawasaidia marafiki zetu kuona mambo ya maana zaidi, na wanaanza kutuheshimu na kutupenda katika mtazamo mpya. Hili hufanyika karibu kila mara. Vijana wengi husema, “Nilikuwa na hofu, lakini nilipozungumza kwa uaminifu, rafiki yangu alianza kuniamini na kuuliza maswali zaidi.” Hatupaswi kuwa na hofu ya kushiriki kile tulichonacho. Ni cha thamani kubwa kwa sababu kinatoka kwake Mungu. Na ni njia gani bora twaweza kuonyesha upendo kwa marafiki zetu kama sio kushiriki nao kile ambacho tunajua kuwa kweli?

NAFASI YETU

MWAMINIFU KATIKA KILA KITU

Alivsi H., Jalisco, Mexico

Mwanzoni mwa kila muhula shuleni, sisi hupata seti za bure za bidhaa vikiwamo daftari, ajenda, na sampuli moja ya bidhaa ngeni bila mpango maalumu. Mwaka mmoja nilikuwa kwenye foleni kupokea seti yangu na nikagundua kuwa sampuli niliyopata ilikuwa hasa ya manufaa kwangu.

Mwishowe niliona kuwa walikuwa wakitoa sampuli mbili za bidhaa aina moja. Ingekuwa rahisi kurudi tena foleni na kupokea seti ya pili na niliamua kufanya hivyo. Licha ya yote, ilikuwa ya bure, na mimi nilihitaji bidhaa hiyo.

Nilipitia msalani kwa haraka, ambako niliona simu ya mkononi

ambayo msichana fulani alikuwa amesahau kwa bahati mbaya. Ilikuwa moja-wapo ya aina ya kisasa, na nilikuwa nimeipoteza simu yangu wiki moja kabla siku hiyo. Lakini hata sikuwazia kuichukua. “Huo ni wizi,” Nilijiambia.

Kisha, njiani kwenda kupokea seti yangu ya pili ya bidhaa za bure, niligundua kuwa hiyo ingekuwa udanga-nyifu kama kuchukua ile simu kwa sababu ningedanganya na kusema kuwa sikuwa nimepewa mbeleni.

Nilikuwa na shukrani kwa tukio hili dogo ambalo lilinifundisha somo

kubwa. Niliirudisha simu na kwenda nyumbani na daftari moja pekee, ajenda moja, na sampuli moja ya bidhaa, lakini nilijisikia vizuri kwa kuwa mwaminifu na mkweli katika mambo yote, bila kujali ni kidogo kiasi gani. ■



NIMEBARIKIWA KWA KUTII SHERIA YA ZAKA

Sabrina T., São Paulo, Brazil

Nilipokuwa mdogo, familia yangu ilipitia katika changamoto nyingi za kifedha ambazo zilidumu hadi nilipokuwa na umri wa miaka 10. Baba yangu hakuweza kupata kazi nyingine, kwa hivyo alifanya kazi kama mchuuzi wa mitaani na alipata pesa kidogo sana. Mama yangu alikaa nyumbani kunitunza mimi pamoja na kakangu mdogo.

Lakini hata tukipitia katika taabu hizo nyingi, tulikuwa na ushuhuda wa kulipa zaka na kutoa matoleo mengine. Tulilipa zaka yetu kila mwezi na hatukukosa chochote. Tunajua kwa uhakika kwamba tunazidi kubarikiwa kwa sababu ya wema Wake Bwana usio na mwisho na kwa

sababu Yeye hutimiza ahadi Zake tunapokuwa waaminifu kwa amri Zake.

Siku zetu za majaribu ya kifedha hatimaye ziliisha. Baraka ambazo Bwana ametupa katika miaka hii michache iliyopita zimekuwa za ajabu.

Ninajua kwa wale ambao hulipa zaka kwa uaminifu pamoja na kulipa matoleo yao kwa upendo na lengo la kubariki maisha ya wengine, hakuna watakachokosa na jambo bora zaidi laweza kuwatokea, kama ilivyotufanyikia kwangu mimi na familia yangu. Baraka zitazidi. Ninajua hili. Niliishi hivi. ■

LAONEKANA ZURI?

Tazama tena. Shetani anataka tubadilishe furaha ya kweli kwa furaha isiyo ya kweli ambayo kamwe hairidhishi. Usijaribu hata mara moja.

(Ona Dieter F. Uchtdorf, "Unaweza Kufanya Hivyo Sasa Hivi," *Liahona*, Nov. 2013, 56.)



“Ninakejeliwa shuleni kwa kuwa MSM. Ninajua ninapaswa kutetea ninachoamini, lakini ni vigumu sana! Ni namna gani naweza kuwa mjasiri vya kutosha?”

Uko sawa kuwa unahitaji ushujaa ili kukabiliana na hali hii. Hata hivyo, Yesu Kristo ameamuru kuwa, “Inukeni na mng’are, ili nuru yenu ipate kuwa bendera kwa ajili ya mataifa” (M&M 115:5). Lakini kuwa na ujasiri wa kuacha nuru yako ing’are yaweza kuwa na au isiwe na maana kuwa utetee msimamo wako kwa wale wanaokukejeli.

Katika hali yoyote ile, waweza kukubali upinzani kukupa msukumo ili uwe bora. Unapofanya jitihadi kuimarisha ushuhuda wako, unaweza kukuza aina ya ujasiri mtulivu utakaokusaidia kuzungumza au kuendelea tu kufanya kile kilicho haki, hata ikiwa wengine watakukejeli.

Kuchokozwa kunaweza fadhaisha, lakini kumbuka kuwa unaweza kuomba ili ujawe na hisani ili wengine waweze kuhisi upendo wa Kristo kupitia kwako (ona Moroni 7:48). Kwa sababu kila hali ni ya kipekee, tafuta uongozi wa Roho kujua jinsi ya kujibu kama Kristo katika kila hali.

Kutegemea na hali, yaweza kuwa vyema kuzungumza na wale ambao wamekufanyia mzaha kwa faragha au hata kupuu-zilia mbali dhahiki huku ukiendelea kuishi kulingana msimamo wako. Ikiwa wengine hawana moyo wa kutaka kusikiliza uliyonayo ya kusema, mfano wako wa ukarimu, kusamehe, na uaminifu wako unaweza kuwa ujumbe bora unaoweza kuwapa.

Onyesha Ujasiri wa Kweli

Wale ambao hukufanyia mzaha wanaweza kosa kusita kufanya hivyo hata ukiwa mjasiri kiasi cha kuwauliza wakome, lakini wanaweza koma unapofanya jitihadi kwa kuishi kile ulicho—Mtakatifu wa Siku za Mwisho. Punde, nuru ya idhini ya Baba yetu wa Mbinguni itang’aa juu yako, kwa matumaini ikifungua macho yao kwa injili ya urejesho maishani mwako.

Bright U., umri 17, Imo State, Nigeria

Pata Nguvu katika Mambo ya Msingi

Maombi na kufunga ni muhimu kwa sababu itakusaidia kukabiliana na mzaha na changamoto shuleni, kama vile Yesu Kristo alikumbwa na dhahiki nyingi alipokuwa hapa duniani. Itakusaidia kuwa na upendo zaidi na subira kwa watu.

Walter C., umri 15, Jaén, Peru



Ongozwa kupitia kwa Maombi

Kwa muda mrefu nilikuwa muumini wa pekee katika shule yangu. Marafiki zangu

wa karibu walionekana kunielewa, lakini marafiki wengine shuleni walinifanyia mzaha. Siku moja nilisali na nikahisi kwamba nilihitaji kuzungumza na mmoja wao ambaye alikuwa akiwashawishi wenzake kunifanyia mzaha. Nilimweleza kwamba sikuwa nimekasirishwa naye, lakini nilimtaka anipe heshima sawa na jinsi ambavyo angetaka kuheshimiwa. Baada ya kusikia mazungumzo yetu, mmoja

wa walimu wetu alinitetea kila mara alipoona chochote kikifanyika. Ninajua kwamba Bwana atakuwa nawe unapozungumza na hawa watu.

Shanela S., umri 14, Pangasinan, Philippines

Jenga Ushuhuda Wako

Kwanza, pata ushuhuda wa kweli kuhusu ukweli unaotaka kushiriki na wengine. Kisha uwe na upendo kwa wale watu wanaokufanyia mzaha na usijiingize kwenye mabishano, kwa sababu ukinzani hauungwi mkono na Mungu (ona 3 Nefi 11:29). Cha muhimu kabisa, jitahidi kuwa Roho awe pamoja nawe daima. Roho atakusaidia kuwa na upendo zaidi na ujasiri zaidi, na atafanya maneno yako yawe na nguvu.

Julia F., umri 19, Hesse, Germany



Wapende Maadui Zako

Nimekuwa katika hali sawa kama hizo. Ukiwa na imani na ujinyenyekeze, utabarikiwa na nguvu na imani unayohitaji “kuwape nda maadui zako, kuwabariki wale wanaokulaani, . . . na kuwaombea” (Mathayo 5:44). Ningekuhimiza upekie maandiko ili upate mjibu kuhusu jinsi unavyoweza kuwa imara. Omba wakati unapohisi upweke katika imani yako. Warumi 8:31 inasema, “Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?” Uko na Mungu kukutetea! Chochote chawezekana.

Matthew T., umri 15, Utah, Marekani



Msiwe na Hofu

Zungumzeni kuhusu dini yenu kila mara au fanyeni mambo maku-sudi ili hilo lifanyike. Nilikuwa katika hali

sawa na nikaandika, “Ninafurahi kuwa MSM” kwenye mkoba wangu. Kwa kufanya hivyo, nilifungua mlango kwa nafasi kadhaa za umisionari na kuwaonyesha watu kuwa sikuwa na hofu kuwajulisha mimi ni MSM. Chochote utakachofanya, usikubali wakuvunje moyo. Waombe na ujiombe. Punde utagundua kwamba ikiwa lengo lako litakuwa kuokoa nafsi za wengine, hautakuwa na hofu sana kuwaambia ukweli kuhusu injili ya Baba yetu.

Savanna P., umri 14, Texas, Marekani



UJASIRI WA MSIMAMO WETU

“Kila mara ni vigumu kuwa tofauti na kusimama pekee yetu kulinda kile tunachoamini katika umati. Ni kawaida kuogopa kile wengine wanaweza kufikiria au kusema. Maneno ya kufariji ya Zaburi: ‘Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu nimhofu nani?’ [Zaburi 27:1]. Tunapomfanya Kristo lengo la maisha yetu, woga wetu utabadilishwa na ujasiri wa msimamo wetu.”

Rais Thomas S. Monson, “Kuwa Mfano na Nuru,” Liahona, Nov. 2015, 88.

SWALI LINALOKUJA

“Nitajuaje Mungu anasiliza maombi yangu?”

Wasilisha majibu yako, na ukipenda, picha ya ubora wa hali ya juu kabla ya Mei 1, 2016, katika liahona.lds.org, kupitia barua pepe kwa liahona@ldschurch.org, au kupitia barua pepe (ona anwani katika ukurasa wa 3).

Taarifa ifuatayo na ruhusa lazima ijumuishwe katika barua pepe yako au barua: (1) jina kamili, (2) tarehe ya kuzaliwa, (3) kata au tawi, (4) kigingi au wilaya, (5) ruhusa yako uliyoandika, na kama u chini ya miaka 18, ruhusa iliyoandikwa na mzazi wako (barua pepe inakubalika) ili kuchapisha majibu yako na picha.

Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya urefu au ufafanuzi.



Na Mzee
David A. Bednar
Wa Akidi ya Mitume
Kumi na Wawili

Je, Mitume hufanya nini?

Mitume ni watumishi wa Bwana. Wao husafiri kwenda kuwatembelea waumini wa Kanisa kote duniani.

Mara ya kwanza niliposafiri kama Mtume, nilikutana na bwana ambaye alikuwa na wakati mgumu kutii Neno la Hekima. Nilimwambia, “Bwana alinituma hapa kukupa ujumbe rahisi sana: ‘Unaweza kufanya hivi. Ninakuahidi utapata msaada Wake unapokabiliwa na changamoto hii.’”

Kuna uwezekano wa Bwana kutuma mmoja wa Mitume Kumi na Wawili nusu ya mzunguko wa dunia ili kumsaidia tu mtu mmoja? Jibu ni *ndio*. Yeye hufanya hivyo wakati wote. ■


*Kutoka kwa Mzee na Dada Bednar wakati wa Matangazo
yao ya Uso kwa Uso Kote Ulimwenguni.*



Na Carol F. McConkie

Mshauri wa Kwanza katika Urais Mkuu wa Wasichana

Amani Moyoni Mwangu



Nilipokuwa na miaka minane, nilimwona nabii, Rais David O. McKay (1873–1970). Alikuwa kuweka wakfu jengo jipya la Kanisa huko Palmyra, New York, Marekani. Familia yangu ilienda kwenye ibada ya uwekaji wakfu huo. Watu wengine wengi walikuja pia. Sote tulisisimka kumuona nabii!

Nilikuwa mdogo sana, kwa hiyo ilikuwa vigumu kwangu kuona nikiwa nimezungukwa na watu wote hao. Lakini bado niliweza kuhisi upendo wa Rais McKay. Kwa dakika moja tu, niliona nywele zake nyeupe na uso wake mkarimu. Nilifikiria, “Hivi ndivyo nabii wa Mungu anavyoonekana.” Nilikuwa

nimesoma kuhusu manabii katika maandiko, lakini huu ulikuwa wakati wangu wa kwanza kumwona nabii au Kiongozi yeyote Mkuu Mwenye Mamlaka kwa macho yangu. Nilitambua kwamba manabii ni watu halisi. Na wanatupenda! Nitakumbuka daima upendo na amani niliyojisikia siku ile.

Nilipokuwa na miaka 11, nilipata tukio jingine ambalo lilinisaidia kusikia amani moyoni mwangu. Mkutano wa kigingi ulikuwa unakaribia, na nilipata nafasi ya kuimba katika kwaya ya kigingi. Nilikuwa na furaha sana! Nilivaa shati zuri jeupe, na kujihisi mtu muhimu. Wimbo tulioimba ulikuwa

na maneno kutoka Yohana 14:27, “Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msiwe na wasiwasi moyoni mwenu, wala msifadhaike.”

Maneno hayo kweli yalinigusa moyo, na nimeyakumbuka tangu wakati huo. Nilipoimba maneno hayo, nilijua yalikuwa ya kweli. Nilihisi Roho Mtakatifu akiniambia kwamba kumfuata Yesu Kristo kunatusaidia kuona amani. Tangu wakati huo, kila mara ninapopata changamoto, maandiko haya huja akilini mwangu na kunipa amani. Ukweli niliojifunza nilipokuwa mdogo umebariki maisha yangu yote. ■

USHUHUDA WA Ethan

Na Larry Hiller

Kutokana na tukio halisi

“Sikiliza, sikiliza. Roho Mtakatifu atanong’ona. Sikiliza, sikiliza sauti ndogo tulivu” (Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 106).

Ethan aliketi katika mkutano wa amfungo na ushuhuda na kutazama juu kwenye mimbari. Rafiki yake wa dhati, Sam, alikuwa akitoa ushuhuda. Rafiki yake Sarah alikuwa ameketi kwenye jukwaa, akisubiri nafasi yake. Sam aliongea kuhusu mradi wa huduma alioufanya. Alisema alikuwa na ushuhuda kuhusu huduma. Sarah alitoa ushuhuda kuhusu familia. Babake Ethan pia alienda kwenye jukwaa. Aliongea kuhusu kazi ya hekalu. Wote walishuhudia kuwa Kanisa ni la kweli. Ilionekana kama kwamba kila mtu isipokuwa Ethan alikuwa na ushuhuda.

“Nina ushuhuda kuhusu nini?” Ethan aliwaza.

Alifikiria kuhusu miaka michache iliyopita wakati ambapo yeye na marafiki zake walibatizwa. Mwalimu wake wa Msingi Dada Calder, alikuwa ametoa hotuba kuhusu Roho Mtakatifu.

“Roho mtakatifu anaweza kukufanya ujisikie kuwaka moyoni mwako. Anaweza kukusaidia ujue kile kilicho cha kweli,” alikuwa amesema. “Na hivyo ndivyo unavyopata ushuhuda wa kile ambacho unaamini.”

Ethan alijaribu kutenda haki ili aweze kumsikia Roho Mtakatifu. Alisoma maandiko na kusali.

Ilionekana kama kwamba kila mtu isipokuwa Ethan alikuwa na ushuhuda.





Lakini hakuwa amewahi kuwa na hisia ile ya kuwaka ambayo watu huiongelea. Je, hilo lilimaanisha hakuwa na ushuhuda?

Swali hili lilikwama akilini mwa Ethan siku nzima iliyofuata. Alikuwa bado anafikiria wakati ambapo yeye na Sam walikuwa wakicheza mchezo wa kibao cha kuteleza bada ya shule. Aliwaza jinsi ambavyo angemuuliza Sam kuhusu swali hilo.

“Halo, Sam,” Ethan hatimaye aliuliza, “je, ulikuwa na hofu wakati ulipotoa ushuhuda wako jana?”

Sam aliruka kutoka kwenye ubao mteleo na kutembea hadi kwenye nyasi. “Sio kweli,” alisema, huko akiketi chini. “Nimetoa ushuhuda wangu kwenye mkutano wa jioni ya familia kabla yake.”

Ethan alijiunga naye na kuweka ubao mteleo wake mapajani pake. “Lakini ni namna gani ulijua kuwa una ushuhuda?”

“Basi, niliomba na nikajisikia vizuri juu ya jambo hilo.”

Ethan aliitikia polepole kwa kichwa na kuzungusha gurudumu kwa mkono wake. Kwa namna fulani alitaka naye ajisikie hivyo pia.

Usiku huo, wakati ambapo nyumba ilikuwa na giza na tulivu, Ethan

alipiga magoti kando ya kitanda chake kuomba.

“Baba wa Mbinguni,” alisema, “tafadhali nisaidie nipate ushuhuda. Nisaidie nijue kuwa Kanisa ni la kweli. Kuwa Joseph Smith alikuwa Nabii. Na kwamba Kitabu cha Mormoni ni cha kweli.”

Katikati ya maombi yake, Ethan alitulia. Alifikiri kwa dakika chache. Kisha akajiuliza, “Je, ninajua chochote hadi sasa?”

Na kisha hisia ya utulivu na amani ikaja juu yake. Haikuwa hisia ya nguvu na yenye kuwaka. Lakini Ethan alijua, *huyo* alikuwa Roho Mtakatifu.

Wazo lilikuja akilini mwa Ethan. “Ninajua kwamba ninajua.” Na alipofikiria kuhusu hayo, aligundua kuwa alikuwa amewahi kuwa na hisia hii ya amani hapo awali.

Wakati wowote aliposoma Kitabu cha Mormoni, alijisikia vizuri na sahihi. Sasa alijua kuwa hisia ile ilikuwa ni Roho Mtakatifu akimshuhudia. Alipoenda kanisani na alijisikia vizuri na ni sahihi kuwa pale, huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu pia. Alikuwa tayari ameanza kupata ushuhuda.

Hakuhitaji kujua kila kitu kwa wakati huu. Lakini alijua ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa halisi na angeweza kumsaidia kuendelea kujenga ushuhuda wake.

Ethan akaanza kuomba tena. Lakini wakati huu ilikuwa ni kusema asante. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

Pesa za Baba wa Mbinguni

Na Angela Peña Dahle

“Shika Amri. Katika hili kuna usalama na amani” (Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 146).

Ana alitafuna kitafunwa Achake cha mwisho cha tortilla. Kilikuwa laini na kitamu. Ana alizipenda tortilla za bibi yake. Zilikuwa sehemu bora ya kifungua kinywa.

Ana alimtazama bibi yake, Abuela, akiosha vyombo.

Ilikuwa ni kama asubuhi nyi-ngine. Lakini kitu kimoja hakikuwa sawa.

Abuela kawaida huenda sokoni kununua chakula. Lakini sio leo. Leo hapakuwa na pesa za kununua chakula.

“Kesho tutakula nini?” Ana aliwaza.

Kisha Ana akakumbuka. Alijua mahali zilipokuwa pesa fulani! Jana usiku alimwona Abuela akiweka pesa fulani katika kitambaa kidogo cheupe.

“Abuela, ulisahau? Unazo pesa za kununua chakula.”

“Pesa zipi?” Abuela aliuliza.

Ana alikimbia kwenda kuleta pesa zile. Alichukua mfuko ule mdogo wa sarafu. *Clink! Clink!*

Abuela alitabasamu. “Hiyo ni zaka yetu, Ana. Hiyo ni pesa *Yake*.”

“Lakini tutakula nini kesho?” Ana aliuliza.

“Usijali,” Abuela alisema. “Nina imani kuwa Baba wa Mbinguni atatusaidia.”

Asubuhi iliyofuatia Abuela alimpa Ana tortilla ya mwisho. Halafu yeye akaketi chini kwenye kiti chake. Ali-shona maua mekundu kwenye vazi



na huku akihadithia kuhusu wakati alipokuwa msichana mdogo. Hakuonekana kuwa na wasiwasi.

Kisha Ana akasikia mtu akibisha hodi. Alikimbia kwenda kufungua mlango.

“Mjomba Pedro!”

“Nilijisikia kuwa lazima niwate-mbelee nyinyi wawili,” Mjomba Pedro alisema. Aliweka mifuko mitatu juu ya meza. Moja ulikuwa na unga wa mahindi wa kutengeneza tortillas. Mwingine ulikuwa na nyama. Mwingine ulikuwa na mboga za majani mabichi kutoka sokoni.

“Loo, mwanangu mpendwa,” Abuela alisema. “Nataka nikutayarishie supu yangu ya kebabu bora kabisa!”

“Supu yako ni bora ulimwengu kote,” Mjomba Pedro alisema.


Ana alicheka na kupiga makofi.

Halafu akasita. Kulikuwa na kitu kimoja alichotaka kujua. “Abuela, ulijua kuwa Mjomba Pedro angeli-kuja leo? Hiyo ndiyo maana hukuwa na wasiwasi?”

“Hapana,” Abuela alisema. “Ninapolipa zaka, nina imani kuwa Baba wa Mbinguni atanibariki. Naye amefanya hivyo!”


Ana akamkumbatia Abuela. Alijiona yu msichana mwenye furaha zaidi katika Mexico. Yeye na Abuela walikuwa na imani katika Baba wa Mbinguni. Sasa alikuwa na hamu kubwa ya kula supu tamu ya Abuela! ■

Mwandishi anaishi Carolina Kaskazini, Marekani.






Kuwafuata Manabii na Mitume

Na Jenna Koford




Mungu huwaita manabii na mitume ili watufundishe kile ambacho Mungu anataka tujue. Katika maandiko tunasoma kuhusu manabii kama Nuhu, Nefi, na Joseph Smith, na mitume kama Petro na Paulo. Tunao manabii na mitume leo!



UTONDOTI KUTOKA KWA BWANA HUTIMIZA MANENO YAKE YOTE. NA CLARK K. PRICE; UTONDOTI KUTOKA KWA JOSEPH SMITH, JR. NA DANQUART A WEGGE-LAND; UTONDOTI KUTOKA KWA HADITHI ZA AGANO JIPIYA, NA PAUL MANN; UTONDOTI KUTOKA KWA NEFI NA LEHI WAKONGOZA KUENGA MELI, NA JERRY THOMPSON; VIELELEZO NA GARTH BRUNER

“Nabii, muonaji, na mfunuzi” ni nini?



Nabii husema kwa niaba ya Mungu.

Muonaji anaweza kujua yaliyopita, ya sasa, na ya siku za usoni.


Mfunuzi anafunua (au anatuonyesha) mapenzi ya Mungu.

- Washiriki wa Urais wa Kwanza wote ni manabii, waonaji, na wafunuzi. Na hivyo kwa Mitume wote.
- Ni Rais wa Kanisa pekee aliye na mamlaka kutoka kwa Mungu kuongoza Kanisa zima.
- Ni manabii, waonaji, na wafunuzi wangapi walio hai tulio nao kwa ujumla?

12 15 3 1

11 :nqf

Kwa nini ni muhimu kumfuata nabii?



Nabii ni kama mtu ambaye anayelinda kutoka juu ya mnara (ona pia ukurasa wa 38) Anaweza kuona hatari inayokaribia na kutueleza jinsi tunavyoweza kujikinga. Anatusaidia kumfuata Yesu Kristo.

Ni nini nabii wetu ametuagiza tufanye.



Nabii wetu leo ni Rais Thomas S. Monson. Hapa kuna mambo kadhaa ametuomba tufanye.

- Tufuate mfano wa Yesu Kristo na tumpende kila mtu.
- Tulipe zaka na tuchangie hazina ya mmisionari.
- Tuepukane na sinema mbaya, Televisheni na vyombo vingine vya habari.
- Tuweke picha ya hekalu katika kila chumba cha kulala.
- Tujifunze hotuba za mkutano mkuu.
- Tuwatembelee wazee na tuwe majirani wema.

Chagua kitu kimoja kutoka katika orodha hii ambacho unaweza kufanya mwezi huu. Utafanya nini? ■

Alma Alitubu

Alma alikuwa kuhani wa Mfalme muovu Nuhu. Alimsikiliza nabii Abinadi akifundisha kuhusu amri. Alma alijua alihitaji kubadili maisha yake na kumfuata Mungu badala ya kufanya mambo maovu. Aliandika yale ambayo Abinadi alifundisha. Alianza kuwafundisha wengine injili. Baadaye alikuwa na familia na akampa mwanawe mmoja jina la Alma.



Nilikuwa mlinda lango na nilikuwa nikifanya kazi nzuri. Kisha nikakumbuka nilihitaji kutubu kwa kusema maneno mabaya jana. Nilihitaaji kufanya hivyo, lakini nilikuwa niki-shiriki katika mchezo wa kandanda. Halafu nikakumbuka jambo fulani. Unaweza kuomba mahali popote unapohitaji kufanya hivyo! Baada ya kuomba, nilijisikia vizuri kwa kutubu.


Peter G., umri 8, Utah, Marekani.



Damon B., umri 8, Utah, Marekani.



Kata, kunja, na uweke kadi hii ya changamoto!




Ninaweza tubu!


- Kariri Mosia 18:9.
- Andika au chora kitu ambacho nabii alisema kwenye mkutano mkuu.
- Chagua njia moja ambayo unaweza kujiboresha. Jaribu kufanya hivyo mwezi huu.
- Ninajipa changamoto ya . . .

Maandiko ya Mwezi Huu

Baada ya kusoma kifungu cha maandiko, chora na kalamu za rangi katika sehemu zilizo na nambari zinazolingana kwenye Maji ya Mormoni!

- 1 Mosia 21:14–16, 32–35
- 2 Mosia 22:2, 10–16
- 3 Mosia 24:8, 10–14
- 4 Mosia 27:8, 11, 18–24
- 5 Mosia 27:30–37
- 6 Mosia 28:3, 5–15, 20
- 7 Alma 8:11–16, 18–27
- 8 Alma 11:38–46






Maji ya Mormoni

Alma alijificha kutoka kwa Mfalme muovu Nuhu karibu na mahali pa amani palipoitwa Maji ya Mormoni. Watu wengi walikuja kumsikiliza Alma akifundisha injili. Walitaka kubatizwa. Alma alipowabatiza, watu walitoa ahadi sawa na hizi, au maagano, tunayofanya wakati tunapobatizwa. Unaweza kusoma zaidi juu ya ahadi hizi katika ukurasa ufuatao. ■


Alma Anabatiza Watu Wengi



Abinadi alikuwa nabii. Alifundisha watu kumwamini Yesu na kuacha kufanya matendo mabaya. Mfalme muovu aitwaye Nuhu alikasirishwa na Abinadi. Nuhu hakutaka kutubu.




Mtu mmoja aliyeitwa Alma alimwamini Abinadi. Alitoroka na kujificha mbali na mfalme mwenye hasira. Alisikitika kwa kufanya matendo mabaya, na alitubu, kama vile Abinadi alivyokuwa amefundisha.



Watu wengi walikuja kumsikiliza Alma akifundisha kuhusu Yesu Kristo. Alma alifundisha kuwa ikiwa wangetubu na kumfuata Yesu, wangeweza kubatizwa.

Watu walipiga makofi kwa shangwe. Waliahidi kuwafariji wengine. Waliahidi kumpenda Mungu na kuwaeleza watu wengine kumhusu Yeye. Walikuwa tayari kubatizwa.





Mmoja baada ya mwingine, Alma aliwabatiza. Walikuwa watu wenye furaha sana kuwa sehemu ya Kanisa la Yesu.

Tunapobatizwa, tunatoa ahadi sawa na zile ambazo Alma na watu wake walitoa. Na sisi tunakuwa sehemu ya Kanisa la Yesu pia! ■

Kutoka Mosia 16–18.

Sabato ni Siku Maalum



KIELEZO NA APRYL STOTT



**Na Rais
George Q. Cannon
(1827–1901)**

Mshauri wa Kwanza
katika Urais wa Kwanza

KUTAFUTA KARAMA ZA KIROHO

Ni wangapi kati yenu wanatafuta karama hizi ambazo Mungu ameahidi kuteremsha?

Kila mwanaume na mwanamke katika Kanisa la Kristo anaweza kuwa na karama za Roho wa Mungu kulingana na imani yao na mapenzi ya Mungu. . . .

Ni wangapi kati yenu . . . wanatafuta karama hizi ambazo Mungu ameahidi kuteremsha? Ni wangapi kati yenu, ambao mnapomwinamia Baba yenu wa Mbinguni katika mzunguko wa familia au katika sehemu zenu za siri, mnapambana kwa ajili ya karama hizi ili ziteremshwe kwenu? Ni wangapi kati yenu mnamuomba Baba, katika jina la Yesu, ajidhihirishe kupitia nguvu hizi na karama hizi? Au mnaendelea siku hadi siku, kama mlango unavyozunguka kwenye bawaba zake, bila ya kuwa na hisia zozote kuhusu mada, bila ya kutumia imani yoyote, mkitosheka na kubatizwa na kuwa waumini wa Kanisa na kupumzika hapo, mkifikiria kuwa wokovu wenu upo salama kwa sababu mmefanya hivi? . . .



. . . Ninajua kuwa ni mapenzi yake Mungu kuwaponya wagonjwa, kuwa ni mapenzi Yake kuteremsha karama ya kuzitambua roho, karama ya hekima, ya maarifa na ya kutoa unabii, na karama zingine zinazoweza kuhitajika. Ikiwa yeyote kati yetu si wakamilifu, ni wajibu wetu kuomba tupate karama ambayo itatukamilisha. Je, mimi nina mapungufu? Niko nayo chungu mzima. Wajibu wangu ni nini? Kuomba kwake Mungu anipe karama ambazo zitasahihisha mapungufu haya. Ikiwa mimi ni mtu mwenye hasira, ni wajibu wangu kuomba ili niwe na hisani, ambayo huvumilia na ni karimu. Je, mimi ni mtu mwenye

wivu? Ni wajibu wangu kutafuta hisani, ambayo haina wivu. Na hivyo kwa karama zote za injili. Zimekusudiwa kwa lengo hili. Mtu yeyote hapa swi kusema, “Loo, siwezi kujizuia, ni maumbile yangu.” Hahalalishwi ndani yake, kwa sababu Mungu aliahidi kutoa nguvu kusahihisha mambo haya, na kutoa karama ambazo zitayatokomezwa. Kama mtu hana busara, ni wajibu wake kumwomba Mungu ampe busara. Vile vile kwa kila kitu kingine. Huo ndio mpango wa Mungu kuhusu Kanisa Lake. Anataka Watakatifu wake wakamilishwe katika ukweli. Kwa madhumuni haya Yeye hutoa karama hizi na kuwateremshia wale wanaozitafuta, ili wapate kuwepo watu wakamilifu usoni mwa ulimwengu, bila ya kujali udhaifu wao mwingi, kwa sababu Mungu ameahidi kutoa karama ambazo ni muhimu kwa ukamilifu wao. ■

Kutoka The Latter-day Saints Millennial Star, Apr. 23, 1894, 258–61; kuwekwa kwa vituo katika maandiko na herufi kubwa kama kiwango elekezi.

UMAIZI



Ni jinsi gani imani ya utotoni hukua na kuwa ufahamu na ushahidi?

“Siwezi kukumbuka wakati ambapo sikuwa nikiamini katika Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Nimewapenda tangu nilipojifunza juu Yao magotini mwa malaika mama yangu, akisoma maandiko na simulizi za injili. Ile imani ya utotoni sasa imekua na kuwa ufahamu na ushahidi wa Baba wa Mbinguni mwenye upendo, ambaye anasikia na kujibu maombi yetu.”

Mzee Ronald A. Rasband wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, “Ninashangaa Sana,” *Liahona*, Nov. 2015, 90.

Pia Katika Toleo Hili

KWA VIJANA WAKUBWA



Kutambua Vitu Bandia vya Shetani

uk.
44

Hapa kuna njia moja muhimu ya kutofautisha kati ya uongo wa Shetani na ukweli wa Bwana.

KWA VIJANA

HATA KAMA

UNAONA HAYA

uk.
60

Umewahi kuona haya sana kiasi cha kuogopa kushiriki injili na wengine? Hapa kuna mapendekezo matatu.



KWA WATOTO



Kuwafuata Manabii na Mitume

uk.
72

Ni jambo gani moja unaweza kufanya mwezi huu kumfuata nabii, Rais Thomas S. Monson?



KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO